JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

## HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI H. CHANA (MB), WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026



MEI, 2025

DODOMA

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. PINDI H. CHANA (MB), WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

# VIONGOZI WAKUU

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII



**Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb)**
**Waziri Maliasili na Utalii**



**Mhe. Dunstan L. Kitandula (Mb)**
**Naibu Waziri Maliasili na Utalii**



**Dkt. Hassan A. Said**
**Katibu Mkuu Maliasili na Utalii**



**Benedict M. Wakulyamba-CP**
**Naibu Katibu Mkuu Maliasili**



**Nkoba E. Mabula**
**Naibu Katibu Mkuu Utalii**

## YALIYOMO


**1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1**

**2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII ........................................................ 8**

**3.0 MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII ........................................................ 9**

**4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ........................ 17**

4.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ........................................ 19

4.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ........... 20

4.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ........................ 20

4.4 Miradi ya Maendeleo ............................................ 100

**5.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ...................... 112**

5.1 Ukusanyaji wa Maduhuli ........................................ 114

5.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ...... 114

5.3 Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake .... 115

5.4 Miradi ya Maendeleo ............................................ 146

**6.0 SHUKRANI ........................................................ 160**

**7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026 .................................................. 163**

**8.0 HITIMISHO ...................................................... 163**

**ORODHA YA VIAMBATISHO .................................... 164**

## ORODHA YA VIAMBATISHO

**Jedwali Na. 1**: Maduhuli ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 na Makusanyo kwa Mwaka 2024/2025 ............................ 165

**Jedwali Na. 2:** Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........................................................... 166

**Jedwali Na. 3:** Mwenendo wa Utalii Nchini kuanzia Mwaka wa Fedha 2020 hadi 2024 ............................................... 167

**Jedwali Na. 4:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025........................................ 167

**Jedwali Na. 5:** Mwenendo wa Uwindaji wa Kitalii na Mapato Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 ...... 168

**Jedwali Na. 6:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Mapori ya Akiba na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 ........................................................... 168

**Jedwali Na. 7:** Mwenendo wa Upandaji Miti katika Mashamba ya Miti Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 ........................................................... 169

**Jedwali Na. 8:** Mauzo ya Asali na Nta Nje ya Nchi kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025................... 170

**Jedwali Na. 9:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 .................................. 171

**Jedwali Na. 10:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 ........................................................... 171

**Jedwali Na. 11:** Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Malikale na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025 ........................................................... 172

**Jedwali Na. 12:** Idadi ya Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa na Mapato Kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 2024/2025 ........................................... 174

**Jedwali Na. 13:** Nafasi ya Tanzania kwa Idadi ya Wanyamapori Barani Afrika kwa Mwaka 2024 .................... 175

**Jedwali Na. 14:** Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa katika Vyuo vilivyo chini ya Wizara kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025. ............................................ 175

**Jedwali Na. 15:** Muhtasari wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026...................... 176

**Jedwali Na. 16:** Muhtasari wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ...................................................... 181

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| AfDB | - | African Development Bank |
| AWF | - | African Wildlife Foundation |
| AWHF | - | African World Heritage Fund |
| BEVAC | - | Beekeeping Value Chain Support |
| CAWM | - | College of African Wildlife Management |
| CBCTC | - | Community Based Conservation Training Centre |
| CBD | - | Convention on Biological Diversity |
| CCM | - | Chama Cha Mapinduzi |
| CITES | - | Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora |
| CMS | - | Convention on Migratory Species |
| COCOBA | - | Community Conservation Banks |
| DMI | - | Dar es Salaam Maritime Institute |
| ESQR | - | European Society for Quality Research |
| EU | - | European Union |
| FAO | - | Food and Agriculture Organization |
| FITI | - | Forest Industries Training Institute |
| FTI | - | Forestry Training Institute |
| FORVAC | - | Forestry and Value Chains Development Programme |
| FZS | - | Frankfurt Zoological Society |
| GEF | - | Global Environmental Facility |
| GIZ | - | Deutsche Gesellschaftf Ür Internationale Zusammenarbeit |
| GMP | - | General Management Plan |
| HACCP | - | Hazard Analysis and Critical Control Points |
| HEAT | - | Honey Exporters Association of Tanzania |
| ICCROM | - | International Centre for the Study of Preservation and Restoration of Cultural Property |
| ICOM | - | International Council of Museum |
| ICOMOS | - | International Council on Monuments and Sites |
| ILO | - | International Labour Organization |

| | | |
|---|---|---|
| IMF | - | International Monetary Fund |
| ITC | - | International Trade Centre |
| IUCN | - | International Union for Conservation of Nature |
| KfW | - | Kreditanstalt für Wiederaufbau (German Development Bank) |
| MoU | - | Memorandum of Understanding |
| MICE | - | Meetings, Incentives, Conferences and Exhibitions |
| MNRT | - | Ministry of Natural Resources and Tourism |
| MSY | - | Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza |
| NABAC | - | National Beekeeping Advisory Committee |
| NFA | - | National Fund for Antiquities |
| NAFAC | - | National Forestry Advisory Committee |
| NCAA | - | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| NCT | - | National College of Tourism |
| NMT | - | National Museum of Tanzania |
| NORAD | - | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| PAMs | - | Protected Area Management System |
| PWTI | - | Pasiansi Wildlife Training Institute |
| REGROW | - | Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth |
| SADC | - | Southern African Development Community |
| SHIMIWI | - | Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali |
| S!TE | - | Swahili International Tourism Expo |
| SWICA | - | Special Wildlife Investment Concession Area |
| TaFF | - | Tanzania Forest Fund |
| TAFORI | - | Tanzania Forestry Research Institute |
| TANAPA | - | Tanzania National Parks |
| TATO | - | Tanzania Association of Tour Operators |
| TAWA | - | Tanzania Wildlife Management Authority |
| TAWIRI | - | Tanzania Wildlife Research Institute |
| TCG | - | Task Coordinated Groups |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TFS | - | Tanzania Forest Services Agency |
| TNBC | - | Tanzania National Business Council |

| | | |
|---|---|---|
| TRA | - | Tanzania Revenue Authority |
| TTB | - | Tanzania Tourist Board |
| TWPF | - | Tanzania Wildlife Protection Fund |
| UNCCD | - | United Nations Convention to Combat Desertification |
| UNDP | - | United Nations Development Programme |
| UNESCO | - | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| UNFCCC | - | United Nations Framework Convention on Climate Change |
| UN Tourism | - | United Nations World Tourism Organization |
| UNPFII | - | United Nations Permanent Forum on Indegineous Issues |
| USAID | - | United States Agency for International Development |
| UVIKO-19 | - | Ugonjwa wa Virusi vya Korona 2019 |
| VVU | - | Virusi vya UKIMWI |
| VGS | - | Village Game Scout |
| WB | - | World Bank |
| WCS | - | Wildlife Conservation Society |
| WHC | - | World Heritage Centre |
| WHO | - | World Health Organization |
| WMAs | - | Wildlife Management Areas |
| WMF | - | World Monuments Fund |
| WTM | - | World Travel Market |
| WTTC | - | World Travel and Tourism Council |
| WWF | - | World Wildlife Fund |

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyopitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai, afya njema, usalama na amani katika Taifa letu na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kutekeleza jukumu letu la msingi la kuipokea na kuijadili taarifa ya Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Mwelekeo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kwa mara nyingine kusimamia Sekta ya Maliasili na Utalii. Naendelea kumuombea afya njema, hekima na nguvu zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa zaidi. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu, uwajibikaji, weledi na uzalendo mkubwa ili kuhakikisha kuwa sekta hii inazidi kuwa nguzo imara ya uchumi wa nchi yetu, huku tukihifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, ninaomba nitumie fursa hii tena kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri, wenye dira, hekima na maono ya maendeleo ya Taifa letu. Uongozi wake umeifanya nchi yetu kuendelea kupiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Aidha, nimpongeze kwa namna alivyoiongoza vyema Serikali ya Awamu ya Sita katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Sisi sote ni mashahidi wa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Maliasili na Utalii.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa wahenga wanasema: "***Chanda Chema Huvikwa Pete***" ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunawatakia kila la heri katika safari hii muhimu ya kulitumikia Taifa letu kwa uzalendo na dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo kwa Watanzania.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu ya kuliongoza Taifa letu. Kwa hakika, miongozo na maelekezo yake yamekuwa chachu katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya maendeleo na kuhakikisha maliasili zetu zinahifadhiwa na sekta ya utalii inaendelezwa kwa manufaa ya Taifa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za dhati katika kuimarisha uchumi na maendeleo ya Wananchi wa Zanzibar. Aidha, nampongeza kwa kupitishwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali. Uongozi wao madhubuti na maelekezo wanayotoa mara kwa mara yamewezesha kufanikisha uhifadhi endelevu wa rasilimali za Taifa na kuchochea ukuaji wa utalii nchini.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa, naomba nikupongeze wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara na hekima. Uongozi wako thabiti unaendelea kulifanya Bunge letu kuwa chombo imara cha kutunga Sheria, kuisimamia Serikali na kuwakilisha wananchi kwa ufanisi. Aidha, nikupongeze kwa kazi nzuri na ya mfano unayoendelea kuifanya katika Umoja wa Mabunge Duniani ambayo si tu inaitangaza Tanzania bali pia inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha majadiliano ya kidemokrasia na mshikamano wa Kimataifa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kukusaidia kwa umahiri mkubwa kuendesha shughuli za Bunge.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia niwapongeze Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini kwa umakini wao mkubwa katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuchukua fursa hii, nikizingatia kuwa "***Umoja Ni Nguvu***" kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Manaibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika kumsaidia kuwaletea Watanzania maendeleo kwa kasi kubwa zaidi. Aidha, ninawashukuru kwa namna wanavyoshirikiana na Sekta ya Maliasili na Utalii katika utekelezaji wa majukumu yake. Tunathamini sana mchango wao, kwa pamoja tutaendelea kujenga Taifa lenye nguvu na ustawi wa wananchi.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava (Mb.) Mwenyekiti; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) Makamu Mwenyekiti; na Wajumbe wa Kamati kwa michango, ushauri na miongozo wanayoendelea kutupatia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka huu wa Fedha sambamba na maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka ujao wa Fedha. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa ili kuhakikisha kuwa sekta hii inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sambamba na hilo, niwapongeze Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuongoza Kamati hizo kwa ufanisi katika kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri

wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuhakikisha uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na malikale pamoja na uendelezaji wa utalii nchini. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi ya kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhamira ya dhati kabisa na nikizingatia kauli ya kwamba "***Kidole Kimoja Hakivunji Chawa***", niwashukuru Viongozi wenzangu na Watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kujituma kwao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Uongozi wao thabiti umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii muhimu. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dunstan Kitandula (Mb.), Naibu Waziri kwa msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu; Kamishna wa Polisi, Benedict Wakulyamba, Naibu Katibu Mkuu (Maliasili); na Bwana Nkoba Mabula, Naibu Katibu Mkuu (Utalii) kwa weledi, umahiri na ufanisi wao katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** nawashukuru pia Wakurugenzi wa Idara, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA, Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro – NCAA, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania – TAWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga -

CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu – FWITC, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT na Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT pamoja na Watumishi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Ushirikiano wao, weledi na kujituma kumefanikisha kwa kiasi kikubwa malengo tuliyojiwekea. Kwa pamoja mmeonesha kuwa kazi ya timu ndiyo msingi wa mafanikio ya kweli.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** tunaaswa kuwa "***Mwenda Omo na Tezi Marejeo Ngamani*** basi kipekee kabisa, naishukuru familia yangu kwa namna wanavyonitia moyo na kuniombea ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Namuomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki na kuwalinda. Vilevile, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa ushirikiano na kutambua dhamana ya kitaifa niliyokabidhiwa. Nawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nanyi katika juhudi za kuleta maendeleo katika Mkoa wetu kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa ninaomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mheshimiwa Cleopa David Msuya. Tutaendelea kumkumbuka kwa umahiri wake mkubwa katika usimamizi na uwajibikaji katika kuleta maendeleo kwa Taifa. Kwa hakika, ametuachia hazina isiyomithilika katika uongozi wa weledi, ukimya na uzalendo kwa nchi yake.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba pia kutoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Ukanda wa Afrika. Kwa namna ya pekee, naungana na Watanzania wote kuwapa pole familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na mpendwa wetu.

***Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.***

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia pia hali inayoendelea nchini kutokana na matokeo ya uhifadhi na muingiliano wa binadamu na wanyamapori, kwa unyenyekevu mkubwa, ninatoa pole za dhati kwa ndugu, jamaa, marafiki na wananchi waliopoteza wapendwa wao kwa kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na wananchi ambao walijeruhiwa au mali zao kuharibiwa na wanyamapori hao katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kutekeleza mikakati thabiti na madhubuti ili kulinda usalama wa wananchi na mali zao. **Kwa pamoja tunaweza.**

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba pia kutambua mchango wa dhati wa Askari na Maafisa wa Jeshi la Uhifadhi ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ujasiri na weledi katika kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu zikiwemo wanyamapori, misitu, nyuki na malikale. Katika mwaka huu wa fedha, baadhi ya askari hawa shupavu, walipoteza maisha wakiwa kazini wakitimiza wajibu wao kwa Taifa na wengine walipata majeraha. Mashujaa wetu CR III Arafat Saidi Miyimba kutoka TANAPA; Askari wa Vijiji (VGS) Bwana Issa Manyinja wa WMA ya Magingo Wilaya ya Liwale; Bwana Masanja Michael wa WMA ya Uyumbu Wilaya ya Urambo; Bwana Felician Isdory

Mgomela; Bwana Shakimu Mohamed na Bwana Boliva Betram Mapunda kutoka TFS walipoteza maisha. Aidha, askari wengine 46 kutoka taasisi za uhifadhi za TANAPA, NCAA, TAWA na TFS walijeruhiwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Matukio haya yalitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kushambuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na majangili waliovamia maeneo ya hifadhi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za marehemu wapendwa wetu mahali pema peponi, Amina.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

**23.** ***Mheshimiwa Spika***, maelekezo ya mgawanyo wa majukumu yaliyotolewa na Hati Idhini ya Rais (Presidential Instrument) ya tarehe 30 Agosti, 2023 kupitia Tangazo la Serikali Namba 619A yanaainisha majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo mbalimbali inayolenga uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki, malikale na maendeleo ya utalii;

(ii) Kusimamia ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu kwa kufanya doria ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu;

(iii) Kujenga uwezo wa Sekta ya Maliasili na Utalii ili iweze

kusimamia rasilimali za maliasili na malikale, kuendeleza utalii, kufanya tafiti na kutoa mafunzo kupitia vyuo vilivyo chini ya Wizara;

(iv) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili, utalii na malikale;

(v) Kushirikisha wadau mbalimbali katika utunzaji na uhifadhi wa maliasili na malikale kwa kutoa elimu na huduma za ugani; na

(vi) Kukuza na kuendeleza mazao ya utalii, kuimarisha utangazaji na kuboresha huduma za utalii kwa lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa.

## 3.0 MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII


**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri na shupavu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Muongoza Watalii Namba Moja nchini, Serikali imeendelea kutekeleza masuala mbalimbali katika sekta za uhifadhi na utalii na hakika tumeshuhudia mageuzi makubwa na mafanikio ya hali ya juu katika miaka hii minne na mwaka mmoja huu wa utekelezaji wa Bajeti. Nitumie fursa hii kuainisha kwa muhtasari **MAFANIKIO 10 YA KIHISTORIA** yaliyopatikana kutokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Maliasili na Utalii kama ifuatavyo:-

### (i) Kuongezeka kwa idadi ya watalii

Idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kwa **asilimia 132.1** kutoka watalii **922,692** Mwaka 2021 hadi watalii **2,141,895**

Mwaka 2024. Aidha, idadi ya watalii wa ndani waliotembelea vivutio vya utalii imeongezeka kwa **asilimia 307.9** kutoka watalii **788,933** Mwaka 2021 hadi kufikia watalii **3,218,352** mwaka 2024. Hatua hii imewezesha idadi ya watalii kufikia **5,360,247** sawa na **asilimia 107.2** ya lengo la watalii **5,000,000** kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2020.

Kwa rekodi hizo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii (UN Tourism), limeitaja Tanzania kuwa nchi ilizoongoza Afrika kwa mwaka 2024 kwa kuwa na ongezeko kubwa la watalii ikilinganishwa na kabla ya janga la UVIKO-19 ambapo utalii Tanzania ulikua kwa asimilia 48, Ethiopia (40%), Morocco (35%), Kenya (11%) na Tunisia (9%). Haya ni matokeo yaliyochagizwa na maono na kujitoa kwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika filamu za ***Tanzania: The Royal Tour*** na ile ya ***Amazing Tanzania***.




*Best Performing Destinations in Africa 2024 - International Tourist Arrivals % Change Over 2019 (UN Tourism - April, 2025)*

### (ii) Kuongezeka kwa Mapato Yatokanayo na Shughuli za Utalii

Mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani **bilioni 1.3** Mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani **bilioni 3.9** Mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 200** kwa watalii wa kimataifa. Aidha, mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka Shilingi

**bilioni 46.3** Mwaka 2021 hadi Shilingi **bilioni 209.8** Mwaka 2024 sawa na ongezeko la **asilimia 353.1**. Hatua hii imeifanya Tanzania kuwa nafasi ya tisa (9) duniani na kushika nafasi ya tatu (3) Barani Afrika kwa ongezeko la mapato ikilinganishwa na hali ilivyokuwa kabla ya UVIKO-19.

### (iii) Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

Maduhuli ya Serikali yaliongezeka kutoka Shilingi **397,428,671,968.00** Mwaka 2020/2021 hadi Shilingi **901,088,264,662.24** Mwaka 2023/2024. Vilevile, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kuanzia Julai 2024, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 912,900,341,299.80** sawa na **asilimia 94.2** ya lengo la makusanyo.

### (iv) Tanzania Imeendelea Kutambulika na Kung'ara Kimataifa

Tanzania imeendelea kung'ara kwa kushinda Tuzo mbalimbali za utalii katika nyanja za Kimataifa. Hatua hiyo imedhihirishwa kwa mafanikio ya kishindo kwa kupata Tuzo maarufu Duniani za *World Travel Awards – WTA* zinazotolewa na taasisi ya *World Luxury Media Group Limited* ya nchini Uingereza katika msingi wa kutambua na kutangaza ubora wa vivutio na huduma za utalii, ambapo Tanzania imeshinda Tuzo saba (7) za Kimataifa ambazo ni: Eneo linalovutia zaidi kiutalii (Africa's Leading Destination, 2024); Eneo linaloongoza kwa utalii wa safari (World's Leading Safari Destination, 2024); Hifadhi ya Taifa Serengeti kuendelea kuwa bora Duniani kwa miaka sita (6) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2024; Mlima Kilimanjaro kuwa kivutio bora cha utalii barani Afrika (African Leading Tourism Attraction, 2024); Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kutambuliwa kama eneo la pili bora zaidi duniani kwa

safari na utalii na gazeti la *The Times of India* (World's Second-Best Destination by Times of India, 2024); Utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa iliyotolewa na Shirika la Utafiti wa Ubora (European Society for Quality Research – ESQR), ambapo TANAPA imeshinda kwa mara ya tano mfululizo kuanzia mwaka 2020 hadi 2024; na Bodi ya Utalii kushinda Tuzo ya Bodi Bora Afrika. Tuzo hizi zimeendelea kuwa chachu ya kujitangaza na kutambulika katika majukwaa ya kimataifa na kuchagiza ongezeko la idadi ya watalii wanaotembelea nchini. Kwa upande mwingine, Tanzania imepewa hadhi ya kuwa mwenyeji wa Tuzo za *World Travel Awards* kwa Kanda ya Afrika zitakazotolewa mwezi  Juni, 2025.




*Kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii,  Mhe. Dunstan Kitandula (Mb) wakifurahia tuzo ambayo Tanzania ilishinda kama eneo linaloongoza kwa utalii wa safari Duniani. Kulia ni baadhi ya tuzo zilizopokelewa kwa mwaka 2024.*

## (v) Kuimarika kwa Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Wanyamapori

Kupitia mikakati madhubuti ya kudhibiti ujangili, kuimarisha doria na matumizi ya teknolojia tumeshuhudia ongezeko la idadi ya wanyamapori na hali ya usalama katika maeneo ya hifadhi kuliko wakati wowote katika historia yetu. Kwa mujibu wa tafiti za mashirika ya kimataifa kama IUCN na Taasisi yetu ya Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), nchi yetu Tanzania imeendelea kuongoza Afrika na duniani kwa kuwa na simba

wapatao 17,000; lakini pia ikiongoza Afrika kwa nyati 225,000 na chui 24,000. Vilevile, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya faru weusi imeongezeka kutoka faru 163 Mwaka 2021 hadi 263 mwaka 2025 sawa na ongezeko la asilimia 61. Sambamba na hilo, takwimu zinaonesha matukio ya ujangili wa tembo yamepungua kwa takriban asilimia 90.

### (vi) Kuimarika kwa Biashara ya Mazao ya Misitu na Nyuki

Serikali imeendelea kushuhudia kuimarika kwa biashara ya mazao ya misitu na nyuki nchini. Kuimarika kwa biashara hii kunatokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi. Katika kipindi cha miaka mitano (5), kumekuwa na ongezeko la kiwango cha uzalishaji wa malighafi mbao katika mashamba ya Serikali yanayolimwa miti kibiashara kutoka mita za ujazo 1,108,791 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia mita za ujazo 1,264,535 mwaka wa fedha 2024/2025. Vilevile, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu vimeongezeka kutoka viwanda vya kati na vikubwa 636 mwaka 2020 hadi kufikia 1,671 mwaka 2025 na viwanda vidogo vidogo kama useremala zaidi ya 7,000. Sambamba na hilo, thamani ya mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi imeongezeka kufikia Shilingi 458,474,543,027.45 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 333.8 ikilinganishwa na Shilingi 105,689,957,500.00 mwaka 2020/2021.

Kwa upande mwingine, Wizara imewezesha ujenzi wa viwanda vya kati na vikubwa vya kuchakata na kuongeza thamani mazao ya nyuki na kufanya idadi ya viwanda hivyo kuongezeka kutoka kiwanda kimoja (1) mwaka 2020 hadi kufikia viwanda nane (8) mwaka 2025. Viwanda hivi vimejengwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Iringa, Katavi na Geita. Hadi

kufikia Aprili 2025, jumla ya tani 1,321.35 za asali zenye thamani ya shilingi 15,856,164,000.00 zimeuzwa nje ya nchi sawa na asilimia 206.9 ikilinganishwa na kiasi cha tani 430.61 zenye thamani ya Shilingi 5,167,332,000.00 zilizouzwa nje ya nchi kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Kwa maendeleo haya, Shirika la Wafugaji Nyuki Duniani limeiteua Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wafugaji nyuki duniani (APIMONDIA) mwaka 2027, utakaohudhuriwa na watu zaidi ya 4,000 kutoka sehemu mbalimbali za dunia.

**(vii) Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro Kurejeshewa Hadhi ya Hifadhi ya Jiolojia ya Ngorongoro Lengai (UNESCO Global Geopark)**

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro limerejeshewa hadhi ya hifadhi ya jiolojia ya Ngorongoro Lengai (UNESCO Global Geopark). Mwaka 2022, eneo hili lilikua kwenye orodha ya hifadhi za jiolojia zilizopoteza hadhi, hata hivyo mwezi Desemba 2024 lilirejeshewa hadhi yake kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ikiwemo kuimarisha shughuli za uhifadhi katika maeneo ya urithi wa jiolojia, kutangaza pamoja na kufuata masharti na miongozo ya UNESCO katika kulinda hadhi ya eneo hilo. Hadhi hii itaongeza thamani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, idadi ya watalii na watafiti watakaotembelea Tanzania kwa shughuli mbalimbali pamoja na kuongeza idadi ya vivutio vya utalii hususan utalii wa miamba.

**(viii) Mafanikio ya 4R za Rais Samia Katika Kukuza Biashara ya Utalii kwa Kuiwezesha Sekta Binafsi**

Katika kipindi hiki, Wizara imefanikiwa kuanza kutekeleza hatua madhubuti na za kimkakati za kusaidia sekta binafsi iweze

kukua katika sekta ya utalii kwa kupunguza na kuondoa tozo na kero zilizokuwa zinawakwaza wadau kama ifuatavyo:-

a) Kufanya mabadiliko ya viwango vya Ada ya Leseni ya Biashara za Utalii (TTBL) kwa ajili ya wawekezaji wazawa wa huduma za malazi zilizopangwa katika daraja za ubora na zile ambazo hazijapangwa katika daraja kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji. Mathalan, Wizara imepunguza: *Daraja la Nyota 5 kutoka USD 2,500 hadi USD 1500; Daraja la Nyota 4 kutoka USD 2,000 hadi USD 1000; Daraja la Nyota 3 kutoka USD 1,500 hadi USD 500; Daraja la Nyota 2 kutoka USD 1,200 hadi USD 300; Daraja la Nyota 1 kutoka USD 1,000 hadi USD 200*. Gharama hizi sasa zinalipwa kwa shilingi ya Tanzania;

b) Kufuta malipo ya waongoza watalii (park fees) walizokuwa wakitozwa kila walipokuwa wakiingia hifadhini kuingiza wageni. Sasa kila muongoza watalii mwenye leseni hai na halali hatatozwa chochote; na

c) Kuanza kutekeleza punguzo la ada ya Wakala wa kupandisha mlima kutoka Dola za Marekani 2000 hadi shilingi za Tanzania milioni tatu (3,000,000). Aidha, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la gharama ya leseni ya waongoza watalii (TTBL) kutoka Dola za Marekani 50 hadi Shilingi 35,000 tu kwa mwaka.

Wizara na Serikali kwa ujumla itaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi katika kuongeza ufanisi wa sekta za uhifadhi na utalii kupitia vikao vya kisekta chini ya TNBC pamoja na mikutano ya mara kwa mara na wadau.

### (ix) Kuandaa Tuzo za Kwanza za Uhifadhi na Utalii

Katika kutambua na kuhamasisha wadau kuendeleza uhifadhi na utalii, Wizara imezindua tuzo maalum zilizojulikana kama *The Serengeti Awards* zenye lengo la kutambua mchango wa wadau katika kuendeleza uhifadhi na kutangaza utalii. Uzinduzi wa tuzo hii ulifanyika Disemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 500 ambapo miongoni mwa watu mashuhuri waliopata Tuzo ni: Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan (**Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono yaani Visionary Leadership Award**); Mhe. Zakia Hamdani Meghji, Waziri wa zamani wa Maliasili na Utalii na familia ya mgunduzi mashuhuri duniani wa zamadamu Louis na Mary Leakey. Tuzo hizi zitaendelea kuimarishwa na kutolewa kila mwaka ili kuendelea kuhamasisha na kutambua michango mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Maliasili na Utalii.

### (x) Mafanikio ya Mikakati Mahsusi ya Kutangaza Utalii

Katika kutekeleza mikakati ya kutangaza utalii kwa njia tofauti na kuyafikia masoko mapya zaidi ya yale yaliyozoeleka, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo Balozi zetu za India na China pamoja na Kamati ya Rais ya Kuitangaza Tanzania, ilifanya mikakati mahsusi miwili. Kuhusu China: Kama mnavyojua mbali na Royal Tour, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi, walishiriki filamu nyingine tena na mcheza filamu mashuhuri wa China Bw. Jin Dong iitwayo *Amazing Tanzania*. Filamu hii baada ya kuzinduliwa Mei, 2024 kule Beijing ilizinduliwa tena hapa nchini jijini Dar es Salaam Novemba mwaka 2024 na inaendelea kutazamwa. Tayari filamu hiyo

imesababisha watalii kutoka China kuongezeka kutoka 45,463 kwa mwaka 2023 hadi kufikia 71,140 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56.5. Aidha, filamu hii ilichagiza waandaaji wa kipindi maarufu nchini China kinachohusisha mastaa cha *Divas Hit the Road* kuja nchini na kuonesha zaidi utalii wetu ambapo baada ya kipindi kuoneshwa kupitia Televisheni ya *Hunan* na mitandao ya kijamii, kilitazamwa na watu takriban bilioni 1.2 ndani ya China na nchi za jirani. Juhudi kama hizo pia zimechochea ongezeko la idadi ya watalii kutoka soko la kimkakati la India kufikia 63,391 mwaka 2024 kutoka 54,558 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16.2.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio haya, kwa uchache, yanadhihirisha uthubutu na weledi wa Serikali ya Awamu ya Sita na yanaonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa chachu ya mabadiliko chanya katika kulinda, kuendeleza na kutumia kwa tija rasilimali zetu za Taifa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na umahiri mkubwa huku akizingatia falsafa yake ya maridhiano, mabadiliko, ustahimilivu na kujenga upya kwa kuzingatia utawala bora na kuchochea maendeleo kiuchumi na kijamii. Huyu ni "**Chanda Chema Tunastahili Kumvika Pete**."

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa dhamana ya kusimamia kisheria maeneo yenye ukubwa wa kilometa za mraba takriban 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la Nchi. Maeneo haya yanajumuisha Hifadhi za Taifa 21, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya

Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 40 ambapo kati ya hizo 26 zimeidhinishwa na 14 ziko kwenye hatua mbalimbali za kuidhinishwa, maeneo 3 ya Ardhioevu chini ya Mkataba wa Ramsar, Hifadhi za Misitu ya Asili 464, Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia 25, Mashamba ya Miti ya Serikali 24, Hifadhi za Nyuki 14, Maeneo ya Malikale 142 na Makumbusho za Taifa 7.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo ya hifadhi za wanyamapori, misitu, nyuki, fukwe na malikale yana mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi, urithi wa utamaduni na ukuaji wa uchumi kitaifa na kimataifa. Sekta ya Maliasili na Utalii inachangia asilimia 21.5 katika Pato ghafi la Taifa ambapo asilimia 17.2 ni utalii na asilimia 4.3 ni misitu na nyuki. Aidha, Sekta hii inachangia asilimia 30.9 ya mapato ya fedha za kigeni ambapo asilimia 25 yanatokana na utalii; na asilimia 5.9 misitu na nyuki; na kuajiri watu takriban milioni 3.6 wenye ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, maeneo ya hifadhi pia ni vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe hai wengine. Vilevile, sehemu kubwa ya Watanzania katika maeneo ya vijijini hutegemea rasilimali hizo kwa ajili ya kujikimu.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2024/2025, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba sasa kuwasilisha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 4.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 968,842,018,480.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 755,422,955,480.00** zinakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia TRA; na **Shilingi 213,419,063,000.00** zinakusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya mapato kutoka Idara, Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale - NFA na Taasisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi - PWTI, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii Likuyu Sekamaganga - CBCTC, Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI, Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora - BTI, Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI, Bodi ya Utalii Tanzania - TTB, Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT na Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania - NMT kupitia mfumo wa *MNRT Portal*.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 912,900,341,299.80** sawa na **asilimia 94.2** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 730,734,560,183.53** zimekusanywa na Wizara kutokana na vyanzo vya Taasisi za TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **Shilingi 182,165,781,116.27** zimekusanywa na Wizara kutokana na Idara, Mifuko na Taasisi zake kupitia mfumo wa *MNRT Portal*.

## 4.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 708,891,841,026.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 532,499,328,026.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 176,392,513,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 540,281,908,764.35** sawa na asilimia **76.2**. Fedha hizi zinajumuisha Fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 436,384,697,790.06** na Fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi 103,897,210,974.29.** Katika fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa, **Shilingi 247,635,129,105.04** ni fedha za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 188,749,568,685.02** ni Mishahara.

## 4.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

### 4.3.1 Sekta ya Wanyamapori

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Wanyamapori ina dhamana ya kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya utafiti wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Sekta hii inasimamia Hifadhi za Taifa 21, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mapori ya Akiba 29, Mapori Tengefu 23, maeneo 3 ya ardhioevu na bustani 5 za wanyamapori zinazomilikiwa na Serikali. Vilevile, sekta hii inaratibu shughuli za uhifadhi katika maeneo 40 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, mashamba 5 ya ufugaji wa wanyamapori, bustani 41 za wanyamapori, maeneo 30 ya uzalishaji wa wanyamapori (captive wildlife breeding facilities) pamoja na ranchi 5 za sekta binafsi.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa majukumu ya sekta ya wanyamapori hufanywa na Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Aidha, utekelezaji wa majukumu hayo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya Mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura ya 283; Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura ya 282; Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura ya 284; Sheria ya Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Sura ya 209; na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura ya 260.

#### 4.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetunga Kanuni za Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi katika maeneo ya Hifadhi za wanyamapori (Mapori ya Akiba na Tengefu) zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 781 la mwaka 2024; Kanuni za Biashara za Nyara zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 884 la mwaka 2024, na Kanuni za Utalii wa Picha zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 875 la mwaka 2024. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii zilizotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 780 la mwaka 2024 na Kanuni za Usimamizi wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) za mwaka 2018. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa Mipango ya Jumla ya Usimamizi wa Rasilimali za Wanyamapori (General Management Plan) ya Jumuiya za ISAWIMA (Kaliua), Ifinga (Madaba), Uyumbu (Urambo), na UKUTU (Morogoro). Katika hatua nyingine, Wizara imeandaa Mwongozo wa upatikanaji wa mazao ya wanyamapori na mimea inayosimamiwa na Mkataba wa CITES ili kuimarisha

utekelezaji wa mkataba huo. Kanuni hizi zinalenga kuimarisha uhifadhi shirikishi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Usimamizi wa Utatuzi wa Migongano kati ya Binadamu na Wanyamapori. Katika kutekeleza Mkakati huo, Wizara kupitia TAWA, TANAPA na TAWIRI imekamilisha ujenzi wa vizimba 12 vya kudhibiti mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya za Bunda (3), Korogwe (1), Ludewa (2), Uvinza (2), Tandahimba (2), Nanyumbu (1) na Mkinga (1). Vilevile, ujenzi wa vizimba sita (6) unaendelea katika Wilaya za Buchosa (2), Sengerema (1), Bunda (1), Newala (1) na Kibiti (1). Vizimba hivyo vitasaidia kuimarisha usalama wa wananchi wanaotumia maji ya mito na maziwa katika maeneo hayo.



*Kizimba cha kuzuia mamba na viboko kilichojengwa katika Kijiji cha Kwaisewa, Wilaya ya Korogwe.*

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara imekamilisha ujenzi wa mabwawa 10 katika Hifadhi za Taifa Nyerere (2), Tarangire (3), Mikumi (1) na Serengeti (2); Pori la Akiba Rungwa (1); na Makuyuni Wildlife Park (1) pamoja na kisima kimoja katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi. Aidha, ujenzi wa mabwawa mengine saba (7) unaendelea katika Mapori ya Akiba

Selous – Liwale (1), Rungwa (1), Muhesi (2), Kizigo (2) na Msanjesi (1). Miundombinu hii itasaidia kupunguza matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu hasa kipindi cha kiangazi ambapo baadhi ya wanyamapori hutoka nje ya hifadhi kutafuta maji na chakula.




*Bwawa la maji katika Pori la Akiba Rungwa.*

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutumia teknolojia za kisasa kufuatilia mienendo ya wanyamapori, ikiwemo tembo kwa kuwafunga Mikanda Maalum ya Mawasiliano (GPS - Satellite Collars) ili kupata taarifa za moja kwa moja zinazoonyesha mienendo yao na kuwadhibiti kabla hawajasababisha madhara kwa binadamu. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau imenunua Mikanda Maalum ya Mawasiliano (GPS - Satellite Collars) 54. Mikanda hii imefungwa kwa tembo viongozi wa makundi 45 katika Mifumo Ikolojia ya Serengeti (2), Burigi-Chato-Ibanda-Rumanyika (6), Mkomazi-Handeni (7), Moyowosi-Kigosi (11), Ruaha-Rungwa (4), Tarangire-Manyara (5) na Nyerere-Selous-Mikumi (10). Aidha, simba watatu (3) na mbwa mwitu sita (6) wamefungwa mikanda ya mawasiliano katika Mfumo Ikolojia Selous-Nyerere-Mikumi. Vilevile, Wizara imenunua ndege nyuki (drones) 17 na mabomu baridi 12,072 kwa ajili ya kuwadhibiti tembo katika maeneo yenye changamoto. Aidha, taratibu za manunuzi za ndege nyuki (drones) 18 na mabomu baridi 4,512 zinaendelea. Matumizi ya teknolojia hizo yamewezesha kupata taarifa kwa haraka na kurejesha makundi ya tembo kwenye hifadhi.




*Kushoto ni Askari wa Uhifadhi akijiandaa kurusha Ndege nyuki (drone) inayotumika katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika makazi ya watu na kulia ni ndege nyuki ikiwa imerushwa.*

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara kupitia TANAPA na NCAA imekamilisha ujenzi wa vituo vinne (4) vya askari wa uhifadhi wa wanyamapori katika Wilaya za Korogwe, Same, Namtumbo na Ruangwa. Aidha, ujenzi wa vituo sita (6) katika wilaya za Bunda, Serengeti, Bariadi, Kalambo, Kilwa na Mbarali unaendelea. Sambamba na ujenzi wa vituo hivyo, Wizara kupitia TAWA imeendelea kuweka vituo vya muda vya askari kwenye maeneo yenye changamoto kubwa ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wanyamapori kwa haraka katika Wilaya 40 zikiwemo Manyoni, Itigi, Morogoro Vijijini, Chalinze, Meatu, Bariadi, Itilima, Buchosa, Tunduru, Liwale, Kaliua, Nachingwea, Handeni, Simanjiro na Babati. Hatua hii itasaidia katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa haraka katika maeneo mbalimbali nchini.




*Kushoto ni Kituo cha Askari katika Kijiji cha Machang'anja, Wilaya ya Ruangwa na kulia ni Kituo cha Askari katika kijiji cha Mheza, wilayani Same.*

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori, Wizara imeajiri askari 542 na kuwapanga kwenye vituo mbalimbali kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ikiwemo kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa uhifadhi, inaendelea kuimarisha uwezo wa jamii katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutoa mafunzo mbalimbali ikiwemo matumizi ya mabomu baridi kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 214 kutoka Halmashauri za Wilaya 40 zikiwemo Babati, Bunda, Ikungi, Karatu, Korogwe, Ludewa, Makambako, Makete, Mbarali, Mkinga, Monduli, Itilima, Manyoni, Chalinze, Lindi, Mvomero, Mwanga, Nachingwea, Njombe, Same, Serengeti na Wanging'ombe. Mafunzo haya yameongeza ufanisi na uwezo wa jamii katika kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu, hivyo kupunguza madhara kwa binadamu na mali zao. Vilevile, Wizara kupitia TAWA imeendelea kuwashirikisha VGS 184 na vikundi vya ulinzi shirikishi 230 katika kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo mbalimbali nchini.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo maalum kwa wakufunzi 170 kutoka Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Itigi, Wanging'ombe, Mbarali na Iringa pamoja na kutoa elimu kwa wananchi 635,228 katika vijiji 945 vinavyopakana na maeneo ya hifadhi. Sambamba na hilo, Wizara imetoa semina kwa Maafisa Wanyamapori 122 wa Wilaya, Makatibu 50 wa Kamati za Kudumu za Bunge na wadau wengine wa uhifadhi. Vilevile, Wizara imenunua pikipiki 49 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uhifadhi kwa Maafisa Wanyamapori wa Wilaya (22), WMA (7) na pikipiki 20 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye kanda 10 za kiikolojia za kupambana na ujangili. Juhudi hizi zimesaidia kujenga uelewa na kuimarisha ulinzi na udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya wananchi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara kupitia Taasisi zake za uhifadhi, ilifanikiwa kudhibiti matukio 4,012 ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, katika jitihada za kuokoa maisha ya wananchi na mali zao wakati wa kudhibiti matukio tajwa, wanyamapori wakali na waharibifu 296 walivunwa wakiwemo mamba 63, viboko 63, tembo 34, nyati 15, fisi 71, simba 10 na chui mmoja (1). Vilevile, simba 10 walihamishwa kutoka eneo la Kijiji cha Mdori na kupelekwa katika Mapori ya Akiba Rungwa (6) na Pande (4); nyani 90 waliondolewa Geita mjini na kupelekwa Msitu wa Hifadhi Kigosi; na Chui watatu (3) waliondolewa kijiji cha Nyichoka na kuhamishiwa Hifadhi ya Taifa Serengeti (1) na Bustani ya Wanyamapori Ruhila (2). Katika hatua nyingine, Wizara imelipa kiasi cha Shilingi 4,604,909,750 ikiwa ni kifuta jasho na machozi kwa wananchi 16,939 walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu kwa matukio yaliyotokea katika kipindi cha mwaka 2021 hadi kufikia Aprili, 2025 katika Halmashauri za Wilaya 78. Aidha, Wizara inaendelea na malipo ya kifuta jasho na machozi kiasi cha Shillingi 1,082,049,500 kwa wananchi 5,542 wa Halmashauri za Wilaya 18. Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali ili kuhakikisha uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu unadhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Nitoe rai kwa wadau wote kuiunga mkono Serikali katika jitihada hizi.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na uratibu wa kuongoa maeneo ya kimkakati ya uhifadhi ikiwemo eneo la Ghuba ya Speke na Bonde la Mto Kilombero ili kuwezesha ustahimilivu wa mifumo ikolojia ya Serengeti-Mara na Nyerere-Selous-Niassa. Hadi Aprili, 2025, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi 61,863,151,045.85 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliopisha uhifadhi katika maeneo ya Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Kilombero na Hifadhi ya Taifa Mahale. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 53,234,754,978.85 zimelipwa kwa kaya 3,493 na kuhamisha makaburi 618 katika Kata ya Nyatwali

iliyopo eneo la Ghuba ya Speke Wilaya ya Bunda Mkoa wa Mara; Shilingi 1,681,882,027.00 zimelipwa kwa kaya 205 zilizofanyiwa uthamini katika kijiji cha Kalilani kilichopo Wilaya ya Uvinza Mkoa wa Kigoma na Shilingi 6,783,714,589.20 zimelipwa kwa kaya 998 na kuhamisha makaburi 107 ya Kijiji cha Ngombo kilichopo katika Pori la Akiba Kilombero. Kiasi cha Shilingi 137,929,949.02 kwa ajili ya kuhamisha makaburi 26 na kaya 52 za kijiji cha Ngombo wahusika hawakujitokeza hata hivyo Serikali imeendelea kutoa matangazo ya kuhamasisha wananchi hao wajitokeze.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022–2026. Mpango huu unatekelezwa kwa ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Rais–TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Maji; Wizara ya Ujenzi; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi imefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kukamilisha Mwongozo wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori Nchini ambao unaainisha hatua mbalimbali za kuzingatiwa wakati wa kuongoa shoroba hizo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la STEP imekamilisha kazi ya kuongoa ushoroba wa Udzungwa-Nyerere ambao umetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 226 la tarehe 04 Aprili, 2025. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa viongozi na wananchi katika Manispaa ya Singida na Wilaya za Mkalama na Monduli ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya kusimika mabango 20 katika shoroba zilizopo katika maeneo hayo ili kutoa tahadhari kwa wananchi kuhusu uwepo wa shoroba za wanyamapori kwa lengo la kupunguza migongano na kuimarisha ustawi wa jamii katika maeneo hayo.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kusimamia Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori – WMAs wa Mwaka 2023 - 2033 kwa lengo la kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za wanyamapori. Hadi Aprili 2025, tathmini ya maeneo mapya yaliyopendekezwa kwa ajili ya kuanzisha Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori imekamilika katika maeneo manne (4) ikijumuisha Mawima (Uvinza), Ifinga (Madaba), Minyughe (Ikungi), na Ndonda (Nachingwea na Nanyumbu). Sambamba na hilo, Wizara imewajengea uwezo viongozi 312 wa WMA 12 zilizopo katika Ukanda wa Magharibi na Kusini kuhusu usimamizi na uendelezaji wa jumuiya hizo ili kuimarisha uhifadhi na maendeleo ya wananchi. Aidha, Wizara imefanya tathmini na ufuatiliaji wa utendaji kazi wa Jumuiya 12 za Mbarang'andu, Kimbanda, Kisungule (Namtumbo); NALIKA, Chingoli (Tunduru); Magingo (Liwale); MUNGATA na Juhiwangumwa (Rufiji); Uyumbu (Urambo); Ipole (Sikonge); Mpimbwe (Mpimbwe); na ISAWIMA (Kaliua) za Ukanda wa Kusini na Magharibi kwa lengo la kubaini changamoto zinazozikabili na namna ya kuzitatua.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na ujangili nchini, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa mwaka 2023-2033 kwa kuratibu doria maalum zinazoongozwa na taarifa fiche kupitia Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili kwenye mifumo Ikolojia mbalimbali nchini na maeneo ya mpakani kati ya Tanzania, Kenya na Zambia. Doria maalum hizi zimewezesha kukamata jumla ya watuhumiwa 66, vipande 68 vya meno ya tembo, magamba 546 ya kakakuona, kobe 132, kenge 13 na aina mbalimbali ya mijusi 213 iliyokuwa ikisafirishwa kwenda nje ya nchi, bunduki mbili (2) na risasi 18 zilizokuwa zikitumika kwenye matukio ya ujangili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Uhifadhi imefanikiwa kuingiza mada zinazohusiana na masuala ya biashara haramu ya nyara kwenye mitaala inayotumika kufundishia vyuo vya Jeshi la Polisi

nchini. Utaratibu huu umeimarisha uwezo wa Askari na Maafisa wa Jeshi la Polisi katika utambuzi wa nyara na mbinu mbalimbali zinazotumiwa na wahalifu katika usafirishaji haramu wa nyara na mbinu za kukabiliana na vitendo hivyo.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa, Wizara iliandaa Mkutano wa 14 wa Baraza la Usimamizi wa Mkataba wa Lusaka uliofanyika tarehe 06 hadi 08 Mei, 2025 Jijini Arusha. Mkutano huu ulihudhuriwa na washiriki 51 kutoka nchi 5 za Tanzania, Kenya, Zambia, Congo na Sudani Kusini pamoja na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNEP, UNODC na AWF. Mkutano huo umewezesha nchi wanachama kubadilishana uzoefu katika kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu wa wanyamapori na misitu unaovuka mipaka. Aidha, Mkutano huu umechagua safu mpya ya uongozi kwa kipindi cha miaka miwili (2) ijayo ikiwajumuisha, Rais ambaye ni Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi H. Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Rosalie Matondo, Waziri wa Uchumi na Misitu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.






*Picha ya kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akikabidhiwa Hati ya Mkataba wa Lusaka na Waziri wa Utalii na Wanyamapori wa Jamhuri ya Kenya na Rais wa Baraza la 13 la Uongozi, Mhe. Rebecca Miano ikiwa ni ishara ya kukabidhi kijiti cha Urais wa Baraza kwa Mhe. Balozi Chana na Picha ya kulia ni Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akimkabidhi kinyago cha faru Mhe. Miano ikiwa ni ishara ya kupokea kijiti cha nafasi ya Urais wa Baraza la Usimamizi la Mkataba wa Lusaka katika Mkutano wa 14 wa Baraza hilo.*

#### 4.3.1.2 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umewezesha utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Doria maalum za kuzuia ujangili zinazotekelezwa na Kikosi Kazi Taifa Dhidi Ujangili, kuidadi wanyamapori nchi nzima; vyuo vya mafunzo kutekeleza majukumu yake; utatuzi wa migogoro baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishaji hadhi maeneo ya hifadhi; uanzishaji na uendelezaji wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwa jamii (WMAs); utoaji elimu ya uhifadhi kwa wananchi; uratibu wa uhifadhi wa faru nchini; uongoaji wa shoroba za wanyamapori; utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia katika Sekta ya Wanyamapori; kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu na kulipa kifuta jasho na kifuta machozi.

#### 4.3.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa lengo la kuboresha uhifadhi, kuimarisha mahusiano na jamii na kuendeleza miundombinu ya utalii. Hadi kufikia Aprili 2025, Shirika limefanya doria 36,411 ambapo watuhumiwa 3,450 wa makosa mbalimbali ya ujangili walikamatwa. Aidha, silaha 43 (shortgun 10 na gobore 33) na mitego ya nyaya 13,276 iliyokuwa ikitumika kuwatega wanyamapori zilikamatwa na kuteguliwa. Sambamba na hilo, Shirika limeendelea kutumia teknolojia za kisasa kuboresha usimamizi na ulinzi wa wanyamapori, ikiwemo matumizi ya visukuma-mawimbi, doria kwa kutumia ndege, na uwekaji wa alama za masikio kwa faru. Hatua hizi zimechangia kuimarika kwa usalama wa hifadhi na kupunguza matukio ya ujangili.

*Baadhi ya mitego ya nyaya na silaha zilizokamatwa katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.*

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano kati ya Hifadhi za Taifa na wananchi waishio pembezoni hususan kupitia Mpango wa Ujirani Mwema, Shirika limechangia utekelezaji wa jumla ya miradi 47 katika katika Sekta za Afya (4), Elimu (21), Maji (10), Ulinzi (8) na Uchumi (4) katika Wilaya za Bunda, Tarime, Kaliua, Kyerwa, Karatu, Arumeru, Serengeti, Bariadi, Kalambo, Mbarali, Kilwa, Ruangwa, Tunduru, Kigoma, Hai, Chato, Mwanga, Mpanda, Urambo, Biharamulo, Makete, Rufiji, Uvinza, Korogwe, Kondoa, Simanjiro, Babati, Liwale, Moshi, Rombo na Longido. Miradi hii pamoja na elimu iliyotolewa kwa wananchi imewezesha kuboresha mahusiano na jamii; na kudhibiti matukio mbalimbali ya uhalifu sambamba na jamii kupata taarifa zinazohusu uhifadhi. Sambamba na hilo, Shirika limekamilisha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji 18 (10 vya Wilaya ya Tanganyika na 8 vya Wilaya ya Uvinza) na kutoa mafunzo ya COCOBA kwa vikundi 36 vyenye wanachama 659 katika Wilaya za Bariadi, Tarime na Bunda kupitia Hifadhi ya Taifa Serengeti. Kuendeleza vikundi vya kukuza uchumi katika Wilaya za Busega, Meatu na Itilima. Aidha, Shirika limekarabati barabara za mchepuko zenye urefu wa kilomita 73.52 (Wilaya ya Serengeti kilometa 27.82 zenye makalavati 5 na Wilaya ya Ngorongoro kilometa 46.7).

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kudhibiti mimea vamizi katika maeneo ya hifadhi ili kukabiliana na athari zinazosababishwa na mimea hiyo ndani ya hifadhi. Hadi kufikia Aprili 2025, mimea vamizi imeondolewa katika eneo lenye ukubwa wa hekta 2,400.23 kwenye Hifadhi za Taifa Arusha, Burigi-Chato, Gombe, Ibanda-Kyerwa, Katavi, Kitulo, Ziwa Manyara, Mikumi, Mkomazi, Nyerere, Ruaha, Kisiwa cha Rubondo, milima ya Mahale na Rumanyika-Karagwe. Vilevile, Mpango wa usimamizi wa moto katika Hifadhi ya Taifa Nyerere umeandaliwa. Hatua hii imesaidia kuhakikisha makazi na malisho ya wanyamapori yanaendelea kuwa ya asili kwa ajili ya kuimarisha mifumo ikolojia.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Shirika limeendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara zenye urefu wa kilomita 2,403.4 katika Hifadhi za Taifa Arusha (97), Katavi (247), Kilimanjaro (73), Kitulo (26), Ziwa Manyara (85.4), Mikumi (87.5), Mkomazi (116.5), Ruaha (371), Kisiwa cha Rubondo (23), Saadani (118), Serengeti (682), Tarangire (113), Burigi-Chato (84), Ibanda-Kyerwa (43), Rumanyika-Karagwe (19) na Nyerere (218). Aidha, ujenzi wa daraja la Matete katika Hifadhi ya Taifa Tarangire umefikia asilimia 68 ya utekelezaji. Shirika pia limekamilisha ukarabati mkubwa wa viwanja vya ndege vitatu (3) vya Lobo, Kusini na Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Shirika limeendelea kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwa viwanja sita (6) vya ndege katika hifadhi za Taifa za Saadan (1), Mkomazi (1), Ruaha (1), Serengeti (2) na Katavi (1) ili kuimarisha usalama wa usafiri wa anga na kuvutia watalii zaidi kutembelea  hifadhi hizo.



*Ukarabati wa viwanja vya ndege vya Lobo, Kusini na Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.*

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na ujenzi wa hoteli yenye hadhi ya nyota tatu katika eneo la Rubambagwe wilayani Chato chini ya Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Rubondo na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Aidha, Shirika limeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa mabanda matatu (3) ya wageni (cottages) katika eneo la Horombo Hut yenye uwezo wa kubeba vitanda 90 na ujenzi wa vyoo vya wageni katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, banda 1 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, vibanda vitano (5) vya kupumzikia wageni (visitor’s sheds) katika Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla na kuweka samani katika hosteli ya Hifadhi ya Taifa Saadani. Vilevile, Shirika limejenga malango saba (7) ya kuingilia wageni katika hifadhi za Taifa Serengeti (2), Tarangire (1), Nyerere (2), Ibanda-Kyerwa (1) na Mkomazi (1). Miundombinu hii imelenga kuboresha huduma za utalii na ukusanyaji wa mapato. Kwa upande mwingine, Shirika limejenga kituo cha taarifa katika eneo la Seronera katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.



*Lango la kuingilia wageni (Machochwe Gate) katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.*

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza juhudi na kupanua wigo wa shughuli za utalii, Shirika limeendelea kuibua na kuendeleza mazao mapya ya utalii, ikiwemo ujenzi wa uwanja wa mpira wa gofu katika Hifadhi ya Taifa Serengeti ambao umefikia asilimia 60 ya utekelezaji wake ikiwa ni ujenzi wa jumla ya mashimo 18, visima (2), mabwawa (2), miundombinu ya maji na umeme. Aidha, ujenzi wa daraja la juu lenye urefu wa kilometa moja katika Hifadhi ya Taifa Milima Udzungwa umekamilika kwa asilimia 67. Vilevile, Shirika limeanzisha utalii wa kuogelea kwenye chemchem ya maji moto katika Hifadhi ya Taifa Ruaha; utalii wa kuruka kwa ndege ndogo katika hifadhi za Taifa za Kilimanjaro, Arusha na Ziwa Manyara na utalii wa kulala nje kuangalia nyota katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara. Aidha, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanzisha utalii wa faru katika Hifadhi za Taifa za Burigi-Chato na Mikumi unaendelea.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi kwa kurusha matangazo ya moja kwa moja, kushiriki matukio ya utalii na kutumia mitandao ya kijamii ili kuvutia watalii kutembelea hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika lilishiriki katika matukio 11 ya utalii ndani

ya Nchi yakiwemo *Land rover festival*, *Zanzibar Tourism and Investment Show,* Wiki ya Mwanakatavi, Tamasha la Kimataifa la Maendeleo ya Filamu na Sanaa Tanzania (TIFAD), Sabasaba, NaneNane, *KILI FAIR*, *Kizimkazi Festival,* Karibu Kusini na *Majimaji Festival* Vilevile, Shirika limeshiriki katika maonesho manne (4) ya kimataifa ambayo ni *World Travel Market (WTM)* Uingereza, *Qatar International Exhibition for Travel & Tourism (MART), International Gita Mahotsav 2024 in India na Swahili International Tourism Festival (SITE)* Tanzania.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kutambulika kimataifa na kushinda tuzo tatu (3) za kimataifa na tuzo moja (1) nchini za kutambua umahiri na ubora katika kutoa huduma, uhifadhi na utalii pamoja na uandaaji wa taarifa za fedha. Tuzo hizo ni ile ya utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa iliyotolewa na Shirika la Utafiti wa Ubora (European Society for Quality Research – ESQR), ambapo Shirika limeshinda kwa mara ya tano mfululizo kuanzia mwaka 2020 hadi 2024. Aidha, Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kushikilia nafasi ya kwanza duniani kama Hifadhi Bora Barani Afrika (Africa’s Leading National Park) kwa miaka sita mfululizo kuanzia 2019 hadi 2024, huku Mlima Kilimanjaro ukishinda tuzo ya Kivutio Bora cha Utalii Barani Afrika kwa mwaka 2024. Vilevile, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imetambuliwa kama eneo la pili bora zaidi duniani kwa safari na utalii na gazeti la *The Times of India* (World’s Second-Best Destination by Times of India, 2024). Tuzo hizi zinatarajiwa kuwahamasisha wadau kuendelea kutoa huduma bora katika sekta ya utalii.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia juhudi hizo zilizofanywa na Shirika, katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya watalii 1,285,876 walitembelea hifadhi za Taifa na kuwezesha makusanyo ya **Shilingi 433,612,732,617.63** sawa na asilimia 100.64 ya lengo la makusanyo ya **Shilingi 430,864,198,480.00** kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wake, Shirika limekamilisha ujenzi wa nyumba za watumishi 30 katika Hifadhi za Taifa za Mkomazi (8), Nyerere (12), Ruaha (5), Burigi-Chato (3), Rumanyika-Karagwe (1) na Milima ya Mahale (1). Sambamba na hilo mifumo mipya ya nishati ya jua imewekwa katika vituo 12 vya askari Hifadhi ya Taifa Serengeti na utafiti wa maji (hydrological survey) katika vituo 2 vya askari umefanyika pamoja na kukarabati visima vinne (4) vya mafuta katika Hifadhi ya Taifa Nyerere. Aidha, Shirika limeajiri watumishi 550 wa kada mbalimbali na kufikia asilimia 76.5 ya uhitaji wa watumishi katika Shirika. Vilevile, Shirika limewezesha watumishi 115 kufanya mafunzo ya muda mrefu na watumishi 227 mafunzo ya muda mfupi. Kwa upande mwingine, Shirika limenunua malori 5 kwa ajili ya hifadhi za Taifa za Serengeti 2 na Nyerere 3, mitambo 5 ya kutengeneza barabara Hifadhi ya Taifa Serengeti (grader 2, compactor 1, excavator 1 na back hoe loader 1), na injini za boti tatu (3) katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

#### 4.3.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa wanyamapori ili kudhibiti ujangili, uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na biashara haramu ya nyara kwa kufanya doria 12,586. Kupitia doria hizo, jumla ya mifugo 48,126 na watuhumiwa 2,513 wamekamatwa. Aidha, kupitia doria hizo bunduki 62, risasi 795 zimekamatwa na mitego 2,061 ya nyaya za kutegea wanyamapori imeteguliwa. Vilevile, katika kuongeza nguvu kazi Mamlaka imeajiri askari 221 wa ajira ya kudumu na askari 280 wa ajira ya muda mfupi.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na shughuli za utalii, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya askari

katika Pori Tengefu Lunda Nkwambi (1) na Mapori ya Akiba Wami-Mbiki (1) na Lwafi (1). Aidha, Mamlaka imekarabati vituo vinne (4) vya askari katika Pori la Akiba Maswa, kukamilisha ujenzi wa uzio katika bustani ya Wanyamapori Ruhila na ujenzi wa eneo la kupumzika wageni (Tourism Lounge) katika Pori la Akiba Mpanga-Kipengere upo katika hatua za mwisho kukamilika. Vilevile, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 120.5 katika Pori la Akiba Pande (km 10.5), Rungwa (km 80) na Makuyuni (km 30). Pia, ujenzi wa barabara unaendelea katika Mapori ya Akiba Wami-Mbiki na Mpanga-Kipengere.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kutatua migogoro ya mipaka katika maeneo ya hifadhi kwa kuweka alama za mipaka ambapo hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya vigingi 691 vimesimikwa katika Pori la Akiba Kilombero. Aidha, uhakiki wa mipaka ya Mapori ya Akiba Selous na Swagaswaga umekamilika na taratibu za utangazaji kwenye Gazeti la Serikali zinaendelea. Katika hatua nyingine, Mamlaka imekamilisha uandaaji wa Mipango ya Jumla ya Usimamizi (GMP) kwa Mapori ya Akiba Rukwa, Lukwika-Lumesule, Liparamba na Msanjesi.

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imeendelea kutangaza uwindaji wa kitalii, utalii wa picha pamoja na fursa za uwekezaji kwa njia mbalimbali ikiwemo kushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Mamlaka imeshiriki katika maonesho matatu (3) ya Kitaifa ambayo ni; Maonesho ya Biashara ya 48 ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane na Kizimkazi Festival (Zanzibar). Aidha, Mamlaka imeshiriki onesho moja (1) la Kikanda la *East Africa Trade Fair* (Mwanza) na maonesho saba (7) ya Kimataifa ambayo ni *Energy Summit* (Dar es Salaam), *Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2024), Dallas Safari Club International - USA, WTM Africa (Cape Town), International Road show, Conservation and Trade in elephant*

*Specimen (Botswana) na Tourism Investment Forum Africa (Cape Town).* Kufuatia juhudi hizo, idadi ya watalii waliotembelea maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka kwa ajili ya shughuli za utalii imeongezeka na kufikia watalii wa picha 209,522 ikilinganishwa na watalii 155,037 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 35.14 na idadi ya wawindaji imeongezeka kufikia 530 ikilinganishwa na wawindaji 484 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 9.5.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka imesaini mikataba mitatu (3) ya uwekezaji katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni (1), Pori la Akiba Kijereshi (1) na Mkataba wa Uwekezaji Mahiri kwenye Maeneo ya Wanyamapori (Special Wildlife Investment Concession Areas - SWICA) kwa kitalu cha uwindaji katika Pori la Akiba Selous (1) ambapo Kupitia uwekezaji huo, Serikali inatarajia kupata Shilingi bilioni 3.33 kwa mwaka. Kwa ujumla, kupitia uwekezaji na shughuli za utalii Mamlaka imeendelea kukusanya mapato ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya Shilingi 65,935,682,043.68 sawa na asilimia 69.73 ya lengo la makusanyo ya Shilingi 94,558,757,000 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha mahusiano kati ya hifadhi na jamii na kuhakikisha wananchi wananufaika na uhifadhi, Serikali imeendelea kurejesha stahili kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori 14, Halmashauri za Wilaya 29 na Vijiji 100 ambapo jumla ya Shilingi 17,101,288,431.08 zimetolewa. Aidha, TAWA imechangia jumla ya shilingi 162,036,860.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa na jamii. Miongoni mwa miradi hiyo ni kuchimba kisima katika Wilaya ya Rufiji; ununuzi wa madawati 295, meza mbili (2) na viti viwili (2) kwa ajili ya shule nane (8) za Wilaya za Bariadi (3) na Itilima (5); ununuzi wa viti 16 na meza tano (5) kwa zahanati ya Visakazi iliyopo Wilaya ya Chalinze; ununuzi wa madawati 300 kwa shule sita (6) za

Sekondari katika Wilaya ya Longido; ununuzi wa mifuko 325 ya saruji kwa ajili ya kuchangia miradi ya ujenzi katika Wilaya ya Makete (40), Wanging'ombe (40), Mbarali (45), Sumbawanga (75), Chemba (100) na Nanyumbu (25); na kuchangia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Zahanati za Kyanyari Wilaya ya Butiama na Ruvu Mbuyuni Wilaya ya Same. Mamlaka pia, imeendelea kuratibu shughuli za Uvuvi na Ufugaji Nyuki katika Mapori ya Akiba ya Ugalla, Uwanda, Moyowosi, Rukwa na Kilombero ambapo jumla ya wavuvi 20,914 na wafugaji nyuki 131 kutoka vijiji 98 katika Wilaya 12 walipewa vibali.

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa ofisi mbili (2) katika Pori la Akiba Muhesi na Kanda ya Ziwa (Bunda); ukarabati wa nyumba 12 katika Pori la Akiba Selous na kukamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuuzia nyara katika mikoa ya Arusha na Mwanza. Aidha, Mamlaka imenunua magari saba (7) ya doria, mitambo miwili (2) na gari aina ya boza la maji moja (1) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara. Vilevile, ujenzi wa ofisi tatu (3) kwa ajili ya Kanda ya Magharibi (1) na Mapori ya Akiba Wami-Mbiki (1) na Kilombero (1) unaendelea. Vilevile, Mamlaka imewezesha watumishi 44 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 454 mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ikiwemo udereva, urubani, ufuatiliaji na tathmini, usalama wa kimtandao (Cyber Security), ukakamavu, na upelelezi wa makosa dhidi ya wanyamapori. Aidha, Mamlaka ilishiriki katika mashindano ya SHIMUTA yaliyofanyika katika mkoa wa Tanga na kufanikiwa kupata medali ya fedha katika mchezo wa kuvuta kamba na medali moja ya shaba katika mchezo wa riadha.



*Mitambo ya ujenzi wa barabara na jengo la ofisi ya Pori la Akiba Muhesi.*

#### 4.3.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea na ulinzi wa maliasili na malikale zilizopo ndani ya Hifadhi kwa kufanya doria 4,592. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 331, mifugo 11,332, meno ya tembo 11, vipande vya meno ya tembo 27 na bunduki 1 pamoja na kutegua mitego 153 ya nyaya za kutegea wanyamapori. Aidha, Mamlaka imejenga vituo viwili (2) vya askari katika Bonde la Kreta ya Ngorongoro kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na ufuatiliaji wa wanyamapori. Katika hatua nyingine, Mamlaka imesafisha mpaka wa kilomita 85, kuweka vigingi 22 na kukarabati vigingi saba (7) kwa ajili ya alama ya mpaka wa eneo la Hifadhi hatua hii itawezesha kupunguza migogoro ya mipaka kati ya eneo la hifadhi na wananchi na matukio ya moto holela. Kwa upande mwingine, Mamlaka imetoa elimu kwa wananchi juu ya namna ya kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, mimea vamizi na mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya mikutano 112 katika wilaya za Karatu (41), Meatu (15) Monduli (12) na Ngorongoro (44) ambapo jumla ya wananchi 4,402 walifikiwa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha na kuendeleza uhifadhi wa faru nchini, Mamlaka imeongeza jumla ya faru

weupe 17 kutoka Afrika Kusini. Faru hawa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuimarisha mfumo ikolojia katika hifadhi na ushirikiano baina ya Serikali ya Afrika Kusini na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika eneo la uhifadhi wa wanyamapori. Aidha, katika kuhakikisha faru hawa wanahifadhiwa kikamilifu, Mamlaka imejenga boma moja (1) kwa ajili ya ufuatiliaji na uangalizi wa karibu miendendo yao. Vilevile, Askari wawili (2) wamepatiwa mafunzo mahsusi kwa ajili ya uangalizi wa faru hawa. Halikadhalika, Mamlaka imeendelea kuboresha ulinzi wa faru kwa kuwawekea alama maalum za utambuzi na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kufuatilia mienendo yao.




*Kushoto ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) na Kiongozi wa Kimila kutoka Afrika Kusini, iNkosi Zwelinzima Gumede wakisaini Hati ya Makabidhiano ya faru weupe kutoka Afrika Kusini katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kulia ni baadhi ya faru hao.*

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha nyanda za malisho ya wanyamapori, Mamlaka imeendelea na juhudi za kudhibiti mimea vamizi (Invasive Plant Species) kwa kufyeka na kung'oa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 460 pamoja na kuchoma moto eneo lenye ukubwa wa hekta 3,098 kwa utaratibu wa moto mpango (prescribed burning) ndani ya Bonde la Kreta na eneo la Ndutu.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza Utalii, Mamlaka imeendelea kuimarisha miundombinu ya utalii kwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya Enduleni -Ndutu yenye urefu wa kilomita 34.5 kwa kiwango cha changarawe. Aidha, Mamlaka

imekarabati mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 369 unaojumuisha barabara kuu ya Loduare hadi Golini (km 88), barabara za bonde la Kreta (km 110), *View point* hadi Nayobi (km 78), Golini hadi Ndutu (km 23), na mtandao wa Ndutu (km 70) na kukarabati kiwanja kidogo cha ndege cha Ndutu. Vilevile, Mamlaka imekamilisha zoezi la kuweka vibao 150 vya maelezo na maelekezo katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya Hifadhi na ujenzi wa *view point* tatu (3) katika eneo la Seneto, Empakai na Gilai. Sambamba na hilo, Mamlaka imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya umeme, vyoo na mifumo ya maji katika maeneo yanayotumiwa na watalii katika maeneo ya Loduare, Ngoitoktok, Olduvai, Seneto ya Juu, Seneto ya Chini, Lerai *picnic site*, Nyati *Public campsite* na *View point*.





*Muonekano wa barabara kuu ya Loduare hadi Golini iliyoboreshwa katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.*

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani ya vivutio vya malikale, Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai katika eneo la Kamny Wilaya ya Karatu ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95. Sambamba na hilo, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa majengo maalum mawili (2) ya kuhifadhi nyayo za zamadamu, choo kimoja (1) na vibanda viwili (2) kwa ajili ya kupumzikia wageni katika eneo la nyayo za Laetoli. Vilevile, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya maji katika

kituo cha utalii cha Kimondo kilichopo Mbozi-Songwe na kuendelea na ujenzi wa lango la kuingilia kwenye mapango ya Amboni-Tanga.



*Mradi wa ujenzi wa makumbusho ya Jiolojia ya Ngorongoro-Lengai katika eneo la Kamny, Wilaya ya Karatu.*



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), akiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea eneo la Mapango ya Amboni, Tanga.*

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kutangaza vivutio vya utalii kwa kufanya kampeni tatu (3) kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani ambazo ni *Merry and Wild - Ngorongoro awaits*, Diko la Amboni na *Mwanamke Talii, Twenzetu Ngorongoro*. Aidha, Mamlaka imeshiriki katika maonesho 12 ndani ya nchi na maonesho sita (6) nje ya nchi. Juhudi hizi zimechangia kuleta matokeo chanya hususan katika kuongeza idadi ya watalii waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya watalii 925,163 walitembelea Hifadhi ya Ngorongoro ikiwa ni ongezeko la asilimia 18 ikilinganishwa na idadi ya watalii katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Idadi hii ya watalii imewezesha Mamlaka kukusanya jumla ya Shilingi 231,186,145,522.22 sawa na asilimia 100.52 ya lengo la Shilingi 230,000,000,000.00 zilizopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea na jukumu la kuendeleza jamii ya wenyeji waishio ndani ya Hifadhi kwa kutoa ufadhili wa ada, fedha ya kujikimu na nauli kwa wanafunzi 1,683 katika ngazi mbalimbali za elimu ikiwemo; Chuo Kikuu (52), vyuo vya kati (245) na sekondari (1,386). Aidha, hadi kufikia Aprili, 2025 Mamlaka imegawa kilo 1,200 za sukari na kilo 13,075 za unga wa mahindi kwa ajili ya huduma ya uji katika shule 27 zilizopo ndani ya eneo la Hifadhi. Vilevile, Mamlaka imewezesha utoaji wa huduma za afya bure kwa wakazi katika Zahanati ya Ngorongoro.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha watumishi wanatekeleza majukumu yao kwa weledi, Mamlaka imeendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya kitaaluma. Hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya watumishi 612 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika nyanja za uongozi, itifaki, maadili, kanuni za jumla za Jeshi la Uhifadhi, matumizi ya silaha ndogo na urubani wa ndege nyuki. Aidha, Mamlaka imewezesha watumishi 45 kuhudhuria mafunzo

ya muda mrefu na watumishi 21 mafunzo ya awali ya Jeshi la Uhifadhi ili kuweza kutekeleza majukumu yao na kuboresha utendaji kazi. Vilevile, Mamlaka imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu katika eneo la Kamyn, Wilayani Karatu ambao ujenzi umefikia asilimia 87.



*Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro katika eneo la Kamyn, Wilayani Karatu*

#### 4.3.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAWIRI ina jukumu la kufanya, kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori nchini kwa lengo la kuishauri Serikali na wadau namna bora ya uhifadhi endelevu na maendeleo ya utalii. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, TAWIRI imetekeleza zoezi la kuidadi wanyamapori nchi nzima. Hadi kufikia sasa, zoezi limekamilika katika mifumo ikolojia sita (6) yenye maeneo makubwa zaidi kati ya 11, ikiwemo Katavi–Rukwa, Ruaha–Rungwa, Nyerere–Selous–Mikumi, Ziwa Natron–Kilimanjaro Magharibi, Mkomazi–Handeni na Tarangire–Manyara yenye ukubwa wa kilometa za mraba 241,537 sawa na asilimia 73.3 ya eneo lote linalotakiwa kufanyiwa sensa ambalo ukubwa wake ni kilometa za mraba 329,537. Aidha, mifumo ikolojia iliyosalia inategemewa kukamilika kabla ya mwaka wa fedha kumalizika. Matokeo ya awali yanaonesha kuendelea kuimarika kwa aina na idadi ya

wanyamapori ikiwa ni kiashiria cha kuimarika kwa uhifadhi, jambo ambalo litaendeleza utalii.



*Zoezi la kuidadi wanyamapori kwa njia ya anga kwa kutumia ndege ndogo na teknolojia ya kamera za kisasa na namna mpya ya upigaji picha kutoka angani ijulikanayo kama "Oblique Camera Count".*

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kubuni teknolojia ili kuboresha namna ya kuhesabu wanyamapori kwa njia ya anga. Ubunifu huu umejikita katika teknolojia ijulikanayo kama *Oblique Camera Count*, ambayo inatumia kamera za kisasa zaidi na namna mpya ya upigaji picha za wanyamapori kutoka angani wakati wa zoezi la sensa na matumizi ya akili mnemba katika kutambua spishi na idadi ya wanyamapori waliopigwa picha. Teknolojia hii inatumika kwa mara ya kwanza nchini kwenye zoezi la sensa za wanyamapori zinazoendelea, sambamba na ile ya awali ili kuweza kupata ulinganifu wa ubora wa matokeo. Matokeo ya awali yanaonesha matumizi ya teknolojia hii yameongeza ufanisi katika zoezi la sensa, kupunguza gharama na muda wa kupata matokeo.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi pia imetekeleza miradi 13 ya utafiti, iliyojikita katika kutatua changamoto za uhifadhi zikiwemo: migongano kati ya binadamu na wanyamapori (4), matumizi ya teknolojia katika uhifadhi (1), afya ya mifumo ikolojia (2), nyuki na mazao yake (1), mahusiano ya viumbe na ikolojia zao (3), uhifadhi wa bioanuai (1) na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia (1). Aidha, Taasisi imeratibu na kusimamia miradi ya utafiti 100 yenye jumla ya watafiti 326 wa ndani na nje ya nchi waliosajiliwa. Matokeo ya tafiti hizi yanalenga kutatua changamoto za uhifadhi, matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori na kuendeleza utalii.

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha afya za wanyamapori, Taasisi imeendelea kufanya tafiti na ufuatiliaji wa magonjwa ya wanyamapori yanayoweza kuathiri uhifadhi na utalii. Kwa kipindi hiki, tafiti na ufuatiliaji zimefanyika katika mifumo ikolojia ya Kaskazini Magharibi na Kusini mwa Tanzania ambapo jumla ya sampuli 1,050 zilikusanywa kwa ajili ya uchunguzi. Matokeo yameonesha kutokuwepo kwa vimelea vya milipuko ya magojwa ya wanyamapori ambayo yangeweza kuleta athari kwenye uhifadhi na maendeleo ya utalii.

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi pia imefanya utafiti wa nyuki wa kujua namna matumizi tofauti ya ardhi yanavyoathiri utendaji kazi na uzalishaji wa makundi ya nyuki. Utafiti huu unafanyika katika manzuki tatu (3) zilizopo katika maeneo ya *West* Kilimanjaro ambapo kuna mashamba ya miti (plantation forests), Magugu kwenye mashamba ya mazao (agricultural areas), na kituo cha Tabora kwenye misitu ya asili (natural forests). Matokeo ya awali yameonesha kwamba tabia na shughuli za makundi ya nyuki zinatofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na matumizi tofauti ya ardhi. Aidha, kwa upande wa uzalishaji (utunzaji wa chavua na asali), maeneo ya mashamba ya miti (plantation forests) yameonesha kuwa na sifa bora zaidi

ikifuatiwa na maeneo yaliyozungukwa na ardhi ya kilimo (agricultural areas) na mwisho ni maeneo ya misitu asilia.

**80.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utendaji kazi na uwezo wa taasisi kutoa huduma, watumishi 11 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 35 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na watumishi 23 wameajiriwa ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi. Kwa upande mwingine, Taasisi imekamilisha ujenzi mfumo wa TEHAMA na kuanza kutumia kwa lengo la kuratibu na kusimamia tafiti za wanyamapori na tayari umeunganishwa na mfumo wa Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) unaowezesha usajili na upatikanaji wa vibali vya utafiti kidijitali.

#### 4.3.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori MWEKA – CAWM

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo kuanzia Cheti cha Msingi, Cheti cha Ufundi, Stashahada ya kawaida, Shahada ya kwanza na Shahada ya Uzamili. Vilevile, Chuo kina jukumu la kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani katika nyanja za usimamizi wa wanyamapori na utalii. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,216 sawa na asilimia 122 ya lengo la wanafunzi 1,000 ambapo wanafunzi 457 ni wanawake na 759 ni wanaume. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 257 (watanzania 227 na wa nje 30). Washiriki kutoka nje ya Tanzania walitoka katika nchi za Ethiopia tisa (9), Kenya nane (8), Rwanda tatu (3), Saudi Arabia sita (6) na Uganda wanne (4). Mafunzo yaliyotolewa ni uongozaji wa watalii wa kupanda mlima (Mountain Guide Course), waongozaji wa wageni (Safari guides), waangalizi wa mazingira na ufuatiliaji wa kidijitali wa matukio ya ujangili. Katika hatua nyingine, Chuo kimeandaa mitaala 9 ya kozi za

muda mrefu na mitaala 13 ya kozi za muda mfupi katika Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa taka.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Chuo kimekamilisha ujenzi wa jengo la mafunzo la ghorofa mbili lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja na ofisi za wahadhiri pamoja na kuweka samani, kufunga kompyuta 25 na projector 10 katika jengo hilo. Aidha, ujenzi wa darasa, jiko, vyoo na mabafu unaendelea katika eneo la mafunzo kwa vitendo lililoko Kijiji cha Arash, Tarafa ya Loliondo. Vilevile, ukarabati wa nyumba nne (4) za watumishi, vyumba vitano (5) vya madarasa, hosteli mbili (2) za wanafunzi umefanyika na kuweka taa za barabarani ili kuimarisha usalama. Sambamba na hilo, Chuo kimenunua mini bus (Coaster) (1), magari mawili (2) maalum aina ya KAMAZ pamoja na mahema 50, magodoro 70 na GPS 20 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kutatua changamoto zinazoikabili Sekta ya Wanyamapori na Utalii, Chuo kinafanya tafiti katika nyanja za Bioanuwai, Uhifadhi wa mazingira na jamii ya mimea, Uhifadhi wa wanyamapori, Magonjwa ya wanyamapori na binadamu, Usimamizi wa utalii na Migogoro baina ya wanyamapori na binadamu katika maeneo mbalimbali nchini. Miongoni mwa Tafiti hizo zimewezesha ugunduzi wa viuatilifu hai (biopesticides) vya kupambana na wadudu waenezao magonjwa kwa wanyama na wadudu waharibifu wa mazao na kutatua baadhi ya changamoto za uhifadhi wa wanyamapori na utalii nchini.

**84.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na tafiti hizo, Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Dkt. Never Mwambela alitunukiwa tuzo mbili za kutambua ubora wa matokeo ya tafiti na ubunifu katika kutatua changamoto za uhifadhi wa mazingira ambazo ni Tuzo

ya kiuatilifu hai bora kinachochangia kuhifadhi mazingira (*Agro-ecological Food Futures Prize*) iliyotolewa na Taasisi ya Biovision ya nchini Switzerland; na Tuzo ya Mtafiti bora Barani Afrika juu ya ubunifu bioanuai zinazochochea uhifadhi wa mazingira (*European Coimbra Award for Young African Researchers*) iliyotolewa na Umoja wa Ulaya.

**85.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo kimetekeleza Mradi wa ukusanyaji wa taarifa za uwindaji haramu katika Mapori ya Akiba ya Mkungunero, Maswa, Kijereshi na Swagaswaga. Kupitia mradi huo, viongozi wa hifadhi hizo na askari 40 wamejengewa uwezo wa kukusanya takwimu za uwindaji, wanyamapori wakali na waharibifu na kuandaa taarifa za kitaalamu kwa kutumia njia za kidijitali.

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo kimefanya Kongamano la Kimataifa la Biolojia ya Uhifadhi Kanda ya Afrika (African Congress on Conservation Biology – ACCB) ambalo ni kongamano la nne (4) kufanyika tangu kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo na ni mara ya kwanza kufanyika nchini. Kongamano hilo lilihudhuriwa na washiriki 201 kutoka nchi 24 duniani kwa lengo la kubadilishana taarifa za utafiti na kuwatambua wahifadhi na jamii zilizo mstari wa mbele katika masuala ya uhifadhi. Katika Kongamano hilo jumla ya dhahania 210 za kisayansi zinazohusu Uhifadhi ziliwasilishwa. Kongamano hilo limewezesha Chuo kujitangaza kimataifa na washiriki kubadilishana uzoefu kwenye masuala ya uhifadhi.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimeendelea kuwajengea watumishi uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa kuwawezesha watumishi 18 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 80 mafunzo ya muda mfupi katika nyanja mbalimbali. Aidha, watumishi 123 wamepatiwa mafunzo kuhusu maadili na mapambano dhidi ya rushwa.

#### 4.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi – PWTI

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina jukumu la kutoa mafunzo kwa kozi za uaskari wa Wanyamapori na uongozaji watalii, kutoa ushauri elekezi na kutoa mafunzo ya kozi za muda mfupi. Kufikia mwezi Aprili, 2025 Taasisi imedahili wanachuo 696 sawa na asilimia 87 ya lengo la wanachuo 800 waliotarajiwa kudahiliwa kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 158 wa kozi fupi ya Uaskari wa Misitu na hifadhi za fukwe na Uaskari Wanyamapori VGS (36) kutoka mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Simiyu, Pwani, Tanga na Arusha. Katika hatua nyingine, Mitaala miwili (2) ambayo ni Stashahada ya Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na Usalama imeandaliwa.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha miundombinu ya mafunzo, Taasisi imekarabati nyumba tano (5) za watumishi na uzio wa ukuta wenye urefu wa mita 240 kuzunguka eneo la Taasisi na ujenzi wa bweni litakalochukua wanafunzi wa kiume 240 unaendelea. Aidha, watumishi watatu (3) wamewezeshwa kuendelea na masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu na mtumishi mmoja (1) katika masomo ya Astashahada ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Himasheria. Sambamba na hilo, Taasisi imeshiriki katika maonesho ya ndani ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Wanyamapori Duniani pamoja na Siku ya Misitu Duniani kwa lengo la kutangaza kazi zake kwa wadau.

#### 4.3.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga – CBCTC

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kimeanzishwa kwa lengo la kuijengea jamii uwezo kwa njia ya mafunzo ili iweze

kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za maliasili kwa maendeleo endelevu. Hadi kufikia Aprili, 2025 kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 329, kati yao wanafunzi 158 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya Utalii na Uongozaji Watalii na 171 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ya Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS). Aidha, Kituo kimeshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya 48 (Sabasaba), Maadhimisho ya Siku ya Wakulima (Nanenane), Siku ya Wanyamapori Duniani, na Siku ya Misitu Duniani na Kumbukizi ya Vita vya Majimaji kwa lengo la kujitangaza na kutoa elimu ya uhifadhi wa wanyamapori.

**91.** ***Mheshimiwa Spika*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na miundombinu, kituo kimeendelea na ujenzi wa darasa moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 150 kwa fedha za ndani. Sambamba na hilo, kituo kupitia ufadhili wa Serikali ya Ujerumani katika mradi wa "SECAD" kimekamilisha uchimbaji wa kisima, kujenga bweni moja (1) la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64 ambalo limefikia asilimia 85, darasa moja (1) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 lililofikia asilimia 90 pamoja na mnara wa kuwekea tanki la maji uliofikia asilimia 87. Aidha, kituo kimewezesha mtumishi mmoja (1) kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi wawili (2) wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Uzamili na Stashahada.

### 4.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta hizi unasimamiwa na Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu

Tanzania Sura 270. Vilevile, jukumu la uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) Tabora, Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) na Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC) Mafinga, Iringa. Pia, Serikali za Mitaa (Vijiji na Halmashauri) zina jukumu la kuhifadhi na kusimamia rasilimali hizo katika maeneo yao.

#### 4.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa rasilimali za misitu na nyuki zinahifadhiwa na kusimamiwa ipasavyo, Wizara imeandaa Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Matumizi ya Msumeno wa Moto, Tangazo la Serikali Namba 62/2025; na Kanuni za Utaratibu wa Usafirishaji wa Venia kwenda Nje ya nchi, Tangazo la Serikali Namba 807/2024. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki, Tangazo la Serikali Namba 760/2023; Kanuni za Jumla za Mazao ya Misitu, Tangazo la Serikali Namba 59/2022 pamoja na kufanya marekebisho ya Kanuni ya Uzalishaji, Usafirishaji na Uuzaji wa Mkaa Mbadala, Tangazo la Serikali Namba 1085/2024. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kitaalam kuhusu Miti ya Mbao inayofaa kwenye Ujenzi na Kutengeneza Samani. Kwa upande mwingine, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) wa mwaka 2007. Matokeo ya tathmini yamebaini kuwa hali ya uhifadhi wa misitu iliyo katika utaratibu wa usimamizi shirikishi imeendelea kuimarika. Wizara inatoa wito kwa jamii kuendelea kushirikiana na Wizara kulinda na kuhifadhi misitu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

**94. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kuelimishwa na kuhamasika kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Upandaji Miti Kitaifa. Maadhimisho haya ni utekelezaji wa maelekezo ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa ambapo lilielekeza kuwa kila tarehe 21 Machi ya kila mwaka iwe ni siku ya maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na kuwataka nchi wanachama kuadhimisha siku hiyo. Kwa upande wa Tanzania, maadhimisho haya yalifanyika Mkoani Njombe na kuongozwa na Kaulimbiu "*Ongeza thamani ya mazao ya Misitu kwa uendelevu wa rasilimali kwa kizazi hiki na kijacho*". Aidha, kupitia maadhimisho hayo wananchi walishiriki katika Kampeni ya Upandaji Miti iliyozinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kushiriki midahalo ya kujadili fursa zilizopo kwenye sekta ya misitu; zoezi la upandaji miti katika Wilaya zote za Mkoa wa Njombe na maonesho ya bidhaa za mazao ya misitu na huduma za utalii. Sambamba na tukio hili, Wizara inaratibu maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park hapa Jijini Dodoma kuanzia tarehe 17 hadi 20 Mei, 2025. Hivyo, natumia nafasi hii kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote kutembelea maonesho haya kwa lengo la kujifunza na kupata huduma na bidhaa mbalimbali zinazotokana na ufugaji nyuki.

**95. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kushiriki kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora. Mpango huu unalenga kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali kutoka tani 33,861 za sasa hadi kufikia tani 75,000 ifikapo Juni, 2035 na kuongeza mauzo ya mazao ya nyuki katika masoko ya kikanda na kimataifa. Aidha, Mpango unatarajiwa kuongeza ajira mpya 43,055 kupitia shughuli zilizopo katika mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki. Mpango

utatekelezwa katika kipindi cha miaka 10 kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa na kusaini Hati ya Makubaliano ya usimamizi wa mradi wa ufugaji nyuki kati ya Wizara, WAGA WMA na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Kwa lengo la kuongeza wigo wa biashara ya asali, kwa niaba ya Serikali Wizara imesaini Itifaki kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China inayoruhusu uuzaji wa Asali ya Tanzania nchini China. Utiaji saini wa Itifaki hii umefungua milango kwa wafanyabiashara wa Tanzania kuuza asali inayozalishwa nchini katika soko la nchini China. Sambamba na hili, Wizara imeratibu uzinduzi wa Alama ya Asali ya Tanzania (Honey Trademark) yenye usajili TZ/T/2023/3136 uliofanyika Oktoba, 2024. Alama hii ni utambulisho wa asali ya Tanzania katika soko la kitaifa, kikanda na kimataifa. Kutokana na jitihada hizi za Serikali, napenda kutoa wito wafanyabiashara wa Tanzania kuendelea kuchangamikia fursa hizi ili kuweza kuongeza kipato kwa Taifa letu kupitia biashara ya mazao ya nyuki.




*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana (Mb) akizindua nembo ya asali ya Tanzania itakayotumika kuitambulisha bidhaa hiyo katika Soko la Dunia.*

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa wadau katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki, kwa kuratibu vikao viwili (2) vya wadau wa misitu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), vikao saba (7) vya Kamati ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA) na vikao viwili (2) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC). Aidha, Wizara imezindua Kamati ya Kitaifa ya Ushauri

ya Misitu (NAFAC) na kufanya Kikao kimoja (1) cha Kamati Endeshi ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa. Wizara pia imefanya vikao vinne (4) baina ya Sekta binafsi na Serikali (Private Public Dialogue) kwa lengo la kutatua vikwazo vya kibiashara katika sekta ya misitu na kikao cha kujadili fursa za uendeshaji wa Biashara ya Mazao ya Misitu na Kilimo Misitu (Agroforestry). Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya Viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu katika mikoa ya Iringa na Njombe pamoja na viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki katika mikoa ya Tabora na Kigoma. Tathmini imebaini kuwa bado kwa sehemu kubwa viwanda vilivyopo vinafanya kazi chini ya uwezo wake kutokana na ufinyu wa malighafi. Wizara inaendelea kuhimiza watu binafsi na Makampuni kuwekeza katika mashamba ya miti pamoja na mashamba makubwa ya kuzalisha asali. Sambamba na hilo, Wizara imetoa mafunzo kwa kampuni 48 za wafanyabiashara wa mazao ya misitu wa halmashauri za Mafinga, Mufindi na Njombe kuhusu utekelezaji wa kanuni na taratibu za uzalishaji na usafirishaji wa venia pamoja na mazao ya misitu yaliyohandisiwa. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa Wafugaji Nyuki Jumuiya WAGA WMA iliyopo Wilayani Mufindi, na Jumuiya ya Wafugaji Nyuki Muhesi na Mwakintaru za halmashauri ya Itigi. Katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (COP-29) kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Jijini Baku, Azerbaijan kwa lengo la kupata fursa za wawekezaji kwa ajili ya uhifadhi na shughuli za utalii unaozingatia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

#### 4.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ulianzishwa kwa lengo la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Aidha, Wakala unatekeleza majukumu mbalimbali

yakiwemo: Kuanzisha na kusimamia Misitu ya hifadhi, Hifadhi za Nyuki za Serikali kuu, mashamba ya miti na manzuki ya Serikali kuu; Kusimamia rasilimali za misitu na nyuki katika ardhi ya jumla (General Land) pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sheria za Misitu na Ufugaji Nyuki.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuzuia uharibifu wa rasilimali za misitu na nyuki nchini, Wakala umefanya jumla ya doria 405 za kiintelijensia na doria 17,510 za kawaida katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Kupitia doria hizo, jumla ya watuhumiwa 3,459 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Aidha, doria hizo zimewezesha kukamatwa na kutaifishwa kwa magunia ya mkaa 36,625 yaliyovunwa bila kufuata utaratibu, mbao 40,621 zenye mita za ujazo 2,671, kuni zenye mita za ujazo 285 na magogo 1,267 yenye mita za ujazo 226.6. Pia mifugo 27,011, pikipiki 2,727, magari 297 na boti tatu (3) zilikamatwa na taratibu mbalimbali za kisheria zinaendelea. Katika hatua nyingine, Wakala umeandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 62 yenye ukubwa wa hekta 775,917. Vilevile, Wakala umesafisha njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 2,023.2, kusimamia minara 10 ya kuangalizia matukio na vituo saba (7) vya kufuatilia na kudhibiti matukio ya moto. Pia, Wakala umetoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na kudhibiti moto kwa vikosi 35 vyenye jumla ya watu 405 vya kudhibiti moto na wananchi 15,632 kutoka vijiji 269 vinavyopakana na hifadhi za misitu katika maeneo mbalimbali nchini.

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kutambua umuhimu wa bioanuai za kipekee na mimea iliyo hatarini kutoweka, Wakala umepandisha hadhi misitu ya hifadhi miwili (2) hifadhi za Rau (mkoani Kilimanjaro) na Nou (mkoani Manyara) yenye ukubwa hekta 30,396.7 kuwa hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia. Aidha, upandishaji hadhi huu unapelekea utendaji endelevu wa misitu kwa faida za kimazingira, shughuli za utalii na uwekezaji

ambapo utaongeza idadi ya watalii na kuimarisha uhifadhi wa misitu hiyo. Katika hatua nyingine, Wakala umetangaza kisheria misitu 43 kuwa Hifadhi za Misitu.

**100.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza kasi ya uhifadhi na upandaji miti kuifanya nchi kuwa ya Kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu Nchini, Wakala umeanzisha vyanzo sita (6) vya kuzalisha mbegu bora za miti vyenye ukubwa wa hekta 60 ambavyo vimechangia uzalishaji wa zaidi ya tani 20.2 za mbegu bora za miti toka vyanzo mbalimbali vya mbegu. Aidha, Wakala umezalisha miche ya miti milioni 33.2 jamii (species) mbalimbali ambayo imeendelea kupandwa katika mashamba 24 ya Serikali na kugawa kwa watu binafsi, taasisi na mashirika ya umma na binafsi. Vilevile, Wakala umepanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8,270.2; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 1,794; kupalilia eneo lenye hekta 23,276; kupogolea hekta 10,769; kupunguzia miti kwenye hekta 2,108 katika mashamba yanayosimamiwa na Wakala. Pia, Wakala umepanda miche ya mikoko 15,650 kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 60 katika mwambao wa bahari ya Hindi kwenye Wilaya za Lindi, Kilwa, Temeke, Mafia na Tanga.




*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson akizindua Kampeni ya upandaji miti mkoani Mbeya.*




*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Dunstan Kitandula, akipokea maelezo kuhusu moja ya kiliba cha miti kutoka kwa Mhifadhi Mkuu wa Shamba la Miti Silayo, Bw. Juma Mwita Mseti, katika Shamba hilo lililopo mkoani Geita.*

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala umeimarisha shughuli za ufugaji nyuki kwa kusimamia manzuki 222 na mashamba matatu (3) ya Nyuki ya Kipembawe (Chunya), Mwambao (Handeni na Kilindi) na shamba la Kati (katika wilaya za Manyoni, Chemba na Kondoa) ambapo tani 22.5 za asali na tani 0.9 za nta zenye thamani ya Shilingi 282,713,700 zimezalishwa. Vilevile, maafisa ufugaji nyuki na maafisa misitu 35 wa halmashauri na vikundi 53 vya ufugaji nyuki vyenye jumla ya wafugaji nyuki 1,825 wamepewa mafunzo kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya ufugaji nyuki; kuhamasisha ufugaji nyuki kibiashara; na uchakataji na ufungashaji bora wa mazao ya nyuki. Aidha, Wakala umekusanya sampuli 132 za asali katika Wilaya 30 na kupelekwa kwenye maabara ya kimataifa nje ya nchi kwa lengo la kujiridhisha na ubora wa mazao ya nyuki yanayozalishwa nchini. Matokeo ya ubora wa sampuli hizo yatawezesha asali ya Tanzania kuendelea kuruhusiwa kuuzwa katika masoko ya kikanda na kimataifa.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kukosekana kwa mipango ya matumizi ya

ardhi katika maeneo mengi nchini, kumekuwepo na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na makazi. Kufuatia changamoto hii, Wakala umeendelea kutatua migogoro baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi kwa kuboresha huduma za ugani katika vijiji vinavyopakana na hifadhi za misitu na kuimarisha mipaka katika misitu ya hifadhi. Aidha, Wakala umeimarisha mipaka ya misitu 116 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 425; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,568; kuweka vigingi 672, mabango 157; na kuchimba mitaro 41 inayoonesha uelekeo wa mipaka ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala umetoa elimu ya uhifadhi na usimamizi wa misitu kwa wananchi 6,074 kutoka vijiji 75 vinavyopakana na misitu ya hifadhi.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza utalii wa misitu na malikale, Wakala umeboresha miundombinu ya utalii katika hifadhi za misitu yenye vivutio vya utalii ikolojia kwa kujenga njia mpya za kutembea watalii zenye urefu wa kilomita 43.6, kukarabati kilomita 339.12 za njia za watalii na kilomita 122 za barabara katika hifadhi za misitu (10) na vituo viwili (2) vya Malikale. Aidha, Wakala umejenga daraja la kitalii, kukarabati mabanda mawili (2) ya kupumzikia watalii; kambi 21 za watalii na minara miwili (2) ya kutazama vivutio. Sambamba na hilo, Wakala umeendelea kutangaza vivutio vya utalii Ikolojia na Malikale katika hifadhi za misitu kwa kuzalisha na kurusha video fupi za picha mjongeo 287, jumbe fupi 372, vipindi 71 vya redio na 85 vya televisheni pamoja na kusambaza machapisho takriban 10,837 yenye jumbe za kuhamasisha utalii. Vilevile, Wakala umeandaa matangazo 21 yanayoonyesha vivutio vya utalii ikolojia yaliyorushwa katika mechi za ligi kuu ya NBC katika Uwanja wa *Azam Complex*.

*Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) akiambatana na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii walipotembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa daraja la watembea kwa miguu (Board walk) katika Hifadhi ya Misitu ya Mikoko Sahare, Tanga.*

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala umeshiriki matamasha tisa (9) ya ndani na nje ya nchi na umeandaa matamasha 10 kama sehemu ya kutangaza utalii wa misitu yakiwemo *Meru Forest Festival*, *Bata Msituni Festival*, *Tukacharu Rau Forest*, *Morogoro Car Rally*, *Mount Rungwe Hiking Challenge* na *Mount Hanang Bush Challenge*. Juhudi hizi zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya utalii ikolojia kufikia 275,723 Aprili 2025 ikilinganishwa na watalii 211,764 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 30. Aidha, mapato yanayotokana na shughuli za utalii ikolojia yameongezeka na kufikia Shilingi 2,169,832,146 Aprili 2025, sawa na ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na Shilingi 1,689,095,459 zilizokusanywa kipindi kama hicho Mwaka 2024.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umetoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 13,755 katika vijiji 94 vinavyopakana na hifadhi za misitu. Aidha, Wakala umegawa miche ya miti 10,769,510 yenye thamani ya Shilingi 3,908,244,024 na mizinga ya nyuki 1,059 yenye thamani ya Shilingi 158,850,000. Vilevile, Wakala umewezesha ujenzi wa jengo la utawala la Shule ya Sekondari Wino Mkoani Ruvuma; kuwezesha ununuzi wa samani (madawati 330, meza 2 na viti

10) na vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Shilingi 665,361,027 kwa shule za msingi 13 na Sekondari 14 katika maeneo mbalimbali nchini.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, Wakala umewezesha mafunzo ya utayari kwa watumishi 89 na mafunzo ya uongozi kwa watumishi 481; mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 95 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 443 katika nyanja mbalimbali. Mafunzo haya yatawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi. Aidha, katika kuongeza nguvukazi ya Wakala, usaili wa watumishi 205 umefanyika ambapo taratibu za ajira zinaendelea kupitia Sekretarieti ya Ajira.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala umepata ufadhili wa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Uhifadhi wa Misitu ya Mikoko kutoka Shirika la Maendeleo ya Serikali ya Ufaransa (AFD) wenye thamani ya Shilingi bilioni 122 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2025/2026 – 2030/2031). Mradi huu unalenga kujenga uwezo wa TFS kusimamia mashamba ya miti kwa jumla na kuongeza kasi ya upandaji miti ambapo jumla ya hekta 22,500 zitapandwa katika Mashamba ya Miti Silayo Mkoani Geita, Mtibwa, Morogoro na Wino lililopo Mkoani Ruvuma. Vilevile, mradi utawezesha usimamizi wa hifadhi za mikoko katika wilaya za Rufiji, Kilwa na Kibiti na kuongeza fursa za kiuchumi kwa kuwezesha miradi mbalimbali ya kiuchumi kwa wananchi wanaoishi karibu na misitu hiyo ili kupunguza utegemezi kwenye misitu.

#### 4.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ina jukumu la kufanya na kuratibu tafiti za misitu na ufugaji nyuki, kutoa ushauri wa kitaalam na kusambaza matokeo ya utafiti katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki kwa wadau. Katika kuhakikisha kuwa jamii inapata matokeo ya tafiti mbalimbali za misitu na nyuki, TAFORI iliandaa Kongamano la Tatu la Kimataifa la Kisayansi lililoongozwa na mada isemayo "Kurejesha Mandhari ya Misitu kwa Maendeleo Endelevu na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Restoring Forest Landscapes for Sustainable Development and Climate Change Mitigation)". Kongamano hili lilifanyika mwezi Disemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na washiriki 996 kutoka Tanzania na Mataifa mbalimbali ikiwemo Kenya, Afrika Kusini, Uswisi, Japan, Estonia, Ufini na Ujerumani. Aidha, kupitia kongamano hili mada 72 ziliwasilishwa zilizojikita katika maeneo ya ufadhili na ubunifu wa teknolojia kwenye Sekta ya Misitu na Nyuki; urejeshwaji wa maeneo yaliyoharibiwa na uhifadhi wa bioanuai; ubunifu na matumizi ya teknolojia katika viwanda vya misitu na nyuki; athari za mabadiliko ya tabianchi katika mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na nyuki; ushirikishwaji wa jinsia katika Sekta ya Misitu na Nyuki; na matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Kutokana na kongamanao hilo, maazimio 18 yalitolewa yenye lengo la kuboresha uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki.

**109.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake, TAFORI imefanya jumla ya tafiti 19 zikiwemo tafiti tano (5) za kimkakati zilizojikita katika mimea vamizi, nyuki na mazao yake, ubunifu na teknolojia ya viwanda vya misitu, uongezaji thamani wa mazao ya misitu na nyuki, mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya nishati mbadala na magonjwa ya miti.

Matokeo ya tafiti hizi yanalenga kutatua changamoto za uhifadhi na kuendeleza sekta ya misitu na nyuki.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kufanya tathmini ya rasilimali za misitu kwa lengo la kuongeza tija katika viwanda vya mazao ya misitu vilivyopo nchini. Matokeo ya tathmini yamebaini uwepo wa jumla ya viwanda vya misitu 614 katika mikoa ya Arusha (136), Kilimanjaro (311),Tanga (130), Morogoro (12), Dar es Salaam (11) na Pwani (14). Vilevile, imebaini kuwa hekta 18,836.04 za mashamba ya miti zipo mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Mashariki. Mahitaji ya malighafi kwa viwanda vya misitu vilivyopo katika kanda hizo ni mita za ujazo 1,136,000.00 kwa mwaka na kiasi kinachopatikana kwa mwaka ni mita za ujazo 312,430.00 sawa na asilimia 27.3 ya mahitaji. Matokeo haya yanaonesha kuwa viwanda vingi vinafanya kazi chini ya uwezo kutokana na ufinyu wa malighafi. Hali hii inachochea na kuhamasisha fursa za uwekezaji zaidi katika kuanzisha mashamba mapya ya miti nchini.

**111.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFORI pia imefanya tathmini ya kiwango cha asali kinachozalishwa kwa mizinga ya aina mbalimbali nchini. Tathmini hii inaendelea kufanyika katika manzuki 21 za majaribio ya kisayansi zilizoanzishwa katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Chamwino, Manyoni, Sikonge, Kasulu, Mlele, Bukombe, Butiama, Itilima, Morogoro, Kibiti, Handeni, Pangani, Mtama (Rondo), Tunduru, Mufindi, Njombe, Chunya, Siha, Same na Simanjiro. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa kiasi cha wastani wa kilo 19.10 za asali huzalishwa kwenye mzinga wa nyuki wa kisasa ikilinganishwa na kilo 10 zinazozalishwa kutoka katika mzinga wa kienyeji. Matokeo ya tathmini hii yanachochea jamii kutumia mizinga ya kisasa ili kuongeza kiwango na ubora wa mazao ya nyuki. Katika hatua nyingine, TAFORI imefanya utafiti wa kuangalia sifa za asali inayozalishwa katika uoto mbalimbali nchini

ambapo matokeo ya utafiti huo yamebaini uwepo wa asali zenye sifa tofauti za ubora zikiwemo ladha, rangi na viambata muhimu. Hatua hii imewezesha kutengenezwa kwa Alama ya Asali ya Tanzania (Honey Trademark) itakayotumiwa na wafanyabiashara kama alama ya kuitambulisha asali ya Tanzania katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**112.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFORI kwa kushirikiana na Taasisi ya Tiba Asilia ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili inafanya utafiti juu ya matumizi na hali ya uhifadhi wa mimea dawa iliyopo mashambani kwa uboreshaji wa maisha na uhifadhi wa misitu katika Milima ya Tao la Mashariki. Utafiti huu umefanyika katika Wilaya za Kilolo mkoani Iringa na Kilombero mkoani Morogoro. Utafiti umeonesha kuwa asilimia 71 ya mimea dawa inapatikana kwenye mashamba ya watu binafsi. Miongoni mwa mimea dawa hiyo ni; Mhungulungu, Mnyonyo, Bangalala, Kiguti, Kimakasa, Kilimandembwe, Kinunu, Lihungutua, Limulimuli, Lipasa, Mhanza, Mwambandusi na Mverevere. Hali hii inaonesha kuongezeka kwa uhifadhi wa mimea dawa katika maeneo ya Milima ya Tao la Mashariki. Aidha, mimea dawa 122 imetambuliwa kwenye maeneo hayo ambayo yanahitaji kuhifadhiwa kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

**113.** ***Mheshimiwa Spika*****,** TAFORI imefanya utafiti wa kuchunguza afya ya udongo katika maeneo yaliyopandwa miti ya misindano na mikaratusi kwa mzunguko wa pili (*second rotation*) kwa lengo la kutambua virutubisho vitakavyowezesha upatikanaji wa mazao bora ya miti yakiwemo mbao, nguzo, vinia na tetefya. Utafiti huu umefanyika katika Shamba la Miti la Sao Hill ambapo matokeo yameonesha kuwepo kwa upungufu wa madini aina ya *Phosphorus* na *Nitrogen* na ongezeko la madini aina ya *Potassium* na kaboni iliyokusanyika kutokana na kuoza kwa majani ya miti hasa kwenye tabaka la juu la udongo. Upungufu wa madini ya *Phosphorus* na *Nitrogen*

umeonesha kutoathiri ukuaji wa miti kwa kuzalisha mita za ujazo zipatazo 71 kwa hekta ikilinganishwa na mita za ujazo zipatazo 68 kwa hekta kwenye maeneo yaliopandwa miti kwa mzunguko wa kwanza. Utofauti wa mita za ujazo umetokana na uwepo wa mboji itokanayo na majani ya miti yaliyooza. Aidha, ubora wa mbao kutoka kwenye mizunguko yote miwili haukutofautiana. Kutokana na matokeo haya, inashauriwa kusifanyike uchomaji wa majani na mabaki mengine ya miti wakati wa uandaaji wa mashamba ili kuendelea kulinda rutuba ya udongo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFORI inatekeleza mradi wa utafiti ujulikanao kama Mimea ya Asili kwa Mazingira na Watu (Native Plants for Environment and People - NATIVE PEP) wenye lengo la kudhibiti mimea vamizi kwenye maeneo ya wafugaji hususan katika mikoa ya Arusha (Longido) na Kilimanjaro (Siha). Aidha, mradi unatarajiwa kuwezesha urudishaji wa uoto wa asili katika maeneo yaliyovamiwa na mimea vamizi ambapo katika awamu ya kwanza majaribio ya mbinu mbalimbali za kurudisha uoto wa asili yameanzishwa katika vijiji vya Tingatinga Wilaya ya Longido na Mawasiliano Wilaya ya Siha. Ufuatiliaji wa majaribio unaendelea ili kubaini mbinu sahihi zitakazotumika kurejesha uoto wa asili katika maeneo hayo. Utafiti huu unasaidia kuimarisha ulinzi dhidi ya mimea vamizi kwenye hifadhi za misitu na wanayamapori hapa nchini. Kwa upande mwingine, TAFORI inashirikiana na Taasisi nyingine za Serikali na wataalam kutoka nchini Cuba kufanya tathmini ya aina, mtawanyiko, athari na mbinu za udhibiti wa mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa. Matokeo ya awali yamebaini uwepo wa aina mbalimbali za mimea vamizi kama vile; *Gutenbergia cordifolia, Bidens schimperi, Parthenium hysterophorus, Verbena officinalis, Chromolaena odorata, Opuntia vulgaris, Datura stramonium, Parthenium hysterophorus, Eichhornia crassipes* (Water Hyacinth), na *Salvinia species*. Kufuatia matokeo hayo, TAFORI inaendelea

kushirikiana na watafiti wa ndani na nje ya nchi kubuni mbinu zitakazowezesha kudhibiti uvamizi na kuenea kwa mimea vamizi katika maeneo ya hifadhi na vijiji.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFORI imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kukarabati jengo la Kituo cha Utafiti cha Malya mkoani Mwanza na kuanza ujenzi wa ofisi za Kituo cha Utafiti Tabora. Vilevile, taasisi imewezesha watumishi 29 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi pamoja na kupandisha vyeo watumishi 28.

#### 4.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki-Tabora – (BTI)

**116.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki - Tabora (BTI) kina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada (Technician Certificate) na Stashahada (Ordinary Diploma) ya Ufugaji Nyuki, mafunzo ya muda mfupi, Ushauri juu ya masuala ya Ufugaji Nyuki na Utafiti. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 287 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimefanya tafiti mbili (2) zinazohusu tathmini ya matumizi ya mizinga ya kisasa katika shughuli za ufugaji nyuki; na masuala yanayoathiri matumizi ya mizinga ya kisasa kwa wafugaji nyuki katika Wilaya ya Sikonge. Matokeo ya tafiti hizi yameonyesha kuwa bado kwa kiasi kikubwa wafugaji nyuki wanaendelea kutumia mizinga ya kienyeji ambayo huzalisha kiwango kidogo cha asali.

**117.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Chuo kilitoa ushauri wa kitaalamu juu ya masuala mbalimbali ya mnyororo wa thamani wa Ufugaji Nyuki kwa vikundi 30 vya wafugaji nyuki na wadau 1,726 kutoka wilaya za Meatu,

Maswa, Magu, Sikonge, Mlele, Tanganyika, Kasulu, Kibondo, Buhigwe, Manyoni, pamoja na Zanzibar. Katika hatua nyingine, Chuo kimekamilisha ukarabati wa nyumba mbili (2) za watumishi na kinaendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara na bweni la wasichana. Aidha, Chuo kimewezesha mtumishi mmoja (1) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 16 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Sambamba na hilo, Chuo kimeshiriki katika matukio na maonesho mbalimbali kama Sabasaba, Nanenane, Siku ya Misitu Duniani na maonesho asali kwa lengo la kutangaza majukumu yake kwa wadau ili kuongeza idadi ya wadau watakaohitaji kuhudumiwa na chuo katika masuala yanayohusu sekta ndogo ya nyuki.

#### 4.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Viwanda vya Misitu kina jukumu la kutoa mafunzo na ujuzi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu kwa ngazi ya Astashahada na stashahada. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Chuo kimedahili wanafunzi 388 wanawake ni asilimia 52 na wanaume ni asilimia 48. Ongezeko la udahili wa wanawake umetokana na hamasa ya Serikali pamoja na fursa nyingi zilizopo katika sekta ya misitu.

**119.** ***Mheshimiwa Spika;*** Chuo pia kimetoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalamu kwa jamii ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, wananchi 250 wamepata mafunzo katika maeneo ya upangaji madaraja na matumizi bora ya mbao, udhibiti wa moto misituni, biashara ya mazao ya misitu na kaboni, ufundi seremala na uchakataji magogo kwa kutumia teknolojia za kisasa. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, ikiwa ni pamoja na kuanza ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike litakalochukua wanafunzi 200, ununuzi wa mitambo ya kukaushia na kutibu mbao pamoja vifaa vya maabara ya

kupimia ubora wa mazao ya misitu. Katika hatua nyingine, Chuo kimewezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na tatu (13) mafunzo ya muda mfupi kwaajili ya kuboresha utendaji kazi.

#### 4.3.2.6 Chuo Cha Misitu, Olmotonyi - FTI

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Misitu, Olmotonyi kina jukumu la kutoa mafunzo ya ufundi sanifu wa misitu, mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalamu wa misitu na uhifadhi wa mazingira. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimedahili na kutoa mafunzo ya astashahada na stashahada ya misitu kwa wanafunzi 884. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya kuzuia na kudhibiti moto kwa maafisa misitu 50 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Vilevile, Chuo kimesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Chuo Kikuu cha HAMK cha nchini Finland, Chuo cha Misitu ya Luua cha nchini Estonia na Chuo cha Misitu Zambia cha nchini Zambia kwa ajili ya kujengeana uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi sanifu na ufundi stadi wa misitu na uhifadhi wa mazingira.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufanisi wa kazi, Chuo kimewezesha watumishi watano (5) kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 10 kupata mafunzo ya muda mfupi. Katika kuongeza chachu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, Chuo kiliotesha miche ya miti 110,000 ambapo miche hiyo imepandwa katika Shamba la Miti la Chuo.

#### 4.3.2.7 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko una jukumu la kuwezesha na kugharamia shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko umetoa ruzuku ya Shilingi 1,835,603,754.16 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi 143 inayoendelea na Shilingi

1,183,393,500.00 kwa ajili ya kugharamia utekelezaji miradi mipya 96 ikiwemo miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kurahisisha utoaji wa mafunzo katika Chuo cha Mafunzo ya Viwanda vya Misitu (FITI) na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI). Aidha, Mfuko umewezesha uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni, uanzishwaji wa mashamba ya miti, na uboreshaji uhifadhi wa misitu kupitia ufugaji nyuki na miradi ya utengenezaji na matumizi ya nishati mbadala. Miradi hiyo inatekelezwa katika Wilaya 97 za mikoa 26 ya Tanzania Bara. Vilevile, Mfuko umetoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kuandaa maandiko ya kuomba ruzuku kwa ajili ya miradi ya uhifadhi kwa wadau 1,864 ikihusisha vikundi (164) vyenye jumla ya washiriki 1,464, shule na watu binafsi (102), Asasi zisizo za kiserikali (73), Taasisi za Serikali (27) na Maafisa Misitu (64) wa TFS na Halmashauri. Kufuatia mafunzo hayo, maombi ya ruzuku zaidi ya 600 yamewasilishwa.



*Jengo la mihadhara linaloendelea kujengwa katika Chuo cha BTI.*

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Mfuko umeendelea kutoa ufadhili wa masomo katika Shahada ya Uzamili na Uzamivu nje ya nchi katika fani zenye wataalam wachache au ambazo hazina wataalam nchini ambazo ni magonjwa ya miti (*Forest pathology*) na uboreshaji wa vizazi vya miti (*Tree breeding*). Mafunzo yametolewa kwa watumishi 3 kutoka TFS, TAFORI na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA). Aidha, Mfuko umewezesha TAFORI kukamilisha tafiti 5 za kimkakati ikiwemo utafiti wa kuongeza mchango wa Sekta

ya Misitu na Nyuki katika Pato la Taifa. Vilevile, Mfuko ulitoa tuzo kwa wanafunzi 27 waliofanya vizuri katika mafunzo ya nadharia na vitendo katika ngazi ya Astashahada (16), Stashahada (8) na Shahada (3) ya misitu.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko uliwezesha vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC); Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Kamati ya Kusimamia Utekelezaji wa Mwongozo wa Mazao ya Misitu yaliyohandisiwa (EWP); na Kikundi kazi cha Misitu kilichopo chini ya Baraza la Taifa la Biashara (TNBC). Aidha, Mfuko uliwezesha na kushiriki Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (COP-29) kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Jijini Baku, Azerbaijan. Vilevile, Mfuko uliwezesha Kongamano la Tatu la Kisayansi la TAFORI kuhusu mchango wa utafiti katika kurejesha mandhari ya misitu na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa Mfuko unaongeza vyanzo vyake vya mapato ili kuwezesha na kugharamia ipasavyo shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki, Mfuko umeandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kutafuta fedha (*Fundraising Strategy*). Sambamba na hilo, Mfuko umeboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua magari mawili (2); kugharamia mafunzo ya watumisihi wa Mfuko, kuandaa miongozo ya utekelezaji wa Muundo na Mgawanyo wa majukumu ya Mfuko na kununua kiwanja na kuandaa mchoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko Jijini Dodoma.

### 4.3.3 Sekta ya Utalii

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii ndani na nje ya Nchi. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa

ya Utalii ya Mwaka 1999, Sheria ya Utalii, Sura ya 65 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania, Sura ya 364. Kulingana na Muundo, jukumu hilo linatekelezwa kupitia Idara ya Utalii inayosimamia maendeleo ya utalii, udhibiti wa ubora na huduma; Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) iliyokasimiwa dhamana ya kutangaza na kuhamasisha utalii ndani na nje ya nchi; na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) wenye jukumu la kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani ya utalii na ukarimu.

#### 4.3.3.1 Idara ya Utalii

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuendeleza na kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imebaini vivutio vipya 337 vya utalii. Vivutio vilivyobainishwa vinajumuisha vivutio vya asili, visivyo vya asili, utamaduni, kihistoria na kidini. Kupitia zoezi hilo, vivutio 193 vimekidhi vigezo vya kuendelezwa na kutangazwa. Vivutio hivyo vipo katika mikoa ya Mtwara (19), Lindi (22), Mbeya (28), Songwe (16), Katavi (8), Kigoma (16), Iringa (23), Njombe (26), Ruvuma (32) na Rukwa (14). Miongoni mwa vivutio vilivyobainishwa ni pamoja na Boma la Mjerumani Newala Lindi, Tamasha la Utamaduni la MAKUYA (Manispaa ya Mtwara) na Mkomaindo (Masasi) Tukio la Kuhama kwa Nyangumi linalojulikana kama *Humback whales migration* (Msimbati), Maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi na eneo la fukwe za ziwa Tanganyika. Zoezi hilo limelenga pia kupunguza utegemezi kwenye zao la wanyamapori pamoja na kuongeza siku za watalii kukaa nchini sambamba na kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Hatua inayofuata ni kuvisajili vivutio hivyo vya utalii kama ambavyo Sheria ya Utalii Sura ya 65 inavyoelekeza ili viweze kuendelezwa na kutangazwa.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuboresha mazingira ya biashara ya utalii na kuvutia wawekezaji wa huduma mbalimbali za utalii, Wizara imefanya maboresho ya Kanuni ya Ada na Tozo ya mwaka 2015 ambapo hivi sasa Ada zote za Leseni za Biashara za Utalii - TTBL zinalipwa kwa Shilingi za Kitanzania badala ya Dola ya Marekani. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara ilianza kutekeleza mageuzi katika mifumo ya tozo mbalimbali ili kuipa unafuu sekta binafsi. Mathalani, tumepunguza tozo ya *Daraja la Nyota 5 kutoka USD 2,500 hadi USD 1500; Daraja la Nyota 4 kutoka USD 2,000 hadi USD 1000; Daraja la Nyota 3 kutoka USD 1,500 hadi USD 500; Daraja la Nyota 2 kutoka USD 1,200 hadi USD 300; Daraja la Nyota 1 kutoka USD 1,000 hadi USD 200*. Gharama hizi sasa zinalipwa kwa shilingi ya Tanzania. Vilevile, Wizara imefuta malipo ya waongoza watalii (park fees) walizokuwa wakitozwa kila walipokuwa wakiingia hifadhini kuingiza wageni. Sasa kila muongoza watalii mwenye leseni hai na halali hatatozwa chochote. Pia, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la ada ya Wakala wa kupandisha mlima kutoka Dola za Marekani 2,000 hadi Shilingi za Tanzania milioni tatu (3,000,000). Sambamba na hilo, Wizara imeanza kutekeleza punguzo la gharama ya leseni ya waongoza watalii (TTBL) kutoka Dola za Marekani 50 hadi Shilingi 35,000 tu kwa mwaka. Wizara na Serikali kwa ujumla itaendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi katika kuongeza ufanisi wa sekta za uhifadhi na utalii kupitia vikao vya kisekta chini ya TNBC lakini na mikutano ya mara kwa mara na wadau.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kutekeleza mifumo ya kidijitali ambapo umeanza utaratibu wa wadau kujisajili na kupata leseni za biashara ya utalii kwa njia ya mtandao wa *MNRT Portal* ambayo imepunguza muda na gharama za upatikanaji wa leseni hizo. Kutokana na maboresho hayo, idadi ya wakala wa biashara za utalii nchini imeongezeka kutoka 3,019 kwa mwaka 2023 hadi

kufikia 4,316 Aprili, 2025 na idadi ya Waongoza Watalii imeongezeka kutoka 5,076 mwaka 2023 hadi kufikia 8,914 Aprili, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 54.9. Sambamba na maboresho hayo, Kanuni ya Mabalozi wa Hiari wa Utalii ya mwaka 2025 imetungwa kwa lengo la kutoa miongozo ya uteuzi wa Mabalozi wa Hiari wa kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza kazi ya uhakiki na utambuzi wa huduma za malazi, Wizara ilifanya zoezi uhakiki na utambuzi wa huduma za malazi katika mikoa yote 26 hadi kufikia Aprili, 2025. Aidha, jumla ya huduma za malazi 2,038 mpya zilifanyiwa uhakiki na utambuzi zikiwa na Mtawanyiko wa Dar es Salaam (47), Arusha (90), Mbeya (47), Mwanza (106), Mara (125), Manyara (52), Kilimanjaro (53), Tanga (87), Morogoro (62), Pwani (37), Dodoma (293) Iringa (179), Singida (108) Kagera (165), Geita (148), Kigoma (115), Njombe (30), Songwe (44), Rukwa (26), Katavi (37), Tabora (20), Shinyanga (14), Simiyu (4), Lindi (42), Mtwara (55) na Ruvuma (52). Sambamba na hilo, kati ya huduma za malazi hizo mpya zilizo hakikiwa, huduma za malazi 362 zimekidhi vigezo vya kuwa na sifa ya kupangwa katika viwango vya ubora wa nyota.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara imeendelea na ukaguzi wa Wakala wa biashara za utalii na waongoza watalii katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Njombe, Mbeya na Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kuwa wadau hao wanazingatia na kufuata taratibu zilizopo za biashara ya utalii. Aidha, kupitia ukaguzi huo, wakala 229 na waongoza wageni 101 walisajiliwa na kulipia Leseni ya Biashara ya Utalii (TTBL) na leseni ya Waongoza Watalii, ambapo jumla ya Shilingi 719,259,600.00 zilikusanywa. Awamu ya pili ya kazi hii inatarajiwa kuendelea kufanyika katika mikoa 14 iliyobaki na katika malango ya hifadhi nchini.

**132. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika mikutano na matukio ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo: Mkutano wa 122 wa Baraza Tendaji la Shirika la Utalii Duniani (UN-Tourism Executive Council) uliofanyika nchini Colombia; Mkutano wa 67 wa Shirika la Utalii Duniani Kamisheni ya Utalii Afrika (UN Tourism CAF) uliofanyika sambamba na Mkutano wa pili wa *Brand Africa* nchini Zambia. Wizara pia imeshiriki katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Ushirikiano wa Kidiplomasia Kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China Jijini Dar es Salaam ambapo ulifanyika uzinduzi wa Filamu ya *Amazing Tanzania* iliyooneshwa kwa zaidi ya watu 1,000. Lengo la filamu hiyo ni kuvutia watalii wengi zaidi kutoka soko la China ambalo ni moja ya masoko ya utalii ya kimkakati. Aidha, kupitia filamu hiyo, idadi ya watalii kutoka China imeongezeka kutoka wageni 45,463 kwa mwaka 2023 hadi kufikia wageni 71,140 mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 56.5. Vilevile, Kampuni ya Changsha Utopia ya nchini China ilirekodi kipindi maarufu cha uhalisia cha *Divas Hit the Road* katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo kilioneshwa katika Televisheni ya *Hunan* na kutazamwa na watu takriban bilioni 1.2 ndani ya China na nchi za jirani. Halikadhalika, Kampuni hiyo imefanikiwa kuleta watu wawili mashuhuri wa nchini China mwezi Aprili, 2025 ili kurekodi kipindi cha uhalisia kinachojulikana kama *Swapping Lives* katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi za Taifa za Tarangire na Ziwa Manyara.

**133. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kukuza zao la utalii kupitia majukwaa, mikutano na matukio nchini. Juhudi hizo zimefanikisha Tanzania kuwa mwenyeji wa mikutano ya Kimataifa pamoja na majukwaa mbalimbali kama vile: Jukwaa la Pili la Kikanda la Utalii wa Vyakula la Shirika la Utalii Duniani (Second UN Tourism Regional Forum on Gastronomy Tourism

for Africa) uliofanyika tarehe 23 hadi 25, Aprili 2025 Jijini Arusha. Jukwaa hilo lilihudhuriwa na Mke wa Rais wa Jamhuri ya Zimbabwe, Dkt. Auxillia C. Mnangagwa, Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Maafisa Waandamizi wa Serikali kutoka nchi mbalimbali za Ukanda wa Afrika wanaohusika na utalii; wawakilishi wa balozi za nchi mbalimbali za ukanda wa Afrika na baadhi ya taasisi za Kimataifa; wataalamu wa utalii na mapishi kutoka Sekta Binafsi ya utalii nchini na nje ya nchi. Mgeni Rasmi wa Jukwaa hilo alikuwa Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani Bw. Zurab Pololikashvili.




*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), akikabidhiwa cheti na Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani, Bw. Zurab Pololikashvili, cha ufadhili wa masomo kwa njia ya mtandao katika fani ya mapishi wakati wa hafla ya ufunguzi wa Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Chakula la Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) kwa Kanda ya Afrika, jijini Arusha.*

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutambua na kuhamasisha wadau kuendeleza utalii, Wizara imeandaa na kuzindua tuzo za Uhifadhi na Utalii zijulikanazo kama *The Serengeti Awards*

zenye lengo la kutambua mchango wa wadau katika kuendeleza uhifadhi na kutangaza utalii. Uzinduzi wa tuzo hii ulifanyika Desemba, 2024 Jijini Arusha na kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 500 ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitunukiwa Tuzo ya Kiongozi Mwenye Maono (Visionary Leadership) ikiwa ni sehemu ya kutambua mchago wake kwenye mafanikio ya Sekta ya Maliasili na Utalii. Vilevile, Wizara ilitoa Tuzo 10 za Heshima na Shukrani kwa wadau mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kutambua michango yao katika Uhifadhi wa Maliasili, Malikale pamoja na uendelezaji utalii. Tuzo hizi zitaendelea kutolewa kila mwaka ili kuendelea kuhamasisha na kutambua michango mbalimbali ya wadau wa Sekta ya Maliasili na Utalii.

#### 4.3.3.2 Tozo ya Maendeleo ya Utalii – TDL

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy-TDL) ina jukumu la kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uendelezaji utalii nchini ikiwa ni pamoja na kuendeleza mazao ya utalii, kudhibiti ubora wa huduma za biashara za utalii, kutangaza utalii ndani na nje ya nchi, kuimarisha miundombinu ya utalii, kujenga uwezo na kufanya tafiti katika sekta ya Utalii. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, TDL imewezesha kuanza kwa ujenzi wa baadhi ya miundombinu ya utalii, kubaini vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji, kuwezesha uhakiki (inventory) wa huduma za malazi na ukaguzi wa wakala wa biashara ya utalii ili kuboresha huduma za kitalii na ukarimu.

**136.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuendeleza kampeni ya kutangaza utalii, TDL imewezesha uzinduzi wa filamu ya *Amazing Tanzania* pamoja na kufanikisha sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na China. Aidha, TDL imewezesha uandaaji na ushiriki wa Tanzania katika maonesho, matamasha na matukio ya utalii ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Jukwaa la Pili la Utalii

wa Chakula (Second UN Tourism Gastronomy) na uzinduzi wa tukio la Tuzo za Utalii. Katika hatua nyingine, TDL imewezesha uratibu na kushiriki katika misafara ya utangazaji utalii (tourism roadshow) katika nchi mbalimbali; na kuandaa ziara za mafunzo (Fam Trip) kwa diaspora, mawakala wa usafiri wa kimataifa, watu mashuhuri, waandishi pamoja na vyombo vya Habari ili kuongeza uelewa kuhusu vivutio vya utalii. Aidha, imewezesha kufanyika mazungumzo ya awali na vilabu vikubwa vya mpira wa miguu duniani na vyombo vya habari vya kimataifa kama sehemu ya jitihada za kukuza utalii kupitia ushirikiano wa kimkakati katika kutangaza vivutio vyetu duniani. Wizara itaendelea kuhakikisha usimamizi thabiti na wenye kuleta tija wa fedha hizi.

#### 4.3.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Utalii Tanzania ina jukumu la kutumia mbinu mbalimbali za utangazaji utalii ili kuifanya Tanzania iwe kituo kikuu kimojawapo mashuhuri cha utalii duniani. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi imeendelea kuratibu ushiriki wa nchi katika kuhamasisha na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali Duniani. Katika kipindi husika, Bodi imetangaza utalii kupitia maonesho saba (7) ya Kimataifa katika nchi ambazo ni masoko ya utalii ya msingi na kimkakati. Maonesho hayo ni pamoja na: WTM – London (Uingereza), ITB – Berlin (Ujerumani), OTM (India), FITUR (Hispania), Gita Mahotsav (India), Qatar Travel Market (Qatar) na Magical Kenya Tourism Expo (Kenya). Kupitia maonesho hayo takriban makampuni 150 ya nchini yalifanya mazungumzo na wafanyabiashara na watalii wa nchi hizo. Ushiriki wa Tanzania katika maonesho hayo umeendelea kuwa chachu ya ongezeko la watalii kutoka Nchi husika. Mathalan, idadi ya watalii kutoka Ujerumani imeongezeka kutoka watalii 23,615 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 102,798 mwaka 2024 sawa na asilimia 335.3.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kushirikiana na Ofisi za Balozi za Tanzania katika kutangaza utalii kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo kuratibu ziara za mafunzo kwa wakala wa utalii, waandishi wa habari na watu mashuhuri; kuwapatia nyenzo za utangazaji utalii; kuratibu maonesho na misafara ya utangazaji utalii; kuratibu makala za utangazaji utalii pamoja na kuratibu "branding" za Ofisi za Balozi zilizopo nje ya nchi. Bodi kwa kushirikiana na Ofisi ya Ubalozi za Tanzania katika masoko ya kimkakati imeandaa na kushiriki katika misafara miwili ya utangazaji utalii (Roadshows) ya nchini India (New Delhi, Chennai, na Bengalore); na Nchi za Ulaya Magharibi ambazo ni Ujerumani (Cologne), Uingereza (London na Manchester), Ubelgiji (Antwerp) na Uholanzi (Amsterdam) ambapo jumla ya wakala wa biashara za utalii 51 kutoka nchini Tanzania walikutana na makampuni 790 na kufanya biashara zinazohusiana na utalii. Jitihada hizo zimechochea ongezeko la idadi ya watalii kutoka soko la kimkakati la India kufikia 63,391 mwaka 2024 kutoka 54,558 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Ofisi zingine za Balozi za Tanzania kwenye masoko ya kimkakati ambayo Bodi imeshirikiana nayo ni Brazil na Canada kwa kuratibu ziara ya mafunzo kwa wakala wa utalii 19. Wakala hao wanatarajiwa kuitangaza Tanzania katika Nchi zao na hivyo kuchochea ongezeko la watalii ikizingatiwa kuwa Brazil na Canada ni miongoni mwa Nchi zenye uchumi mkubwa Duniani. Vilevile, Ofisi za Balozi za Tanzania nchini Nigeria, Ujerumani, Sweden, Zimbabwe, Msumbiji, Rwanda na Zambia walipatiwa nyenzo za utangazaji utalii kama vile *QR codes* zenye taarifa za vivutio vya utalii, video na vipeperushi. Ushirikiano wa Bodi na Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi umechochea ongezeko la watalii kutoka Nchi husika. Mathalan, idadi ya watalii kutoka Uingereza imeongezeka kutoka watalii 27,667 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 88,345 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 219.3.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeandaa makala mbili (2) za kivutio cha Kisiwa cha Mafia ambapo moja (1) imeendelea kurushwa katika kituo cha televisheni *Tanzania Safari Channel* na nyingine inatumika katika matukio ya kimataifa kwa lengo la kukitangaza Kisiwa hicho kama kivutio cha ikolojia. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Moments Entertainment* kutoka Afrika Kusini imeratibu maandalizi ya makala moja (1) inayolenga kuonesha mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Vilevile, Bodi imeshiriki katika uzinduzi wa Filamu ya *"Tantalizing Tanzania"* Jijini Mumbai, India iliomhusisha Bi. Shakti Mohan, Mcheza Muziki maarufu nchini humo mwenye ushawishi mkubwa anaefuatiliwa na wafuasi zaidi ya milioni 17.5 katika mitandao ya kijamii. Kwa upande mwingine, Bodi imeendelea kutangaza utalii kupitia mitandao ya kijamii kwa kutengeneza maudhui na kuyatangaza kwenye majukwaa mbalimbali ikiwemo *Instagram, Linkedin, X*, *TikTok, Facebook* na *Youtube*.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ushiriki wa Bodi katika msafara wa utangazaji utalii nchini India, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Jio Creative Lab* imeratibu utayarishaji wa makala ya kutangaza utalii katika soko la India na Bara la Asia. Makala hiyo imehusisha watu mashuhuri wane (4) katika tasnia ya filamu wanaoitwa Kunwar Amar Jeet Singh, Anushka Sen, Siddharth Nigam na Sumedh Vasudev Mudgalkar ambao wana wafuasi zaidi ya milioni 50 kwenye mitandao ya kijamii kutembelea Hifadhi za Serengeti na Kilimanjaro; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Kisiwa cha Mafia. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Kampuni ya *Jio Creative Lab*, inakamilisha uhariri wa maudhui ya makala hizo, sambamba na kufanya makubaliano na vyombo vya habari vya India vitakavyorusha makala husika katika lugha mbalimbali za nchi hiyo ikiwemo Hindi, Bengali, Tamil, Gujarati na Telegu. Kupitia ushirikiano kati ya nchi hizi mbili, idadi ya watalii kutoka India imeendelea kuongezeka kutoka watalii 12,393 mwaka 2020 hadi kufikia

watalii 63,391 mwaka 2024 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 411.5.




*Mwenendo wa idadi ya watalii kutoka nchini India waliotembelea Tanzania kati ya mwaka 2020 na 2024.*

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutangaza utalii, Bodi iliratibu onesho la Nane la "Swahili International Tourism Expo (S!TE 2024)" kuanzia tarehe 11 hadi 13 Oktoba, 2024 Jijini Dar es Salaam. Kupitia Onesho hilo, waoneshaji 92 na wanunuzi 124 kutoka nchi 24 katika mabara ya Amerika, Ulaya, Asia na Afrika walishiriki onesho husika lililoambatana na Kongamano la pili la Uwekezaji wa Sekta ya Utalii lenye washiriki takriban 300. Aidha, onesho hilo lilifuatiwa na ziara za mafunzo (Familiarization trips) kwenye vivutio 7 vya utalii ikiwemo Hifadhi za Taifa Mikumi, Milima ya Udzungwa, Nyerere na Ruaha; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; Hifadhi ya Msitu Pugu; Eneo la Kihistoria la Magofu ya Kilwa; Kisiwa cha Mafia; na Zanzibar. Onesho la S!TE limeendelea kuwa fursa ya kuwakutanisha wadau wa utalii kutoka ndani na nje ya Nchi kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza ushirikiano wa kibiashara.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano na Mabalozi wanaowakilisha nchi zao nchini Tanzania pamoja na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Bodi kwa kushirikiana

na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeratibu ziara ya mafunzo kwenye Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Zanzibar. Kundi hilo la Viongozi Mashuhuri lilihusisha Waheshimiwa Mabalozi wa: Angola, Burundi, Comoros, Cuba, Denmark, Egypt, Ethiopia, Iran, Kenya, Korea, Morocco, Rwanda, Saudi Arabia, Somalia, Sudan, Syrian Arab Republic, Uturuki, Zimbabwe na Wawakilishi wa Mashirika ya: *International Labour Organization, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization* na *United Nations Population Fund*. Ziara hiyo imewezesha kuwajengea uwezo Mabalozi hao kuhusu utalii wa Tanzania ili waweze kuutangaza katika Nchi zao kwa lengo la kuvutia watalii na wawekezaji.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Bodi imeratibu ziara nne (4) za mafunzo kwa washiriki 78 ikiwemo wakala wa utalii, waandishi wa habari, wazalishaji wa makala, makundi maalum na watu mashuhuri ili kuwajengea uelewa juu ya vivutio vya utalii wa Tanzania. Washiriki hao wametokea nchi za Brazil, Canada, India na Tanzania ambapo walipata fursa ya kutembelea Hifadhi za Taifa Serengeti, Kilimanjaro, Mikumi na Tarangire; Zanzibar; Kisiwa cha Mafia na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa kutambua mchango wa makundi ya watu makundi maalum katika uhifadhi na uendelezaji utalii, Bodi iliratibu ziara ya mafunzo kwa washiriki 50 makundi maalum kutembelea Hifadhi ya Taifa Mikumi. Jitihada hizi zimelenga ushirikishwaji wa makundi maalum kutembelea na kutangaza vivutio vya utalii.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Utalii Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi za Wizara na Sekta Binafsi imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani ya nchi kupitia maonesho, matukio na kampeni za utangazaji utalii. Bodi iliandaa kampeni moja ya utangazaji utalii "*Funga Mwaka Kijanja, Talii*" ambapo zaidi ya watalii wa ndani 103,785 walitembelea vivutio mbalimbali

pamoja na kushiriki katika kampeni moja ya "*Twenzetu Kileleni*" ambapo zaidi ya watalii 400 wa ndani walishiriki katika kupanda Mlima Kilimanjaro. Bodi pia ilishiriki matukio mbalimbali ikiwemo "*Churchill Comedy Show – Arusha*" ambayo ilihudhuriwa na watu takriban 1,800, "*Bata la Funga Mwaka – Arusha*" iliyohudhuriwa na takriban watu 5,000, Uzinduzi wa Wiki ya Simba na Miaka 60 ya Hifadhi ya Taifa Mikumi iliyohudhuriwa na takriban watu 1,232, "*Great Ruaha Marathon-Iringa*" iliyohudhuriwa na takriban watu 600 pamoja na "*Rombo Marathon and Festival – Kilimanjaro*" iliyohudhuriwa na takriban watu 1,200.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuratibu ushiriki wa wadau wa utalii katika maonesho ya ndani ya nchi kwa ajili ya kutangaza utalii ikiwemo: Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Maonesho ya Wakulima (Nanenane), *Simiyu Cultural* and *Tourism Festival, Zanzibar Tourism and Investment Show, Zanzibar Sports Bonanza, Usandawe Festival,* Maonesho ya Wiki ya Vijana Mwenge, *Serengeti Cultural Festival,* Tamasha la Taifa la Utamaduni Ruvuma (Utamaduni Festival), *Nyangumi Festival*, *Khanga Festival*, *Landrover Festival*, *Meru Forest Adventure Race Tourism Festival, Maasai Festival*, *Kizimkazi Festival*, na *Mafia Festival*. Maonesho haya yameendelea kuwa chachu ya ongezeko la watalii wa ndani na mapato yatokanayo na shughuli za utalii.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushirikiano na kutangaza utalii wa Tanzania sehemu mbalimbali Duniani, Bodi imesaini Hati ya makubaliano (MoU) na mashirika ya ndege mawili ambayo ni Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Shirika la Ndege la Uturuki (Turkish Airlines). Kupitia makubaliano hayo, Bodi itapata fursa ya kutangaza vivutio vya utalii katika ndege 490 za Shirika la Ndege la Uturuki ambazo hufanya safari katika miji zaidi ya 350 Duniani. Aidha, Bodi ipo

kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wa makubaliano hayo ikiwemo kuandaa maudhui yatakayorushwa ndani ya ndege sambamba na kuratibu kampeni za pamoja. Vilevile, Bodi inaendelea na majadiliano ya utangazaji utalii na mashirika ya ndege ya *Precision, Emirates, Ethiopian Airlines, Qatar Air* na *Air Asia*, kukamilisha mazungumzo na vilabu mbalimbali vya michezo na kuendeleza misafara ya kimkakati ya kutangaza utalii (roadshows).

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza mazao ya utalii wa meli na fukwe, Bodi imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuratibu mapokezi ya meli sita (6) za kitalii zilizokuwa na watalii 3,157 ambapo Meli ya *OCI Riveira* ilikuwa na watalii 1,160, *Seabourn Sojourn* (620), *MS Europa* (443) *Hebridrean Sky* (172), *Ledumon't D'urville* (278) na *Le Bougainville* (484). Watalii hao wametokea masoko ya kimkakati ikiwemo Ujerumani, Ufaransa, Canada, Uingereza, Australia na Marekani ambapo walipata fursa ya kutembelea vivutio mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam (City Tour); Hifadhi ya Urithi wa Utamaduni wa Dunia ya Magofu ya Kale Kilwa Kisiwani na Songo Mnara; Mji wa Kihistoria Bagamoyo; na Hifadhi za Taifa Nyerere na Serengeti. Ujio wa watalii hao unatokana na jitihada za serikali za kuendeleza zao la utalii wa meli.

#### 4.3.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Taifa cha Utalii kina dhamana ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika fani za utalii na ukarimu. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Chuo kimetoa mafunzo ya umahiri (Competence Based Education and Training - CBET) kwa jumla ya wanafunzi 1,398 katika ngazi ya Astashada na Stashahada sawa na asilimia 93.2 ya lengo la wanafunzi 1,500.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 214 walifanya mafunzo maalum ya programu ya Uanagenzi katika fani za ukarimu chini ya ufadhili wa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha kiwango cha ubora wa huduma kwa watalii, Chuo cha Taifa cha Utalii kimeendelea na mkakati wa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa utalii. Hadi April 2025, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa jumla ya washiriki 1,377 ambapo washiriki 40 wamepata mafunzo ya umahiri wa uratibu wa matukio (Event Management Masterclass); 33 mafunzo ya umahiri wa Usafirishaji na Utalii (Travel and Tourism Masterclass); 15 Mafunzo ya umahiri wa Huduma za Ukarimu (Hospitality Masterclass); 14 Mafunzo ya Upishi wa Melini (Ship Cooks) kwa ushirikiano na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI); 100 Mafunzo ya huduma bora za vinywaji; 220 mafunzo kwa Maafisa Uhamiaji na 955 mafunzo ya Huduma bora kwa Watalii yaliyotolewa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari wa vyeo mbalimbali wa Jeshi la Polisi Tanzania. Aidha mafunzo haya ni njia muhimu katika kuboresha huduma kwa wageni ili kuimairisha sekta ya Utalii na kuongeza Pato la Taifa.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuongeza uwezo wa kudahili pamoja na kutoa mafunzo yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira, Chuo kimeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo jipya la taaluma kwa kampasi ya Arusha, ambao umefikia asilimia 65 na kufanya ukarabati wa miundombinu ya jengo la mafunzo kwa kampasi ya Bustani uliofikia asilimia 30.

*Kushoto ni hatua iliyofikiwa ya mradi wa Ujenzi wa jengo la taaluma la Chuo cha Taifa cha Utalii Kampasi ya Arusha na kulia ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipotembelea jengo hilo.*

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo kimeendelea na jitihada za kujitangaza ili kufikia lengo ya udahili wa wanafunzi 1,500 kwa kutekeleza mikakati mbalimbali, ikiwemo kufanya huduma mkoba (Outreach programs) za uhamasishaji, kushiriki maonesho pamoja na kuandaa vipindi vya televisheni na redio kwa ajili ya kutangaza programu za mafunzo kwa wanafunzi wa shule za Sekondari na wadau mbalimbali wa utalii. Aidha, Chuo kilipata ushindi wa pili kama banda bora la ubunifu kwenye maonesho ya Kitaifa ya Kazi za Utamaduni na Sanaa yaliyoandaliwa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Maonesho hayo yalihitimishwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Prof. Palamagamba Kabudi.

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, chuo kimeendeleza ushirikiano wa kimataifa na kubadilishana uzoefu kati ya wanataaluma na waendeshaji wa huduma za kitalii kwa kuandaa Kongamano la 3 la Kimataifa la Kuunganisha Wanataaluma na Wadau wa Utalii na Ukarimu katika Nchi Zinazoendelelea (The 3$^{rd}$ Conference in Linking Industry with Academia in the Tourism and Hospitality in Developing Countries (LIATH-DC). Kongamano hili lilifanyika jijini Arusha mwezi Novemba 2024 na kuhudhuriwa na washiriki takriban 250 kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, Kenya, Zambia, Malawi, Sweden, Korea, Ethiopia, Ujerumani, Zimbabwe na Tanzania. Matokeo

ya Kongamano hilo ni pamoja na kuboresha mitalaa ya Chuo ili kuendana na mahitaji ya soko; kuongeza nafasi za mafunzo kwa vitendo, na kusaidia maamuzi ya msingi katika sekta kutokana na tafiti mbalimbali zilizowasilishwa. Aidha, kongamano hilo limeimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa, kuchochea ubunifu, kuboresha huduma, na kuhimiza maendeleo jumuishi kupitia utalii unaojumuisha jamii na unaozingatia mazingira.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha watumishi wanakuwa na ujuzi stahiki, Chuo kimeendelea na utekelezaji wa Mpango wa mafunzo kwa kuwezesha watumishi 42 kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi ambapo watumishi 12 wanapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Uzamili na wanne (4) Uzamivu. Aidha, watumishi 26 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi katika fani za Utalii, Ukarimu na mbinu za ufundishaji.

### 4.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi, utafiti na uendelezaji wa rasilimali za malikale. Utekelezaji wa jukumu hilo unazingatia Sera ya Malikale ya Mwaka 2008, Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa, Sura ya 281. Sekta hii inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale, Shirika la Makumbusho ya Taifa la Tanzania na Mfuko wa Mambo ya Kale.

#### 4.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi, kuboresha mazingira ya kibiashara na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Mambo ya Kale, Wizara imefanya marekebisho ya

Kanuni za Tozo ya Usimamizi na Uendelezaji Malikale kwa Tangazo la Serikali Na. 873 la tarehe 25 Oktoba, 2024, imekamilisha Rasimu za Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura ya 333, rasimu tatu za miongozo ya usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya malikale ambazo ni: Mwongozo wa Uandaaji wa Mipango ya Usimamizi na Uendelezaji wa Maeneo ya Malikale, Mwongozo wa Utafiti wa Malikale. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kutwaa na Kubadilisha Umiliki wa Malikale. Sambamba na hatua hizo, Wizara imekamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Malikale ya Mwaka 2008 na imeandaa rasimu mbili za Mipango Jumuishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa eneo la Urithi wa Dunia, Kilwa Kisiwani na Songo Mnara pamoja na Mji wa Kihistoria Bagamoyo.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutekeleza Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale na Masalia ya Binadamu yaliyochukuliwa wakati wa Ukoloni, Wizara imeshiriki katika ziara ya Kamati ya Kitaifa ya Majadiliano kuhusu malikale na masalia ya binadamu iliyopo nchini Ujerumani ambapo Kamati hiyo imetembelea taasisi nne (4) za Ujerumani zinazohifadhi mikusanyo ya Tanzania. Lengo la ziara hiyo lilikua ni kuona na kufanya tathmini ya hali halisi ya malikale za Tanzania zilizopo nchini Ujerumani. Taasisi zilizotembelewa ni Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Fraas (Stuttgart); Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Berlin; Makumbusho ya ethnolojia ya Linden Stuttgart; Makumbusho ya Rothenbaum (Hamburg) na Taasisi za *Humboldt Forum na Prussian Cultural Heritage Foundation na* afya ya Charrite. Tathmini hiyo ilibaini kwamba mikusanyo ya Tanzania iliyopo katika taasisi hizo inajumuisha mabaki ya miili ya binadamu, paleontolojia (visukukuu vya wanyama na mimea), akiolojia na vifaa vya mila na utamaduni. Taarifa zilizizopatikana kutokana na ziara hiyo, zitatumika katika kuimarisha majadiliano baina ya Serikali za Shirikisho la Ujerumani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu

namna ya kurejesha au kunufaika na malikale zilizopo nchini Ujerumani.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maeneo ya malikale yanalindwa kisheria, kuendelezwa na kutumika kiutalii, Wizara imekusanya taarifa za kiuhifadhi za maeneo 163 katika mikoa 10 kwa lengo la kuyatangaza katika Gazeti la Serikali kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo ambayo taarifa zake zimekusanywa ni katika mikoa ya Ruvuma (8), Iringa (3), Lindi (54), Tanga (44), Singida (13), Morogoro (7), Manyara (2), Kagera (5), Mwanza (10), Mbeya (1), Tabora (2) na Pwani (14).

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya maeneo 163 ambayo taarifa zake zimekusanywa, taratibu za kisheria zinazohusu maeneo 16 yaliyopo katika mikoa ya Morogoro maeneo (2), Lindi (1), Ruvuma (2), Tanga (3), Mbeya (1), Singida (4), Tabora (2) na Iringa (1) zimekamilika kwa ajili ya kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa. Maeneo hayo ni pamoja na kambi zilizotumiwa na wapigania uhuru wa nchi ya Afrika ya Kusini na Msumbiji zilizopo Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kampasi ya Solomon Mahlangu-Mazimbu – Morogoro, Kihesa Mgagao – Iringa na Shule ya Sekondari ya Samora Machel - Mbeya; Makazi ya Watemi Fundikira na Isike – Tabora; Jengo la Kihistoria la Hospitali ya Afya ya Akili na Kanisa la KKKT Lutindi, Korogwe na Jengo la Kanisa na kituo cha Hija Magila Msalabani, wilayani Muheza - Tanga; na eneo la Mnara wa Kumbukumbu ya Hayati Edward Moringe Sokoine, Mvomero-Mkoani Morogoro.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine, imefanya tathmini ya hali ya uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo 18 ya malikale yaliyopo kwenye Orodha ya Urithi wa Taifa katika mikoa ya Dodoma (12), Singida (2) na Lindi (4). Maeneo

yaliyofanyiwa tathmini yanajumuisha michoro ya miambani, miji na majengo ya kihistoria na maeneo ya palentolojia ambayo yamebeba ushahidi wa chimbuko na maendeleo ya binadamu katika ardhi ya Tanzania. Lengo la tathmini hiyo ni kuhuisha orodha ya maeneo ya Urithi wa Taifa, kuandaa mipango ya kuendeleza yaliyo katika hali mbaya na kuyakabidhi kwa wadau wenye uwezo na nia ya kuyatumia kwa maendeleo endelevu. Tathmini hiyo imebaini kwamba maeneo hayo, yapo katika hali nzuri ya kiuhifadhi isipokua manne (4) hayajaanza kutumika kiutalii. Katika kuhakikisha kuwa maeneo hayo manne (4) yanatumika kwa faida za kijamii na kiuchumi, Wizara imeyakabidhi kwa wadau ambao wameonesha nia ya kuyatumia kwa maendeleo endelevu. Wadau hao ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa maeneo (2) na Kanisa la Anglican Kilimatinde, wilayani Manyoni (2). Aidha, maeneo 14 yaliyobaki yanaendelezwa na Wizara ya Maliasili na Utalii.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutatua migogoro ya mipaka kuhusu umiliki na uendeshaji wa maeneo ya malikale, migororo miwili (2) imefanyiwa kazi ambapo mgogoro wa kwanza unaohusu Kijiji cha Engaruka ulikuwa ni utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta. Kwa sasa, Wizara na uongozi wa Kijiji cha Engaruka, mkoani Arusha wanaendelea na vikao kupata namna bora ya kupunguza eneo la kihistoria la Engaruka kwa ajili ya kuwapatia wananchi bila kuathiri uhifadhi. Katika mgogoro wa pili unaohusu Familia ya Mtwa Mkwawa, makubaliano yamefanyika kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Usimamizi wa eneo la Makumbusho ya Mtwa Mkwawa, Iringa ambao utabainisha wajibu na haki za wadau wa eneo hilo.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na kusimamia matamasha manne (4) ya Kumbukumbu kwa lengo la kurithisha historia ya Taifa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine

na kuhimiza matumizi endelevu ya malikale. Matamasha hayo ni Kumbukizi ya Vita ya Majimaji, Nandete – Lindi na Songea – Ruvuma; na Maadhimisho ya Kumbukizi ya Miaka 103 Mwl. Nyerere yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2024 Butiama – Mara na Aprili, 2025 jijini Dodoma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa miaka kumi wa Kuenzi na Kutangaza Urithi wa Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akitazama onesho la Historia ya Vita vya Majimaji, katika Makumbusho ya Majimaji, Songea Mkoa wa Ruvuma.*

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa kwenye uhifadhi wa maeneo yanye sifa za kipekee, Wizara ilishiriki Mkutano uliofanyika Paris, Ufaransa Desemba 2024 ambao ulijadili hifadhi za jiolojia za UNESCO (UNESCO Global Georpark) ikiwemo Eneo la Jiolojia la Ngorongoro Lengai. Kupitia mkutano huo, Eneo la Jiolojia Hifadhi ya Ngorongoro Lengai lilirejeshewa hadhi yake iliyokuwa imepotea tangu mwaka 2022. Urejeshwaji huo umetokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa ikiwemo kuzingatia vigezo vilivyowekwa na UNESCO kwa kuimarisha uhifadhi, kuboresha miundombinu, kukusanya taarifa, kulitangaza pamoja na kushirikisha jamii katika matumizi endelevu ya eneo hilo. Vilevile, Wizara

imeshiriki mkutano wa tisa (9) wa wataalam wa fani ya akiolojia na paleontolojia uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Agosti, 2024 ambapo wataalam walijengewa uwezo katika fani za uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya paleontolojia na akiolojia.

### 4.3.4.2 Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mambo ya Kale – NFA ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale, Sura ya 333 kwa lengo la kuwezesha majukumu ya uhifadhi na utafiti wa malikale. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mfuko umewezesha utekelezaji wa Mpango wa Urejeshwaji wa Malikale na Masalia ya Miili ya Binadamu iliyochukuliwa wakati wa Ukoloni, uandaaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maeneo 2 ya Malikale ya Mji wa Kihistoria wa Bagamoyo na Magofu ya Kaole; na kutambua maeneo 16 ya malikale ili yaweze kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa. Aidha, Mfuko umewezesha uratibu wa shughuli za uhifadhi wa malikale katika maeneo 18 nchini; kufanya vikao 2 vya wadau kujadili uhifadhi na ufukuaji wa Nyayo za Laetoli; na kuandaa Kanuni za Utafiti wa Malikale na Uanzishwaji wa Makumbusho Binafsi. Vilevile, Mfuko umewezesha utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere.

### 4.3.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa – NMT

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Makumbusho ya Taifa lina jukumu la kukusanya, kuhifadhi, kutafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu mikusanyo ya kisayansi na kiutamaduni yenye hadhi ya urithi wa Taifa. Vilevile, Shirika linasimamia na kuendeleza vituo saba (7) vya Makumbusho ya Taifa na maeneo 107 ya Malikale yaliyopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuimarisha uhifadhi wa malikale na makumbusho kwa kujenga nyumba za asili saba (7) kwa mfumo wa Kaya zinazojumuisha jamii za Waha (2), Wabembe (3) na jamii ya Wamasai (2) katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Aidha, ukarabati wa nyumba za asili 13 uliohusisha Kaya za Wangoni, Wazaramo, Wamakua, Wagogo, Jamii za Makete na Wabena umefanyika katika vituo vya Makumbusho ya Majimaji, Songea (2) na Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam (11). Vilevile, ukarabati wa majenzi ya kale tisa (9) umefanyika katika eneo la Lindi mjini (1), Mbuamaji (1), Majimaji (4), Mikindani (2) na Makumbusho ya Mwl. Nyerere, Butiama (1).

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kulinda na kuhifadhi urithi wa malikale, Shirika limeongeza mikusanyo mipya 1,146 inayohusisha mila, historia na biolojia na kufanya idadi ya mikusanyo iliyopo Makumbusho ya Taifa kufikia 483,937. Kati ya mikusanyo hiyo, 15 ya mila imetolewa kwa hiari na wananchi wakati wa Tamasha la Utamaduni lililofanyika mwezi Septemba, 2024 Mkoani Ruvuma; 33 ni historia ya Mwami Theresa Ntare; 11 ni fedha za kale; 1,000 ni Masalia ya Mnyama aina ya Pomboo (Dolphine); 87 ni mikusanyo ya mila iliyotolewa kutoka kwa jamii za Waha na Wabembe kutoka Mkoani Kigoma na Jamii ya Wanyakyusa kutoka Mkoani Mbeya.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeimarisha miundombinu ya uhifadhi na utangazaji wa utalii wa malikale kwa kuweka vibao elekezi vitano (5) katika maeneo ya Mtwara-Mikindani (3), Tendaguru (1), Azimio la Arusha (1) na kuanza taratibu za ujenzi wa kituo cha taarifa pamoja na ukarabati wa Mnara wa Mashujaa wa Vita ya Majimaji Nandete wilayani Kilwa.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeboresha uhifadhi na ukusanyaji wa taarifa za mikusanyo kwa kuendelea kutumia mfumo wa teknolojia ya kidijitali ujulikanao kama *Digital Record*

*Archive and Management System – DRAMPS*. Mfumo huu umefanikisha usajili wa jumla ya mikusanyo 1,840, hivyo kufikisha jumla ya mikusanyo 10,115 iliyosajiliwa. Kwa upande mwingine, Shirika kwa kushirikiana na Taasisi ya CyArk ya nchini Marekani imeendesha warsha ya uchukuaji taarifa za Malikale kwa teknolojia ya kidijitali katika Hifadhi ya Urithi wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara. Hatua hiyo inalenga kutumia mifumo ya kidijitali katika kuhifadhi kumbukumbu za maeneo ya malikale nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa matumizi ya utafiti na utoaji wa elimu kwa umma.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeratibu na kufanya tafiti sita (6) za kimkakati zinazolenga kuimarisha maendeleo ya sekta ya malikale kwa kuongeza mikusanyo na kushirikisha wadau katika uhifadhi na uendelezaji malikale nchini. Vilevile, Shirika limetoa machapisho matano (5) na kusimamia ufanyikaji wa tafiti saba (7) katika masuala ya paleontolojia, akiolojia na michoro ya miambani zilizofanyika katika maeneo ya Olduvai Gorge, Ziwa Natron na Makuyuni-Arusha, Luxmanda-Manyara, Hifadhi ya Taifa Saadani-Pangani, Ismila-Iringa na Siuyu-Singida. Pia, miradi kazi (school projects) 291 imefanyika kwa wanafunzi wa shule za sekondari 109 katika mikoa ya Dar es Salaam (187), Arusha (85), Ruvuma (11) na Mara (8). Matokeo ya kazi na tafiti hizo, yamesaidia kuimarisha maendeleo ya sekta kwa kuongeza mikusanyo; kuongeza ujuzi kwa wataalam na kuboresha programu za ushirikishaji wadau.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine Shirika limeweka Onesho Jipya la kudumu la ndege ya kwanza ya Serikali aina ya Jet, Fokker-28-5H-CCM iliyotumiwa na Marais wa nchi kwa Awamu Tano kuanzia mwaka 1978 hadi 2018. Onesho hilo limebeba historia ya namna usafiri wa anga ulivyokuwa na mchango kwa viongozi wakuu wa nchi katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika na shughuli mbalimbali

za kujenga Taifa. Sambamba na hilo, Shirika limekusanya taarifa na kuandaa maudhui ya Onesho la kudumu la Dinasoria ambalo litawekwa katika Kituo cha Taarifa Tendaguru kwa lengo la kujenga uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa urithi wa asili, uendelezaji wa malikale, kujenga uzalendo na kutambua fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya malikale.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea kuhamasisha umma wa watanzania kuhifadhi historia zao na kuzirithisha kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limetoa ushauri kwa Taasisi (4) na jamii (4) kuanzisha na kuendesha makumbusho binafsi. Taasisi hizo zinajumuisha: Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu uanzishwaji wa makavazi ya Muungano; Mamlaka ya Bandari kuhusu kuanzisha Makumbusho ya Historia ya Usafiri wa Majini; *Ujiji Heritage Development Organization-UHDO* inayotarajia kuanzisha makumbusho ya mji wa kihistoria wa Ujiji- Kigoma; na *Nangwanda Sijaona Foundation* ya Newala Mkoani Mtwara inayotarajia kuanzisha makumbusho itakayohifadhi historia ya Ndugu Lawi Nangwanda Sijaona ambaye ni miongoni mwa Wapigania Uhuru wa Tanganyika. Vile vile, ushauri umetolewa kwa jamii (4) ambazo ni Wamatumbi kutoka wilayani Kilwa kuhusu uhifadhi wa historia ya Vita ya Majimaji; Jamii za watu wa Njombe na Nachingwea kuendeleza uhifadhi kupitia makumbusho za utamaduni; na Familia ya Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa katika kuhifadhi, kuendeleza na kutangaza historia ya kiongozi huyo.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Taasisi moja (1) na wamiliki wawili (2) wameanzisha makumbusho binafsi. Taasisi hiyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichoanzisha makumbusho ya historia ya Chuo hicho, na watu binafsi wawili (2) wameanzisha makumbusho za: Jiolojia iliyopo Bagamoyo,

Pwani na Makumbusho ya Kata ya Kanyigo iliyopo Misenyi, Kagera. Vilevile, wadau wawili (2) wamekarabati majengo ya kale na kuhuisha matumizi yake. Wadau hao ni Taasisi ya *Islamic Club* ya Kigamboni - Dar es Salaam ambayo imekarabati Msikiti wa Kale wa Mbuamaji na Bwana Vasantsinh Champs amekarabati jengo la kale moja (1) katika Mji wa kihistoria Bagamoyo na kulitumia kwa ajili ya huduma za malazi.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendesha matamasha na matukio makuu matatu (3) ya kuhamasisha uhifadhi na utalii wa malikale ambayo ni Tamasha la Waha na Wanyakyusa yaliyofanyika Kijiji cha Makumbusho-Dar es Salaam, Tamasha la Kumbukumbu ya Vita vya Majimaji-Nandete (Lindi) na Songea (Ruvuma). Aidha, programu 11 za kimakumbusho zimefanyika ikiwemo programu ya *Museum Art Explotion,* programu kwa wanafunzi wa vyuo vikuu (Museum Hub), na programu ya simulizi za kimakumbusho *Museum Talk* zinazorushwa kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari. Vilevile, vipindi 74 vya kutangaza huduma na mazao ya utalii wa malikale vimerushwa kupitia vipindi vya Radio (24), Televisheni (16) na Makala (34) katika mitandao ya kijamii. Pia, programu 40 za uhamasishaji zimefanyika katika shule za sekondari zilizopo mkoa wa Dar es Salaam (17), Arusha (5), Ruvuma (12), Mara (4) na Mtwara (2). Kupitia matamasha, programu na matukio hayo, jamii imepata elimu kuhusu uhifadhi, matumizi endelevu ya malikale na kujenga uzalendo.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya Nchi kutembelea Makumbusho, Shirika limeandaa maonesho ya muda matano (5) ambayo ni Onesho la Kimataifa la Ushirikiano kati ya Tanzania na Italia; Fursa ya Soko la Utalii Bagamoyo, Mapishi ya Vyakula vya Asili, Siku ya Zinj Duniani na Mchango wa Wanawake katika Uhifadhi wa Utamaduni, Ukombozi na Maadili ya Taifa. Uandaaji na uwekaji wa maonesho hayo umefanikisha kuhamasisha utalii wa

malikale kimataifa; kujenga uzalendo kwa wananchi; kutambua manufaa yatokanayo na shughuli za uhifadhi wa Malikale Nchini pamoja na kuleta watalii takriban 7,400; Hivyo, kuwezesha idadi ya watalii waliotembelea vivutio vya makumbusho na malikale kuongezeka kutoka watalii 226,135 kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024 kufikia watalii 312,048 katika kipindi cha kufikia Aprili 2025.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji kazi, Shirika limewezesha watumishi 35 kuhudhuria mafunzo ndani na nje ya Nchi. Kati ya hao, watumishi 18 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 17 wanapata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuongeza ufanisi. Vilevile kufikia mwezi Aprili 2025, watumishi 19 wamepandishwa vyeo na watumishi watatu (3) wameajiriwa kwa masharti ya ajira ya kudumu na malipo ya pensheni.

### 4.3.5 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka

#### (i) Kuimarisha Utendaji wa Wizara (Utawala na Rasilimaliwatu)

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Nne. Aidha, Wizara imeendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kuwahimiza watumishi kutoa huduma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu, maadili ya utumishi wa Umma, uwajibikaji pamoja na utekelezaji wa majukumu wakizingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Sambamba na hilo, Wizara imetoa elimu kwa watumishi kuhusu rushwa na maadili ambapo jumla ya watumishi 1,347 wamepatiwa mafunzo.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa watumishi kulingana na mahitaji, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imeajiri watumishi 676 wa kada mbalimbali na inakamilisha taratibu za ajira za watumishi wapya 556. Aidha, Wizara imewawezesha watumishi 1,800 kupata mafunzo ambapo watumishi 425 kujiunga na mafunzo ya muda mrefu, watumishi 1,375 kupata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 872 kupata mafunzo ya jeshi la uhifadhi. Mafunzo hayo yamekusudiwa kuwajengea uwezo watumishi kumudu majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kupata sifa za kimuundo ili kuwawezesha kupata sifa za kupanda vyeo pamoja na kuwaandaa watumishi wanaotarajia kustaafu kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kumudu maisha baada ya kustaafu. Vilevile, watumishi wa kada mbalimbali 737 wamepandishwa vyeo.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika mapambano dhidi ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) kwa kuwahudumia watumishi waathirika waliojiweka wazi kwa kuwapa posho maalum kwa ajili ya lishe bora na kuwahudumia watumishi wenye ulemavu. Pia, Wizara inaendelea kutoa vifaa kinga kwa watumishi wa Wizara na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kutunza afya zao kupitia vipeperushi na vikao rasmi vya Wizara.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kutoa stahili za watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo. Aidha, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kufanya mazoezi mahala pa kazi, Wizara imeendelea kutekeleza mwongozo huo unaolenga kuimarisha afya za watumishi kwa kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo michezo ya SHIMIWI iliyofanyika Mkoani Morogoro Oktoba, 2024; SHIMMUTA iliyofanyika Mkoani Tanga Novemba, 2024 pamoja na Bunge Marathon 2025. Vilevile, Wizara ilishiriki katika michezo ya maadhimisho ya Mei Mosi iliyofanyika Kitaifa

Aprili, 2025 mkoani Singida. Katika mashindano hayo Wizara ilifanikiwa kutwaa makombe mawili (2) na medali 36 baada ya kuzigaragaza bila huruma timu za Wizara zingine. Ushiriki wa Michezo hiyo umekuwa chachu ya kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi ya viungo, kuimarisha afya na kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukiza.

### (ii) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilishiriki Mkutano wa 31 wa World Travel Awards Portugal uliofanyika mwezi Novemba 2024 na kufanikiwa kupata fursa ya kuwa mwenyeji wa tukio la utoaji wa Tuzo za Kimataifa za Utalii zinazotolewa na Taasisi ya Kimataifa ya *World Travel Awards* kwa mwaka 2025 Kanda ya Afrika na *Ocenic*. Katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki Mkutano wa 46 wa Kamati ya Urithi wa Dunia, New Delhi-India uliofanyika Julai 2024 ambapo masuala mbalimbali yanayohusu uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia yalijadiliwa na kuonekana kwamba maeneo ya Urithi wa Dunia ya Tanzania yana hali nzuri ya kiuhifadhi. Vilevile, Wizara ilishiriki Mkutano wa 122 wa Baraza Tendaji la Shirika la Utalii Duniani uliofanyika nchini Colombia Novemba, 2024.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa kwenye masuala ya uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii, Wizara imeshiriki mikutano mbalimbali ya kikanda na kimataifa ikiwemo SADC, EAC, IORA, UNESCO, CITES, UNFCCC, UNPFII, COP-29 na Mkutano wa tisa (9) wa wataalam wa fani ya akiolojia na paleontolojia uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mwezi Agosti, 2024. Ushiriki katika matukio hayo huchochea ongezeko la idadi ya watalii, kujenga uwezo kwa watumishi, kuitambulisha Tanzania katika medani ya utalii wa kimataifa, kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kwa muktadha wa kukuza Sekta ya Utalii, Malikale na Maliasili pamoja na ongezeko la mapato kwa ujumla.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Wizara imeendelea kutekeleza mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa mazingira, maliasili, malikale na utalii. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya TabiaNchi (UNFCCC); Mkataba wa UNESCO unaohusu Uhifadhi na Ulinzi wa Maeneo ya Urithi wa Dunia ya Asili na Utamaduni; Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES); Mkataba wa Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ukame (UNCCD); Mkataba wa Wanyamapori Wahamao (CMS); na Mkataba wa Uhifadhi wa Bioanuai (CBD). Kwa kutekeleza mikataba hiyo, Tanzania imeendelea kushirikiana na Nchi nyingine duniani katika uhifadhi wa maliasili, malikale na ulinzi wa urithi wa Dunia.

### 4.4 Miradi ya Maendeleo

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilitengewa **Shilingi 176,392,513,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 97,225,838,000.00** fedha za ndani; na **Shilingi 79,166,675,000.00** fedha za nje. Aidha, fedha za Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 52,753,101,479.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali chini ya Wizara na **Shilingi 123,639,411,521.00** za Miradi inayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA, NCT, TTB, NMT, TAWIRI, TAFORI, PWTI, FTI, FITI na BTI). Hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 103,897,210,974.29** sawa na **asilimia 58.9** ya fedha zilizoidhinishwa kwa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,997,221,261.09** ni fedha za ndani na **Shilingi 52,899,989,713.20** ni fedha za nje. Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

## A. Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 jumla ya **Shilingi 1,501,044,606.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 1,501,000,000.00** zimetolewa ambazo ni sawa na asilimia 99.9 ya fedha zilizoidhinishwa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuhuisha teknolojia zilizotumika kutengeneza moduli mbalimbali za Mfumo wa *MNRT Portal;* kuongeza moduli mpya pamoja na kufungamanisha mfumo wa *MNRT Portal* na mifumo ya taasisi nyingine; kufanya manunuzi ya vifaa vya TEHAMA; Hadi sasa Wizara imefanikiwa kununua *Storage* mpya kwa ajili ya *Data centre* na *DR site* kwa gharama ya Shilingi 450,000,000.00; kuwezesha mafunzo ya muda mfupi kwa maafisa sita (6) nchini India na Afrika Kusini kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa uendeshaji na usimamizi wa mifumo pamoja na usimamizi wa usalama wa mifumo (cyber security); na Kuwezesha kukamilisha nyaraka mbalimbali za ujenzi wa mfumo wa Kupanga madaraja huduma za malazi (ASERT), ikijumuisha kutoa mafunzo ya mfumo huo wa *ASERT* pamoja na kufanya majaribio ya ukubali wa mfumo (User Acceptance Test – UAT).

## B. Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Hifadhi za Taifa Nyerere, Mikumi, Ruaha, Udzungwa

na katika Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Kilombero. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, mradi ulitengewa jumla ya **Shilingi 40,972,672,655.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi 92,672,655.00** zilikuwa fedha za ndani na **Shilingi 40,880,000,000.00** fedha za nje kutoka Benki ya Dunia (WB). Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 26,724,909,880.75** zimepokelewa na kutumika sawa na asilimia 65. Fedha hizo zilijumuisha **Shilingi 26,632,237,225.75** fedha za nje na **Shilingi 92,672,655.00** fedha za ndani. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: uboreshaji na ujenzi wa viwanja vya ndege vinne (4) katika Hifadhi za Taifa Mikumi (1), Nyerere (1) na Ruaha (2) ambapo ujenzi wake umefikia wastani wa asilimia 87.7. Maboresho hayo yamewezesha kuongezeka miruko ya ndege katika Hifadhi ya Taifa Mikumi kutoka miruko 1,719 mwaka 2022/2023 hadi 2,705 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 57.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi umekamilisha ujenzi wa majengo 41 ya utalii na watumishi katika hifadhi za Taifa Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Nyerere ikiwemo malango matatu (3) ya kuingia na kutoka hifadhini, nyumba 32 za kufikia watalii, hosteli moja (1), vituo viwili (2) vya kutolea taarifa za utalii. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa Kituo cha ufuatiliaji wa ikolojia ambapo ujenzi wa majengo katika Hifadhi za Taifa Nyerere na Ruaha umekamilika na katika Hifadhi ya Taifa Mikumi ujenzi umefikia asilimia 92. Pia, ujenzi wa njia ya juu ya utalii "canopy walkway" katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Udzungwa umefikia asilimia 70 na ujenzi wa kambi za kufikia wageni katika Hifadhi ya Msitu Asilia Kilombero umekamilika. Majengo ya utalii yataongeza uwezo wa huduma za malazi katika hifadhi za kipaumbele kwa kupokea watalii kutoka 100 kwa siku hadi watalii 453 pamoja na ongezeko la makazi kwa watumishi kutoka familia 18 hadi 72.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa kituo cha utafiti wa wanayamapori katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa umekamilika ambapo utasaidia kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na wanyamapori katika hifadhi za kusini mwa Tanzania. Aidha, ujenzi huu umegharimu jumla ya Shilingi 1,554,918,738.00 kati ya fedha hizo, Shilingi 1,536,707,285.21 zimelipwa sawa na asilimia 99. Ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha utalii katika eneo la Kihesa Kilolo – Iringa unaendelea ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 33 Ujenzi huu utagharimu jumla ya Shilingi 21,395,440,150.62 kati ya fedha hizo, Shilingi 4,494,082,089.04 sawa na asilimia 21 zimelipwa.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za mabonde madogo ya mito Chimala na Kimani na ujenzi unaendelea katika skimu za Mbuyuni-Kimani na Makangarawe zilizopo Wilaya ya Mbarali kwa kuboresha mfereji wenye urefu wa kilometa 1 na ujenzi wa skimu hizi umefikia asilimia 38.5; ujenzi wa ofisi 10 za Jumuiya za Watumia Maji (WUA) katika wilaya za Mbarali (Mwakaganga, Madibira, Mambi, Masage na Mswiswi), Makete (Matamba na Ikuwo), Wanging'ombe (Ihai na Mdadu) na Mufindi (Ikiwela) ambapo ujenzi umekamilika na utawezesha jumuiya hizo kusimamia matumizi ya maji.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuwezesha ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 1,050 kutoka vijiji 61 katika vyuo 50 vilivyopo nchini ambapo jumla ya Shilingi 7,715,169,120.00 zimetumika. Aidha, vijana 561 wamemaliza masomo na 16 kati yao wamepata ajira katika taasisi mbalimbali. Ufadhili wa masomo unawasaidia vijana kujiajiri au kuajiriwa katika utoaji wa huduma za utalii na kupunguza utegemezi katika rasilimali za hifadhi; na kuratibu upatikanaji wa vikundi vya awamu ya pili katika vijiji 46 kutoka wilaya 10 (Morogoro, Kilombero, Kilosa, Mvomero, Iringa, Kilolo, Chamwino, Mbarali, Rufiji na Kisarawe) ambapo jumla ya vikundi 397 vyenye jumla ya wanachama

7,701 (Me-2,612, Ke-5,089) vimekidhi vigezo kupata fedha mtaji ambapo jumla ya Shilingi 3,593,658,275 zimetolewa. Upatikanaji wa fedha mtaji kwa awamu ya kwanza na ya pili, umewezesha uwezo wa wanachama kupata mikopo kutoka Shilingi 2,466,425,360 hadi Shilingi 5,861,754,187 sawa na ongezeko la asilimia 58 na kumwezesha mwanakikundi mmoja mmoja kujikwamua kiuchumi ambapo baadhi yao wameanzisha biashara mpya, kuboresha makazi na kuanzisha miradi.

## C. Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania)

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira (Global Environmental Facility – GEF). Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 3,660,500,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali. Hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 2,632,475,000.00** zimetolewa ambayo ni sawa na asilimia **72** ya fedha iliyoidhinishwa. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa ruzuku Shilingi 337,500,000.00 kwa WMA (3) zinazoshiriki uhifadhi katika ikolojia ya Ruaha – Rungwa zikiwemo WMA za WAGA, UMEMARUWA na Chamwino na jumuiya za wafugaji nyuki za MUHESI na MWAKINTARU kwa ajili ya kuwezesha miradi ya kukuza kipato na kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu. Ruzuku hiyo imewezesha utengenezaji wa mizinga 2,190 ambapo Umemaruwa WMA imepata mizinga 250, WAGA Mizinga 300, Chamwino 135, jumuiya za wafugaji nyuki za MUHESI mizinga 880 na MWAKINTARU mizinga 740. Aidha, WMA ya WAGA imepatiwa vifaa vya kufugia nyuki na kuchakata mazao ya nyuki.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu pia umewezesha ununuzi wa pikipiki 20 kwa ajili ya kuwezesha shughuli za ulinzi kwa vikosi maalum vya kudhibiti ujangili katika kanda 10 za kiikolojia na WMA za WAGA, UMEMARUWA na MBOMIPA. Sambamba na hilo, mradi uwezesha kikao cha wadau wa uhifadhi na himasheria kujadili utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu kuzuia ujangili. Miongoni mwa masuala yaliyoazimiwa ni kuanzishwa kwa utaratibu shirikishi (Public – Private Partnership - PPP) utakaowezesha wadau kuchangia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili wa mwaka 2023 – 2033.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Mradi umewezesha mafunzo ya uchunguzi, utambuzi wa nyara, intelijensia na uendeshaji wa mashitaka kwa maafisa 56 kutoka Jeshi la Uhifadhi, Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili na Kanda za ki-ikolojia za kuratibu Doria. Sambamba na hilo mradi umewezesha mafunzo ya mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii kwenye mfumo Ikolojia wa Ruaha – Rungwa katika Wilaya ya Itigi, Manyoni, Iringa, Mufindi na Mbarali.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha ushirikiano katika uhifadhi wa ukanda wa Afrika Mashariki, mradi umewezesha mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kubadilishana taarifa za ujangili (EAC-TWIX) kwa maafisa 31 wa Idara ya Wanyamapori, TAWA, TANAPA, TFS na NCAA na kuwaunganisha na maafisa wengine kutoka Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na DRC ili kubadilishana taarifa kupitia mtandao huo. Mradi pia umewezesha mtandao wa ufuatiliaji wa kijamii katika mfumo ikolojia wa Ruaha - Rungwa kwa kuwapatia mafunzo, vifaa (simu) na namba mbili (2) maalum za simu za kupiga bure kupokelea taarifa. Mtandao huo umewezesha ukusanyaji wa taarifa za vitendo vya ujangili na

kufanyiwa kazi kabla madhara hayajajitokeza. Katika hatua nyingine mradi umewezesha mafunzo kuhusu uhifadhi na faida zake, utatuzi wa migongano baina ya binadamu na wanyamapori na uendeshaji wa doria kwa viongozi 127 wa WMA za WAGA, Chamwino na UMEMARUWA.

## D. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mradi wa kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki uliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 950,672,655.00** fedha za ndani. Hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 858,000,000.00** zimetolewa kwa ajili ya kulipa madeni ya TAFORI na kuboresha miundombinu ya kufundishia katika Chuo cha Mafunzo ya Misitu Olmotonyi (FTI) na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi (FITI).

## E. Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)

**195.** ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya. Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Singida, Tabora, Kigoma, Shinyanga na Katavi kwa upande wa Tanzania Bara na mkoa wa Pemba upande wa Zanzibar. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 1,371,141,150.00** kati ya **Shilingi 1,587,948,290.00** zilizoidhinishwa zimepokelewa na kutumika kwa shughuli zifuatazo: kuwezesha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 148 pamoja na ununuzi wa samani (vitanda, meza na viti) katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora. Hadi sasa, ujenzi wa bweni umefikia asilimia 68 na unatarajiwa

kukamilika mwezi Julai, 2025. Vilevile, mradi umewezeha ujenzi wa vituo sita (6) vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika halmashauri za wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo, na Mlele. Katika hatua nyingine, ujenzi wa kituo cha kufundishia (Manzuki darasa) kwenye Chuo cha Kilimo Zanzibar umekamilika.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande mwingine, Mradi umewezesha taratibu za uanzishwaji wa misitu ya vijiji 22 iliyotengwa kuwa Hifadhi za Nyuki katika mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma na Singida; na hifadhi za nyuki 7 kwa mikoa ya Pemba Kaskazini na Pemba Kusini. Aidha, katika maeneo hayo mradi umewezesha kuanzisha ukanda wa kufugia nyuki kwenye Pori la Akiba Moyowosi (Hekta 139,200); kuwezesha maandalizi ya Mpango wa Biashara wa Maabara ya Taifa ya Tafiti za Ufugaji Nyuki Njiro – Arusha; kuwezesha mapitio ya Sera ya Misitu ya Zanzibar kwa kujumuisha kipengele cha ufugaji nyuki; na kuwezesha mafunzo ya ufugaji nyuki kwa wakufunzi sita (6) kutoka Chuo cha Kilimo Zanzibar. Vilevile, mradi umeandaa mwongozo wa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa Chuo cha Kilimo Zanzibar; kuwezesha maandalizi na uzinduzi wa Alama ya Asali ya Tanzania (Honey Trademark); vikao sita (6) vya wafanyabiashara ya Mazao ya Nyuki na Serikali ili kutatua vikwazo vya kibiashara; na vikao 10 vya kujenga uwezo katika usimamizi na uendeshaji wa taasisi au Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi pia umewezesha mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa vijana na wanawake 973 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar na kutoa mizinga ya nyuki 2,200 kwa vikundi 40 vya wafugaji nyuki; kuwezesha mafunzo ya kushona mavazi kinga ya nyuki kwa mafundi 20 kutoka Pemba; kuwezesha mafunzo ya kujenga uwezo kwa

wafanyabiashara 35 kuhusu Kanuni mpya za biashara ya mazao ya nyuki kwenye masoko katika nchi za Umoja wa Ulaya; mafunzo ya kuimarisha ushirika kwa wajumbe 25 wa bodi kutoka TABEDO na PEBA; na kuwezesha wafanyabiashara 35 wa mazao ya nyuki kushiriki katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) Jijini Dar es Salaam.

## F. Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR)

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Mazingira Duniani "Global Environmental Facility – GEF". Mradi una lengo la kukuza usimamizi jumuishi wa rasilimali za ardhi, maji na misitu nchini, na unatekelezwa katika kongani ya Kilombero kwa upande wa Tanzania Bara na Kaskazini A na B kwa upande wa Zanzibar. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 2,474,900,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Hadi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 1,422,400,000** zimetolewa na kutumika kutekeleza kazi zifuatazo: Kufanya maboresho ya ofisi za mradi zilizopo Kilombero na Zanzibar kwa kununua vifaa vya ofisi na vitendea kazi vya mradi; kuwezesha vikao vya mradi kwa ajili ya kujadili na kupitisha mpango na bajeti ya utekelezaji wa shughuli za mradi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kikao cha wadau cha utekelezaji wa mpango huo; kukusanya taarifa za msingi za mradi kuhusu maeneo mahsusi ya ikolojia kwa ajili ya uhifadhi, mnyororo wa thamani wa zao la mpunga na kuandaa mpango wa uhifadhi wa ikolojia ya Kiashange-Mokotoni na Kinyasini Zanzibar. Vilevile,mradi umewezesha kazi ya utambuzi wa fursa za uwekezaji, na maeneo ya kuhifadhi, kuanzisha na kuimarisha jukwaa la pamoja la wadau watekelezaji mradi katika ikolojia ya Kilombero na Zanzibar.

## G. Mradi wa Ujenzi wa Makumbusho ya Marais - Dodoma

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo katika mwaka wa Fedha 2024/2025, jumla ya **Shilingi 1,000,000,000.00** ziliidhinishwa na kupokelewa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2025, kazi zilizotekelezwa ni kuajiri Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu, kuandaa michoro na makadirio ya gharama za ujenzi. Mtaalam huyo, amekabidhiwa eneo la mradi mwezi Machi, 2025 na anaendelea na kazi ambayo itakamilika mwezi Julai, 2025. Aidha, taratibu za ununuzi wa vitendea kazi likiwemo gari la mradi zinaendelea.

## H. Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za ndani. Mwaka wa fedha 2024/2025, **Shilingi 2,757,658,485.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mafunzo. Hadi Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 1,240,171,685.59** zimepokelewa na kutumika katika ujenzi wa jengo la taaluma lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 katika Kampasi ya Arusha ambapo ujenzi umefikia asilimia 65 pamoja na kufanya ukarabati wa jengo la taaluma katika Kampasi ya Bustani kwa kutumia fedha kutoka vyanzo vya mapato ya ndani (Own source) kiasi cha **shilingi 88,049,700.00** ukarabati huu umefikia asilimia 30.

## I. Miradi ya TANAPA

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/2025 (Julai 2024 – Aprili 2025) Shirika limeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kwa kutumia fedha za nje

ambapo miradi iliyotekelezwa ni pamoja na Mradi wa Msaada wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Tanzania; Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti awamu ya kwanza na ya Pili pamoja na Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya Hifadhi za Taifa za Katavi, Mahale, na Ushoroba wa Uunganishi. Miradi hii yote inafadhiliwa na Serikali ya Ujerumani kupitia benki ya maendeleo ya KfW ambapo jumla ya **Shillingi 16,475,916,669.99** zilitumika kati ya **Shilingi 18,633,325,000.00** zilizotengwa.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi wa Msaada wa Dharura wa Urejeshaji wa Bioanuai Nchini Tanzania (ERB) shughuli zilizotekelezwa ni ununuzi wa malori 5 (Serengeti - 2 na Nyerere – 3), mitambo 5 ya kutengeneza barabara Hifadhi ya Taifa Serengeti (grader 2, compactor 1, excavator 1 na back hoe loader 1), kulipia gharama za doria za askari za magari na ndege zikiwemo posho, sare, mafuta ya magari, matengenezo ya magari 79 (Serengeti 51 na Nyerere 28), uwekaji wa mifumo mipya ya nishati ya jua katika vituo 12 vya askari hifadhi ya Serengeti, kufanya utafiti wa maji katika vituo 2 vya askari pamoja na kukarabati visima vinne (4) vya mafuta katika hifadhi ya Taifa Nyerere. Vilevile mradi umejenga karakana moja ya magari Arusha, umetoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi 5,621 pamoja na kuendeleza vikundi vya kukuza uchumi katika Wilaya za Busega, Meatu na Itilima. Aidha, Mradi umefanikisha uandaaji wa mpango wa usimamizi mioto (FMP) katika hifadhi ya Taifa Nyerere.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia wa Serengeti (SEDCP I) - Awamu ya Kwanza umetekeleza miradi ya matengenezo ya barabara za mchepuko (rehabilitation of feeder roads) zenye urefu wa kilomita 73.52 (Wilaya ya Serengeti kilometa 27.82 na box culvert 5, Wilaya ya Ngorongoro kilometa 46.7), ujenzi wa kituo cha kutolea taarifa katika eneo la Seronera na miradi ya kijamii

18 pamoja na mabwawa 8 katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Vilevile, Mradi wa Maendeleo na Uhifadhi wa Mfumo wa Ikolojia ya Serengeti (SEDCP II) Awamu ya Pili umewezesha tafiti za topografia na haidrojia kwa ujenzi wa daraja la Kogatende, ukarabati wa jengo la Fort Ikoma, visima vya uvunaji maji. Aidha, mradi umewezesha ukamilishaji wa mipango ya matumizi bora ya Ardhi kwenye vijiji 18 na kutoa mafunzo ya COCOBA kwa vikundi 36 vyenye wanachama 659 katika Wilaya za Bariadi, Tarime na Bunda kupitia hifadhi ya Taifa Serengeti.

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Uhifadhi wa Ikolojia ya Hifadhi za Taifa Katavi, Mahale, na Ushoroba unaounganisha hifadhi hizi mbili (KAMACO) umefanikisha kazi ya kuwekwa kwa vigingi 45 na mabango 15 katika Hifadhi ya Msitu ya Kijiji cha Lufubu, Wilaya ya Uvinza na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 18 (10 vya Wilaya ya Tanganyika na 8 vya Wilaya ya Uvinza); marejeo ya Mpango wa Usimamizi wa Misitu kwa kushirikisha jamii katika vijiji vitatu: Kafisha, Kaparamsenga, na Songambele; uondoaji wa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 159; na kuzoesha na kufuatilia sokwe 63 katika Hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale. Aidha, mradi umekabidhi mashine aina ya excavator, mahema, simu za mkononi katika hifadhi ya Taifa Katavi; na lori la tani saba (7) na injini za boti tatu (3) katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale.

## J. Miradi ya TAWA

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ilidhinishiwa kutumia kiasi cha **Shilingi 22,004,578,381.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha **Shilingi 11,479,826,671.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,524,751,710.00** fedha za nje. Hadi Kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 3,881,872,668.45** zimepokelewa ambapo **Shilingi 2,960,569,668.45** ni fedha

za nje na **Shilingi 921,303,000.00** ni fedha za ndani. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: Kufanya ukarabati wa kilometa 393 za barabara na viwanja vidogo viwili (2) vya ndege katika Pori la Akiba Selous; Kununua na kufunga injini mpya ya ndege (5H SGR); na kununua magari matano (5) ya doria.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa katika Shule ya Ngumbu-Liwale, Shule ya Sekondari Mwaseni-Rufiji na Shule ya Msingi Miguruwe; ujenzi wa ofisi, nyumba ya wageni umefikia asilimia 46, bweni la watumishi ambao umefikia asilimia 76 na karakana ambao upo asilimia 41 katika Pori la Akiba Selous kanda ya Kingupira; ofisi katika Pori la Akiba Selous kanda ya Miguruwe ambao upo katika hatua ya kupiga plasta; Bweni la wasichana Shule ya Sekondari Mchengerwa ambao upo katika hatua ya kuezeka. Aidha, Miradi inayoendelea inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2025.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Sera na Sheria mbalimbali; Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge, maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kutangaza utalii ndani na nje ya nchi kupitia matangazo katika ligi kuu za michezo mashuhuri duniani, mashindano ya kimataifa, mashirika ya ndege; misafara ya utangazaji utalii; matamasha makubwa ya kimataifa na mitandao mbalimbali ya Kimataifa na Vyombo vya Habari;

(ii) Kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo maeneo ya malikale pamoja na utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli, michezo, tiba na utamaduni;

(iii) Kuboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi ikiwemo barabara, viwanja vya ndege na huduma za utalii;

(iv) Kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika usimamizi wa uhifadhi na rasilimali, ufuatiliaji, utangazaji na uendeshaji wa shughuli za utalii;

(v) Kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, misitu, nyuki na malikale;

(vi) Kuongeza uzalishaji na thamani ya mazao ya Misitu na Nyuki;

(vii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa takwimu mbalimbali, kufanya tafiti za kimkakati na kutoa huduma za ushauri zinazohusu masuala ya uhifadhi endelevu wa wanyamapori, misitu na nyuki, malikale na uendelezaji utalii;

(viii) Kuelimisha na kuhamasisha Jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, malikale, misitu na ufugaji nyuki;

(ix) Kuimarisha usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii na uhifadhi; na

(x) Kuandaa na kufanya Mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii.

### 5.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,183,584,115,330.55** kutoka kwenye Idara na Taasisi zake.

### 5.2 Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 359,982,271,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000.00** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 105,749,922,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Mishahara **Shilingi 130,709,054,000.00** na Matumizi Mengineyo **Shilingi 123,523,295,000.00.** Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 32,476,051,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** fedha za nje.

**211.** ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi 254,232,349,000.00** zinajumuisha **Shilingi 32,527,989,914.00** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 221,704,359,086.00** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 10,189,499,000.00** ni Mishahara na **Shilingi 22,338,490,914.00** ni Matumizi Mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 120,519,555,000.00** za Mishahara na **Shilingi 101,184,804,086.00** za Matumizi Mengineyo.

## 5.3 Kazi zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

### 5.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya Shilingi **48,312,790,524** zimetengwa kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa helikopta 2 kupitia taasisi za uhifadhi za TANAPA (1) na NCAA (1); uchimbaji wa mabwawa 12 katika Mapori ya Akiba ya Rungwa (2), Kizigo (2) Muhesi (2), Maswa (1), Selous-Kingupira (1), Wami-Mbiki (1), Msanjesi (1) na Hifadhi za Taifa za Katavi (1), na Mikumi (1); uchimbaji wa visima vya maji 18 katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro (1), Mikumi (6), Mkomazi (2), Tarangire (7), Mto Ugala (1) na Milima ya Udzungwa (1).

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara kupitia taasisi za TANAPA na NCAA itajenga uzio wa umeme wenye jumla ya urefu wa Kilometa 53 ambapo Kilometa 38 ni kutoka Tabora B hadi Mto Mara katika Hifadhi ya Taifa Serengeti na Kilometa 15 kutoka lango la Loduare kuelekea Oldiani katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, Wizara kupitia taasisi zake (TAWA, TANAPA na NCAA) itajenga vituo 19 vya askari kwenye maeneo yenye changamoto za wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya za Tunduru (2), Kiteto (1), Ikungi (1), Nkasi (1), Itilima (1), Manyoni (1), Kilosa (1), Rufiji (1), Babati (1), Morogoro (2), Karatu (1), Monduli (2) na hifadhi za taifa za Ibanda Kyerwa (1), Mto Ugala (1), Rumanyika Karagwe (2) na ujenzi wa vizimba 50 katika maeneo yenye changamoto ya mamba na viboko katika Halmashauri za Wilaya za Nkasi (3), Sengerema (3), Buchosa (3), Kibiti (3), Rufiji (3), Morogoro (3), Namtumbo (2), Nanyumbu (2), Uvinza (2), Geita (2), Kibaha (2), Mkuranga (2), Busega (2), Mvomero (2), Nyasa (2), Songwe (2), Iringa (3), Kilosa (1), Tarime (2), Kalambo (2), Mkinga (1), Nanyamba (1), na Ukerewe (2).

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na wadau itawajengea uwezo Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) 100 kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri za Wilaya 20. Vilevile, Wizara itafanya semina pamoja na kununua pikipiki 22 kwa ajili ya Maafisa Wanyamapori wa Wilaya 22 ili kuendelea kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao na kuwawezesha kufika kwenye maeneo ya matukio kwa wakati, mtawalia.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa jamii katika uhifadhi, Wizara itaendelea kuwezesha uanzishaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori nne (4) katika wilaya za Uvinza, Mkalama, Kilolo na Ikungi. Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo kwa WMA mpya na zilizopo kwa kuziwezesha vitendea kazi zikiwemo pikipiki 12 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori. Vilevile, Wizara itaendelea kuandaa miongozo mbalimbali kwa ajili ya kutatua changamoto za usimamizi wa WMA nchini.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutumia teknolojia katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kununua ndege nyuki (drones) 12 na mikanda maalum ya mawasiliano 50 (GPS Satellite Collars) kwa ajili ya ufuatiliaji wa mienendo ya wanyamapori hao. Mikanda hiyo itafungwa kwa tembo viongozi katika maeneo yenye changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Wizara itanunua na kusambaza mabomu baridi 40,000 katika maeneo yenye changamoto ya Tembo. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kufanya tafiti za kimkakati kwa ajili ya kugundua mbinu mpya za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka

2022 - 2026 kwa kuendelea kuelimisha jamii zilizopo kwenye maeneo ya shoroba za wanyamapori za: Ziwa Manyara, Kwakuchinja, Serengeti Complex – Yaeda Chini, Nyerere Selous – Niassa, Ruaha – Rungwa – Udzungwa, Ruaha – Rungwa – Katavi Complex, Kilombero – Milima ya Udzungwa, Nyerere Selous – Wami Mbiki, Serengeti Complex – Longido, na Udzungwa – Mikumi; pamoja na kuendelelea kufanya tathmini ya hali halisi ya maeneo hayo, kubainisha mipaka na kuweka mabango.

**218.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi watakaoathirika na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011 na marejeo yake ya mwaka 2024.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori, Wizara kupitia Taasisi zake za Uhifadhi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kupambana na Ujangili wa Mwaka 2023-2033; Mpango wa Usimamizi wa Tembo wa Mwaka 2023-2033; na Mpango wa Taifa wa Kuongoa Shoroba za Wanyamapori wa Mwaka 2022-2026. Utekelezaji wa mipango na mikakati hii itawezesha kudhibiti matukio ya ujangili na biashara haramu ya nyara nchini pamoja na kuimarisha uhifadhi. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283 na Kanuni zake kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori.

#### 5.3.1.2 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko utaendelea kuwezesha; utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu mbalimbali za kudhibiti wanyamapori

wakali na waharibifu; kulipa kifuta jasho na machozi kwa wananchi watakaoathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu; kuwezesha Kikosi kazi cha Taifa cha Kudhibiti Ujangili; utatuzi wa migogoro kati ya jamii na maeneo yaliyohifadhiwa; upandishaji hadhi maeneo yaliyohifadhiwa; na kujenga uwezo katika usimamizi wa rasilimali za wanyamapori. Katika hatua nyingine Mfuko utawezesha vyuo vya mafunzo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tafiti za kimkakati za wanyamapori.

#### 5.3.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania – TANAPA

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za ulinzi katika hifadhi za Taifa kwa kufanya doria 99,291. Aidha, Shirika litaweka alama kwa faru 45 ili kufuatilia mienendo yao katika Hifadhi za Taifa Serengeti (25) na Mkomazi (20) pamoja na kufunga mifumo ya redio katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro (1), Milima ya Udzungwa (1), Ruaha (1), na Saadani (1) kwa ajili ya mawasiliano. Vilevile, Shirika litajenga vituo vinne (4) vya askari katika hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Mto Ugalla (1) na Rumanyika-Karagwe (2) na kukarabati vituo vya askari vitano (5) katika Hifadhi za Taifa Katavi (1), Kitulo (1), Milima ya Mahale (1), Milima ya Udzungwa (1) na Tarangire (1) ili kuimarisha ulinzi na kukabiliana na matukio ya ujangili.

**222.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika litaendelea kuimarisha shughuli za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuhakikisha wanyamapori wanapata maji ya kutosha ndani ya hifadhi kwa kuchimba mabwawa (2) na visima virefu 18 na katika Hifadhi za Taifa (Kilimanjaro (1), Mikumi (7), Mkomazi (2), Tarangire (7), Mto Ugala (1), Katavi (1), na Milima ya Udzungwa (1). Sambamba na hilo, Shirika litaondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8,838.20 ili kuongeza nyanda za malisho kwa wanyama katika hifadhi za

Taifa Arusha (1,105.6), Mikumi (4,800), Mkomazi (200), Burigi-Chato (300), Gombe (10), Katavi (6), Nyerere (50), Serengeti (500), Saadani (372), Rumanyika-Karagwe (25), Kisiwa cha Rubondo (400), Ziwa Manyara (40), Milima ya Udzungwa (39.6), Ibanda-Kyerwa (800), Tarangire (100), Ruaha (15), Kitulo (5), Kisiwa cha Saanane (22) na Mto Ugalla (48). Aidha, Shirika litaboresha eneo la malisho ya wanyamapori lenye ukubwa wa hekta 900 katika hifadhi ya Ziwa Manyara.

**223.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye uhifadhi, Shirika litatekeleza miradi mbalimbali kwa jamii zinazopakana na hifadhi zote 21. Miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa mabweni saba (7) katika shule za Sekondari wilayani Namtumbo (1), Kyerwa (1), Serengeti (2), Moshi (1), Arumeru (1), na Tunduru (1) pamoja na hosteli ya wasichana wilaya ya Chunya; kuweka mifumo ya gesi ya kupikia katika shule sita (6) wilaya za Moshi (2), Hai (2) na Rombo (2); kujenga madarasa 24 wilayani Handeni (4), Busokelo (2), Monduli (2), Kilosa (2), Kyerwa (3), Serengeti (6), Lushoto (2) na Bariadi (3). Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha ujenzi wa nyumba 2 za walimu wilayani Simanjiro (1) na Babati Vijijini (1); kujenga matundu 30 ya vyoo katika shule za msingi Wilayani Busokelo (7), Simanjiro (7), Urambo (7) na Karatu (9) na kusambaza samani (viti na meza) 600 katika shule zilizopo katika Wilaya za Kaliua (200), Urambo (200), na Uvinza (200), pia ununuzi wa kompyuta 20 na kompyuta mpakato 24 katika shule ya sekondari Musati Wilaya ya Serengeti. Aidha, Shirika litawezesha miradi ya ufugaji nyuki kwa vikundi viwili wilayani Karatu kwa kugawa mizinga ya nyuki 200; Ujenzi wa mabwawa na Vizimba (3) kwa ajili ya ufugaji samaki Wilayani Mpanda (1), Chato (1) na Nyamagana (1). Vilevile, Shirika litawezesha ujenzi wa maabara katika zahanati mbili (2) Wilayani Karagwe (1) na Kigoma (1), jengo la wagonjwa wa nje (OPD) kituo cha afya Mwakijembe wilaya ya Mkinga; pamoja na ujenzi wa jengo la "infusion unit" hospitali

ya Mpanda. Sambamba na hilo, Shirika litawezesha ujenzi wa kituo cha polisi wilaya ya Iringa Vijijini pamoja na ujenzi wa ofisi ya kijiji wilaya ya Kilombero.

**224.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za utalii, Shirika litajenga "Picnic Sites" 4 katika Hifadhi za Taifa Ziwa Manyara (1), Kisiwa cha Rubondo (1) na Rumanyika-Karagwe (2); Cottages 18 katika Hifadhi za Taifa za Saadani (1), Arusha (1), Kilimanjaro (2), Ziwa Manyara (5), Katavi (2), Ibanda-Kyerwa (3), Milima ya Mahale (1) na Kisiwa cha Rubondo (3); majiko katika kambi za utalii na maeneo ya kulia chakula matano katika Hifadhi za Taifa za Mkomazi (1), Tarangire (1), Katavi (1), Kitulo (1) na Burigi-Chato (1); "Rest Houses" 3 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (2) na Ziwa Manyara (1) na vyoo vya wageni 15 katika Hifadhi za Taifa za Mikumi (2), Arusha (1), Kilimanjaro (5), Tarangire (4), Nyerere (1) na Ruaha (2). Shirika litajenga malango 6 ya kuingilia wageni katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Saadani (2), Mikumi (2) na Mto Ugalla (1).

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Shirika litaboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga barabara ya kilomita 6.69 ya tabaka gumu ili kuunganisha Hifadhi ya Tarangire na barabara ya lami eneo la Minjingu hadi lango kuu la Hifadhi. Sambamba na hilo, Shirika litafungua barabara mpya kuu na barabara za utalii zenye urefu wa kilomita 1,027.19 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 2), Burigi-Chato (km 50), Milima ya Mahale (km 22), Nyerere (km 150), Rumanyika-Karagwe (km 1), Serengeti (km 561), Tarangire (km 181.19), Milima ya Udzungwa (km 45) na Mto Ugalla (km 15). Sambamba na hilo, Shirika litafanya ukarabati mkubwa wa viwanja vya ndege 11 katika Hifadhi za Taifa Ibanda-Kyerwa (1), Serengeti (7), Katavi (1), Milima ya Mahale (1) pamoja na Kisiwa cha Rubondo (1); na kufanya ukarabati mdogo kwa viwanja 17 katika hifadhi za Nyerere (5), Kilimanjaro (5), Ugalla (2), Mikumi (1), Saadani (1), Serengeti (1) na Tarangire (1).

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Shirika litakarabati barabara za utalii na barabara kuu zenye urefu wa kilomita 2,596 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 104), Burigi-Chato (km 50), Ibanda-Kyerwa (km 90), Katavi (km 159.50), Kilimanjaro (km 286.80), Kitulo (km 25), Ziwa Manyara (km 341), Mkomazi (km 20), Nyerere (km 400), Ruaha (km 231), Kisiwa cha Rubondo (km 79), Saadani (km 16.5), Tarangire (km 220), Milima ya Udzungwa (km 93.8), Rumanyika-Karagwe (km 90), Mikumi (km 140) na Mto Ugalla (km 100). Vilevile, Shirika litakarabati njia za kutembea kwa miguu (trails) za kilomita 908.7 katika Hifadhi za Taifa za Arusha (km 32), Gombe (km 10), Kilimanjaro (km 629.20), Ziwa Manyara (km 4.8), Milima ya Mahale (km 105), Kisiwa cha Rubondo (km 21), Saadani (km 30), Tarangire (km 1.7), Kitulo (km 1) na Kisiwa cha Saanane (km 0.4).

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kutangaza fursa za uwekezaji ikiwemo malazi katika hifadhi kulingana na mpango wa ujumla wa hifadhi husika. Kadhalika, Shirika litaboresha na kuimarisha mazao ya utalii kwa kuendelea kuboresha mazao yaliyopo na kubuni mazao mapya ya utalii ikiwemo kuanzishwa kwa utalii wa majini ndani ya Ziwa Viktoria unaounganisha Hifadhi za Taifa Kisiwa cha Saanane, Kisiwa cha Rubondo na Serengeti ili kufungua aina mpya ya utalii kupitia eneo la Ghuba ya Speke. Aidha, Shirika litaendelea na ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa gofu pamoja na hoteli ya Chato ili kuanza kutumika na kuongeza idadi ya wageni pamoja na mapato kwa ujumla. Vilevile, Shirika limetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa Samani na vifaa katika majengo yaliyojengwa na ufadhili wa mradi wa REGROW katika Hifadhi za Taifa Ruaha, Nyerere, Mikumi, na Milima ya Udzungwa ili majengo hayo yaliyokamilika yaweze kutumika na kufikia malengo tarajiwa.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Shirika linaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato pamoja na kuboresha huduma kwa wageni, jumla ya "smart gates" 15 katika hifadhi za Serengeti (8), Manyara (1), Arusha (2), Mkomazi (2), Mikumi (1) na Tarangire (1) zitawekwa.

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, Shirika litajenga nyumba 3 za watumishi, na kukarabati nyumba 133 katika hifadhi za Ibanda-Kyerwa (1), Milima ya Mahale (36), Mkomazi (1), Nyerere (61), Ruaha (5), Rumanyika-Karagwe (1), Serengeti (1), Tarangire (2), Milima ya Udzungwa (7), Kitulo (2), TANAPA Makao Makuu (16), Southern Zone (1) na Mto Ugala (2). Aidha, Shirika litajenga ofisi 3 katika Kanda za Magharibi (1), Kaskazini (1), na Mashariki (1). Vilevile, Shirika litawezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi (6) na mafunzo ya muda mfupi ya nyanja mbalimbali kwa watumishi (1,500) ikiwa ni pamoja na kuwezesha watumishi kushiriki michezo katika ngazi zote. Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha upatikanaji wa vifaa vya utendaji kazi ikiwemo ununuzi wa magari 28, magari ya zimamoto 4 kwajili ya viwanja vya ndege vya Hifadhi za Taifa Mikumi (1), Nyerere (1) na Ruaha (4), ili kuongeza ufanisi.

### 5.3.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania–TAWA

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za wanyamapori nje ya maeneo ya Hifadhi za Taifa na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka itaendelea kudhibiti ujangili na biashara haramu ya nyara kwa kuimarisha doria ambapo jumla ya doria 18,920 zitafanyika. Aidha, Mamlaka itajenga vituo vitatu (3) vya askari katika mapori ya akiba ya Moyowosi, Luganzo na Pori Tengefu Ziwa Natron. Sambamba na hilo, Mamlaka itanunua injini 10 za boti, pikipiki

16, boti (1) na trekta (1) kwa ajili ya kuimarisha doria katika maeneo ya nchi kavu, maeneo yenye maziwa, mito na ardhioevu. Vilevile, Mamlaka itanunua ndege nyuki (drones) sita (6) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na mwitikio wa haraka kudhibiti na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu.

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha miundombinu ya uhifadhi na utalii, Mamlaka itajenga kilomita 197 za barabara katika Mapori ya Akiba Wami-Mbiki (150), Mpanga Kipengere (30), Rukwa (17) na kufanya ukarabati wa kilomita 220 za barabara katika Mapori ya Akiba Kizigo (120) na Muhesi (100). Vilevile, Mamlaka itajenga kiwanja cha ndege katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere; kambi moja (1) ya wageni (campsite) katika Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni; maeneo ya kupumzikia wageni (picnic sites) matatu (3) katika Mapori ya Akiba Mpanga Kipengere (2) na Wamimbiki (1); na njia ya waenda kwa miguu kilomita 2 katika Bustani ya Wanyamapori Tabora.

**232.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka itashiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kimataifa na Kikanda kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji pamoja na utalii wa picha na uwindaji. Miongoni mwa maonesho hayo ni *Abu Dhabi International Hunting & Equestrian Exhibition (ADIHEX, 2025), Dallas Safari Club International - USA,* Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), Nanenane na *Kizimkazi Festival* (Zanzibar).

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Kanda ya Uhifadhi Magharibi mkoani Tabora; ujenzi wa nyumba ya watumishi (1) katika Pori la Akiba Piti; ununuzi wa magari 23 kwa ajili ya shughuli za doria (18), utawala (1) na usimamizi wa utalii (4); na ujenzi wa uzio kwa ajili ya ghala la silaha katika

Pori la Akiba Lukwika-Lumesule. Vilevile, Mamlaka itawezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 163 katika fani mbalimbali; mafunzo ya ukakamavu na utayari kwa watumishi 351; na kuwezesha watumishi kushiriki katika mashindano ya SHIMUTA.

#### 5.3.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro – NCAA

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa wanyamapori kwa kufanya doria 5,492, doria maalum mbili (2) na doria za mwitikio wa haraka wa kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Sambamba na hilo, Mamlaka itajenga vituo viwili (2) vya askari katika maeneo ya Ndorobo na Mbulumbulu na kufanya ukarabati wa vituo vya askari vitatu (3) katika maeneo ya Naiyobi, Endamagha na Lemala. Aidha, Mamlaka itafunga visukuma mawimbi kwa faru 32 ili kufuatilia mienendo yao ndani ya Hifadhi pamoja na kuwapatia mafunzo askari 33 katika mfumo wa kufuatilia mienendo ya faru.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Mamlaka itasafisha mpaka wenye urefu wa kilomita 200 na kuweka vigingi 150 kwa lengo la kuweka alama ya mipaka na kuepusha changamoto ya moto holela. Aidha, Mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano na jamii zinazopakana na hifadhi kwa kuwezesha miradi ya maendeleo na kufanya mikutano 108 ya ujirani mwema kwa lengo la kutoa elimu ya uhifadhi na kutatua migogoro. Sambamba na hilo, Mamlaka itafanya mafunzo kwa vikundi vitano (5) vinavyozunguka Hifadhi. Mafunzo hayo ni katika eneo la ufugaji bora wa nyuki, kuongeza thamani mazao ya nyuki na utafutaji wa masoko ya nyuki.

**236.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kuondoa mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,000 lililoathirika ndani ya hifadhi. Vilevile, hekta 8,000 zitachomwa moto kupitia moto mpango ili kuboresha nyanda za malisho katika maeneo hayo. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaotesha jumla ya miche ya miti 100,000 na kuigawa kwa wadau mbalimbali na jamii zinazopakana na hifadhi kwa lengo la kuimarisha mfumo wa ikolojia wa Serengeti-Masai Mara.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha miundombinu ya utalii, Mamlaka itajenga barabara zenye jumla ya kilomita 64.5 ambazo ni Loduare hadi Golini kilomita 29.5 kwa kiwango cha tabaka gumu la zege, Enduleni hadi Olpiro kilomita 15 kwa kiwango cha changarawe na mtandao wa barabara za Ndutu kilomita 20 kwa kiwango cha changarawe. Vilevile, Mamlaka itafanya ukarabati wa mtandao wa barabara wenye kilomita 346 na ukarabati wa viwanja viwili (2) vya ndege Ngorongoro na Ndutu. Sambamba na hilo, Mamlaka itachimba kisima kimoja (1) Laitole na kusimika pampu tano (5) za maji katika kisima cha Olduvai (1), Ndutu (1), kituo cha Askofu (1) na Lerai (2). Katika hatua nyingine, Mamlaka itafunga umeme wa nishati ya jua katika vituo vya askari vinne (4) vilivyopo maeneo ya Galusi, Ndolobo, Lostete na Olduvai na itafanya ukarabati katika vituo vya huduma za utalii sita (6) katika maeneo ya Lemala, Ngoitiktok, *Viewpoint*, Simba A, Lerai na Mumba.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka itaendelea kuongeza thamani vivutio vya utalii kwa kuboresha njia za watembea kwa miguu (walking trails) katika eneo la Endoro na Empakai; kuendelea na utangazaji wa vivutio na matukio mbalimbali kutoka hifadhini mubashara kupitia Ngorongoro *live streaming* na; kushiriki katika matukio na maonesho ya utalii na uhifadhi ndani ya nchi (15) na nje ya nchi (14) pamoja na misafara ya

utalii mitano (5) na kampeni nne (4) za ndani kwa ajili ya kuhamasisha utalii wa ndani.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea na jukumu la kutoa ufadhili wa ada, fedha ya kujikimu na nauli kwa wanafunzi wenyeji 1,347: katika ngazi za chuo kikuu wanafunzi 14, vyuo vya kati wanafunzi 167, na sekondari wanafunzi 1,166. Aidha, Mamlaka itaendelea na huduma ya ugawaji unga wa uji na sukari kwa shule 26 za msingi zilizopo ndani ya hifadhi, ujenzi wa vyoo vitano (5) katika shule za msingi za Bulati, Ildonyo, Makao mapya, Meshili na Misigiyo. Vilevile, Mamlaka itaendelea na utoaji wa huduma za afya kwa wakazi ndani ya Hifadhi katika zahanati ya Mamlaka.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi Mamlaka itakamilisha ujenzi wa ofisi ya Makao makuu wilayani karatu katika eneo la Kamny. Aidha, Mamlaka itawezesha watumishi 35 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 80 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Mamlaka itawawezesha watumishi 93 kuhudhuria katika mashindano ya SHIMUTA pamoja na mashindano mengine ambayo Mamlaka inaalikwa kushiriki.

#### 5.3.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania – TAWIRI

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi itaendelea kufanya, kuratibu, na kusimamia tafiti za wanyamapori kwa lengo la kuhakikisha uhifadhi na utalii endelevu. Maeneo ya kipaumbele katika tafiti zitakazofanyika ni pamoja na; tafiti za mahusiano ya viumbe na ikolojia zao; afya ya mifumo ikolojia; uhifadhi wa bioanuai na urejeshwaji wa baadhi ya wanyamapori katika mifumo ikolojia mbalimbali; matumizi ya teknolojia katika uhifadhi; na

migongano kati ya binadamu na wanyamapori. Aidha, Taasisi itatekeleza zoezi la kuidadi wanyamapori aina ya Kanivora katika mifumo ikolojia 9 nchini. Vilevile, Taasisi itasambaza matokeo ya tafiti kwa Serikali na wadau wa uhifadhi na utalii, kuandaa Kongamano la 15 la Kimataifa la Kisayansi na kutoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi na mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi 12 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 40 ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

#### 5.3.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka – CAWM

**243.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka kitaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo kwa kudahili wanafunzi wapatao 1,498 katika fani za Usimamizi wa Wanyamapori na Utalii; na Usimamizi wa Mazingira na Uthibiti wa taka. Kozi hizo zitatolewa katika ngazi ya Cheti cha Msingi hadi Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi katika Nyanja za Usimamizi wa Wanyamapori, Utalii na Usimamizi wa Mazingira na Udhibiti wa taka.

**244.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha utoaji wa mafunzo na kutoa mchango katika utatuzi wa changamoto zinazokabili Sekta ya Wanyamapori na Utalii, Chuo kitaendelea kufanya tafiti katika nyanja za bioanuwai, uhifadhi wa mazingira na jamii ya mimea, Uhifadhi wa wanyamapori, magonjwa ya wanyamapori na binadamu, Usimamizi wa utalii na Migongano baina ya wanyamapori na binadamu. Aidha,

Chuo kitaendelea kutekeleza jukumu la kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na ugani kwa wadau mbalimbali wakiwemo Serikali na Taasisi zake pamoja na Sekta binafsi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi na wanafunzi, Chuo kitajenga jengo la Maktaba ya Kisasa, Darasa moja (1), ghala la silaha (1) na uzio wa ukuta katika Kampasi ya Chuo. Aidha, Chuo kitakarabati mabweni manne (4), madarasa mawili (2), nyumba tano (5) za watumishi, ofisi nane (8) na kujenga njia za ndani zenye urefu wa kiomita 1.5 katika Kampasi kuu ya Chuo. Vilevile, Chuo kitanunua na kufunga vifaa vya TEHAMA, kununua mabasi mawili (2) na mahema 100 kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi. Sambamba na hilo, Chuo kitaweka miundombinu ya umeme na kuchimba kisima kimoja (1) cha maji katika eneo la mafunzo lililoko Arash, Tarafa ya Loliondo.

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua nyingine, Chuo kitaandaa mitaala mipya miwili (2) katika nyanja za Usimamizi wa Malikale (Cultural Heritage Management) na Uendeshaji wa Utalii na Safari (Travel and Tourism Management). Aidha, Chuo kitafanya mapitio ya program za mafunzo zilizopo ili kutoa elimu yenye tija katika kutatua changamoto za wanyamapori na utalii nchini.

**247.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwajengea watumishi uwezo wa kufanya kazi kwa weledi na kuongeza tija, Chuo kitawawezesha watumishi 36 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 85 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitaajiri watumishi wapya 22 ili kukidhi mahitaji ya utendaji na kuendelea kutoa stahiki kwa watumishi wa Chuo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na miongozo.

#### 5.3.1.8 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC)

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo cha mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa wanafunzi 489, kati yao wanafunzi 169 watapatiwa mafunzo ya muda mrefu na 320 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, kituo kitaendelea kushiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa ajili ya kutangaza shughuli za kituo na kutoa elimu.

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, kituo kitaendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga nyumba moja (1) ya watumishi, bweni moja (1), na kukamilisha ujenzi wa nyumba moja (1) ya watumishi. Aidha, kituo kitanunua vifaa vya mafunzo na malazi ikiwemo kompyuta (35), meza za kompyuta 35, vitanda 100, magodoro 200 na madawati 100. Sambamba na hilo, Kituo kitaweka mfumo wa maktaba mtandao (E- Library) pamoja na kufanya mapitio ya mtaala wa kozi ya Stashahada ya Utalii na Uongozaji Watalii. Vilevile, Kituo kitaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwezesha watumishi sita (6) kushiriki mafunzo ya muda mfupi na watumishi wawili (2) wataendelea na masomo ya muda mrefu.

#### 5.3.1.9 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi – PWTI

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taasisi itadahili wanafunzi 670 katika fani za Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji Watalii na Usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Vilevile, Taasisi itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 250. Katika hatua nyingine, Taasisi itaanza kufundisha Kozi za Stashahada ya Uaskari wa Wanyamapori na Uongozaji watalii na Usalama.

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Taasisi itawezesha watumishi watatu (3) kuendelea na masomo ya muda mrefu. Aidha, taasisi itakamilisha ujenzi wa maktaba na uzio; kujenga bweni la ghorofa mbili (2) lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 240, madarasa manne (4) ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400. Vilevile, Taasisi itachimba kisima kimoja (1) cha maji katika kambi mpya ya mafunzo iliyoko Kata ya Matongo Wilaya ya Bariadi.

### 5.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

#### 5.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya Mwaka 2002; Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (CBFM) wa Mwaka 2007 na Mwongozo wa Uvunaji Endelevu katika Misitu ya Asili. Vilevile, Wizara itaandaa miongozo mitano (5) ikiwemo Mwongozo wa Kitaifa wa Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mashamba ya Miti, Mwongozo wa Bima ya Mazao ya Misitu na Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Mazao ya Nyuki Tanzania. Sambamba na hilo, Wizara itatafsiri na kusambaza Kanuni, Miongozo na Mikakati mbalimbali ya Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki kwa wadau.

**253.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuimarisha ushiriki wa jamii kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara itatekeleza Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Ufugaji Nyuki kwa Tanzania Iliyo Bora kwa kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki, kuwezesha mizinga ya nyuki 13,000 na mavazi ya kinga 650 kwa vikundi vya wafugaji nyuki 130. Aidha, Wizara itawezesha uanzishwaji wa hifadhi za nyuki tatu (3) na hifadhi za misitu zenye ukubwa wa hekta

10,000 na kuandaa mipango mitano (5) ya usimamizi wa hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau 1,500 kuhusu mikakati ya mazao ya misitu yaliyohandisiwa, zao la mianzi na kilimo misitu, matumizi ya nishati safi ya kupikia na fursa za biashara ya hewa ya kaboni katika kanda tatu (3) za TFS. Kwa upande mwingine, Wizara itafanya mikutano miwili (2) baina ya Wizara za kisekta na wadau wa misitu na ufugaji nyuki kuhusu fursa na changamoto zilizopo katika sekta ya misitu na nyuki. Wizara pia itawajengea uwezo maafisa ufugaji nyuki pamoja na kununua pikipiki 20 kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za ufugaji nyuki.

**254.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande mwingine, Wizara itafanya vikao vitatu (3) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki (NABAC); vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Misitu (NAFAC); Vikao viwili (2) vya Kamati ya Uendashaji ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa na vikao viwili (2) vya Kamati Kuu ya Maandalizi ya Mkutano Mkuu wa 50 wa Wafugaji Nyuki Duniani (APIMONDIA). Aidha, Wizara itaanzisha Baraza la Wataalam wa Misitu; na jukwaa la wadau wa biashara ya hewa ya kaboni na kilimo misitu.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazao yatokanayo na misitu na nyuki, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya viwanda vya misitu na ufugaji nyuki, utekelezaji wa miradi na programu za misitu na ufugaji nyuki pamoja na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara itashiriki mikutano na warsha za kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Mkutano wa 49 wa APIMONDIA; Vikao vya Ushirikiano katika Sekta ya Misitu na Nyuki baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Kamati ya Misitu ya Dunia (COFO); na kuratibu ushiriki katika maonesho ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Siku ya Kitaifa ya Upandaji Miti na Siku ya Misitu na Nyuki Duniani.

### 5.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania – TFS

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wakala utaimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuandaa Mipango ya Usimamizi ya Misitu 16 yenye ukubwa wa hekta 221,825 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi 32. Aidha, Wakala utafanya jumla ya doria 16,688 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Vilevile, Wakala utaimarisha mipaka ya misitu 170 kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 554; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,394; kuweka vigingi 1,675; mabango 279; na kununua ndege nyuki (drones) 3.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza kampeni ya Tanzania ya Kijani na kukidhi mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu nchini, Wakala utaanzisha mashamba mapya mawili ya miti (Geita na Rwamgasa) yenye jumla ya hekta 28,000; kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za miti nchini kwa kuanzisha vyanzo vipya 12 vya mbegu; kuzalisha tani 27.5 za mbegu; na miche ya miti milioni 35.2. Aidha, Wakala utaendeleza mashamba 24 ya miti kwa kupanda miti katika eneo lenye hekta 7,052; kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 2,084; kupalilia eneo lenye hekta 34,031; kupogolea hekta 9,447; na kupunguzia miti kwenye hekta 3,208. Vilevile, Wakala utapanda miche ya mikoko takriban 79,000 katika eneo la hekta 57 ili kurejesha uoto wa asili katika maeneo hayo.

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala utaimarisha miundombinu ya utalii katika misitu ya hifadhi kwa: kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 223 za kuwezesha kufika kwenye hifadhi; mabanda matano (5) ya kupumzika watalii katika hifadhi ya mikoko Wilaya ya Kinondoni; geti moja (1) katika kituo cha NAFRAC - Shinyanga; na kukarabati kilomita 301.6 za njia za watalii, kilomita 112.1 za barabara za kufika kwenye hifadhi, na

kambi 21 katika hifadhi za misitu 33. Aidha, Wakala utaimarisha vituo vya utalii wa malikale kwa kujenga kituo cha utalii wa nyuki, na kukarabati makaburi 15 ya kihistoria katika vituo vya Michoro ya Miambani Kolo - Kondoa, Mji Mkongwe - Bagamoyo, Tembe la Kwihara - Tabora, Magofu ya Tongoni - Tanga na Kaole - Bagamoyo.

**259.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala utaendeleza mashamba matatu (3) ya nyuki na manzuki 82; kuzalisha tani 45 za asali; tani 3 za nta; kusimamia viwanda vitatu (3) vya mazao ya nyuki; kutoa elimu kwa wafugaji nyuki 161; na kuchonga mizinga ya nyuki 2,500. Vilevile, Wakala utakusanya sampuli 126 za asali kutoka wilaya 30 na kuzipeleka Maabara ya kimataifa nchini Ujerumani kwa ajili ya kuhakiki viwango vya ubora wa asali inayozalishwa nchini Tanzania kwa lengo la kuongeza wigo katika masoko ya kimataifa.

**260.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala utaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kukamilisha ujenzi wa vituo vitano (5) vya ulinzi (ranger posts); kujenga ofisi saba (7) ikiwemo jengo la Makao Makuu ya Wakala moja (1) Jijini Dodoma, Ofisi za Wilaya sita (6) za Simanjiro, Bahi, Ngorongoro, Mkinga, Rombo na Kakonko; vituo saba (7) vya askari, na nyumba tatu (3) za watumishi. Vilevile, Wakala utanunua magari nane (8), malori mawili (2), pikipiki 40, boti tatu (3) na trekta moja (1). Aidha, Wakala utawezesha watumishi 75 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na 685 ya muda mfupi katika fani mbalimbali.

### 5.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania – TAFORI

**261.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, TAFORI itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Tatu wa Utafiti wa Misitu (2021 – 2031) na

Mpango Kabambe wa Kwanza wa Utafiti wa Ufugaji Nyuki (2020 – 2030). Aidha, TAFORI itafanya utafiti wa kuangalia jinsi wadudu wachavushao wanavyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwenye milima ya Uluguru na Udzungwa Mkoani Morogoro. Aidha, TAFORI itakamilisha tathmini ya miti dawa na matumizi yake kwa ajili ya kuboresha maisha na uhifadhi wa misitu katika eneo la Milima ya Tao la Mashariki. Vilevile, TAFORI itaendelea na utafiti wa kuchunguza athari za mizunguko ya uvunaji wa spishi za miti aina ya misindano na mikaratusi kwenye uzalishaji na ubora wa mbao; kufanya utafiti kuhusu gharama na faida ya uzalishaji wa utomvu unaofanywa na wakulima wadogo wa miti katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa. Sambamba na hilo, TAFORI itaendelea na utafiti juu ya kudhibiti mimea vamizi kwenye maeneo ya hifadhi; na kufanya utafiti wa nyuki wasiodunga na aina ya mizinga inayofaa kwa kufugia katika maeneo mbalimbali nchini. Pia, TAFORI itafanya utafiti wa namna bora ya kutumia tasnia ya ufugaji nyuki kuboresha utalii wa nyuki (*Api-tourism*); na kuanzisha manzuki za utafiti na mashamba ya kuzalisha mazao ya nyuki katika Mikoa ya Dodoma, Shinyanga na Singida.

**262.** ***Mheshimiwa Spika***, Kwa upande mwingine, TAFORI itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kukarabati maabara na jengo la Ofisi ya Makao Makuu, kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Tabora na kuweka vitendea kazi kwenye jengo la Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Kibaha. Vilevile, TAFORI itaimarisha uwezo wa kitalu cha miti kilichopo katika Kituo cha Utafiti wa Misitu cha Kibaha kwa kuboresha teknolojia ya uzalishaji wa miche ya miti ili kuongeza upatikanaji wa vipando bora vya miti katika maeneo ya Pwani ya Tanzania. Aidha, TAFORI itaendelea kuwezesha watumishi 11 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, 28 mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 25 wa kada mbalimbali.

### 5.3.2.4 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora – BTI

**263.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitadahili wanafunzi 420 kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau wa Sekta ya Nyuki kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam juu ya masuala mbalimbali ili kuendeleza na kukuza Sekta ya Nyuki. Vilevile, Chuo kitaendelea na ujenzi wa awamu ya pili wa bweni la wanafunzi wa kike, ujenzi wa maabara, kujenga uzio kuzunguka eneo la Chuo; kukarabati nyumba mbili (2) za watumishi; kununua vifaa saba (7) na mashine tatu (3) vya karakana ya mbao kwa ajili ya kutengeneza mizinga ya nyuki; pamoja na kuimarisha mifumo ya TEHAMA. Katika hatua nyingine, Chuo kitawezesha mtumishi mmoja (1) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitashiriki katika maonesho mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

### 5.3.2.5 Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kitakuwa na jukumu la kutoa mafunzo ya ujuzi na ufundi stadi katika matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Chuo kitadahili wanafunzi 500 wa teknolojia ya viwanda vya misitu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada, pia wanafunzi 100 katika elimu ya ufundi stadi. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam katika matumizi endelevu ya mazao ya misitu na nishati mbadala kwa wananchi. Kwa upande mwingine, Chuo kitashirikiana na wadau mbalimbali kuandaa maandiko ya miradi ya maendeleo.

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kitaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200; ukarabati wa madarasa mawili (2) na mabweni mawili (2) mjini Moshi; darasa moja (1) na bweni moja (1) katika kituo cha mafunzo kilichopo West Kilimanjaro. Vilevile, Chuo kitaendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kuboresha utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha watumishi wanne (4) kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 33 kupata mafunzo ya muda mfupi.

#### 5.3.2.6 Chuo cha Misitu, Olmotonyi - FTI

**266.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Misitu, Olmotonyi kitadahili wanafunzi 930 katika ngazi ya astashahada na Stashahada ya misitu. Katika hatua nyingine, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 200 na ushauri wa kitaalamu wa misitu na uhifadhi wa mazingira kwa wanafunzi katika shule 10 za Msingi na Sekondari katika Wilaya ya Arumeru na Jiji la Arusha. Sambamba na hilo, Chuo kitajenga miundombinu ya utalii ikolojia, kitakarabati bwalo la chakula la wanafunzi na maktaba. Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Chuo kitawezesha watumishi wanne (4) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 10 ya muda mfupi. Vilevile, Chuo kitashiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

#### 5.3.2.7 Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu - FWITC

**267.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu cha Mafinga kitadahili wanafunzi 80 katika ngazi ya ufundi stadi wa misitu na viwanda vya misitu. Katika hatua nyingine, Kituo

kitatoa mafunzo ya muda mfupi ya misitu na viwanda vya misitu kwa wakulima wadogo 200 wa miti. Sambamba na hilo, Kituo kitajenga bweni moja (1) la wanafunzi. Aidha, katika kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi, Kituo kitawezesha watumishi wawili (2) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi nane (8) wa muda mfupi. Vilevile, Kituo kitashiriki katika maonesho na matukio mbalimbali kwa lengo la kujitangaza.

#### 5.3.2.8 Mfuko wa Misitu Tanzania – TaFF

**268.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mfuko utaendelea kuwezesha na kugharamia miradi ya kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu na nyuki kwa kutoa ruzuku kwa miradi 183 ambayo utekelezaji wake unaendelea na miradi mipya 120 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti, upandaji miti, ufugaji nyuki na miradi ya nishati mbadala. Aidha, Mfuko utaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 katika Chuo cha FITI kwa lengo la kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa wanafunzi wa kike pamoja na kuendelea kugharamia ujenzi wa jengo la Ofisi ya Kituo cha Utafiti wa Misitu mkoani Tabora. Vilevile, Mfuko utaendelea kugharamia tafiti mpya tano (5) za kimkakati zinazoratibiwa na TAFORI zenye lengo la kuboresha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu.

**269.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko utaendelea kugharamia masomo ya shahada ya uzamili na uzamivu kwa fani ambazo zina watalaam wachache hapa nchini ambazo ni uboreshaji wa vizazi vya miti *(tree breeding)* na utambuzi wa magonjwa ya miti na misitu *(forestry pathology).* Mafunzo hayo yataboresha na kuongeza uzalishaji wa mazao ya misitu hususani mazao ya misitu kutoka mashamba ya miti ya kupandwa.

**270.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko utaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi za Mfuko katika eneo la Nzuguni 'C' Jijini Dodoma. Aidha, Mfuko utaendelea na utekelezaji wa muundo mpya kwa kuongeza watumishi katika kada za uchumi, sheria na mawasiliano pamoja na kuongeza watumishi katika vitengo vingine ili kuweza Mfuko kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Vilevile, Mfuko utaendelea kuboresha utendaji kazi kwa kuwezesha watumishi wawili (2) kushiriki mafunzo ya muda mrefu na watumishi 12 kushiriki mafunzo ya muda mfupi.

### 5.3.3 Sekta ya Utalii

#### 5.3.3.1 Idara ya Utalii

**271.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kutanua wigo wa mazao ya utalii na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, Wizara itafanya ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne (4) za Kaskazini, Kusini, Mashariki na Kati pamoja na kufanya uhakiki wa wakala wa biashara za utalii. Vilevile, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora wa nyota katika mikoa 18 pamoja na kubaini vivutio vya utalii katika mikoa 16 kwa mujibu wa Sheria ya Utalii, Sura ya 65.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau wa utalii kuhusu matumizi ya mfumo wa kusajili wageni MNRT Portal; na mafunzo ya mfumo wa kujitathmini na kupanga ubora wa nyota kwa huduma za malazi AserT. Wizara pia itaandaa warsha mbili (2) za kuhamasisha na kuwajengea uelewa wadau wa utalii kuhusu vigezo vya kupanga huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora wa nyota. Sambamba na hilo, Wizara itaandaa warsha (2) zitakazoshirikisha wadau kuhusu umuhimu wa utambuzi wa mazao mapya ya utalii. Hatua hizi zinalenga kuimarisha huduma za utalii nchini.

**273.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Utalii nchini, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008; Kanuni za Usajili na Utoaji Leseni za Wakala wa Utalii za Mwaka 2015; Kanuni za Huduma za Malazi za Mwaka 2015 na Kanuni za Waongoza Wageni za Mwaka 2015. Vilevile, Wizara itafanya mapitio ya Mwongozo wa Usajili na Utoaji wa Leseni kwa Wakala wa Biashara za Utalii pamoja na kufanya mikutano minne (4) ya kuwajengea uwezo wadau kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Utalii. Sambamba na hilo, Wizara itafanya mikutano mitatu (3) ya wadau wa utalii ili kujadili masuala yanayohusu uendelezaji wa mazao ya utalii ya kimkakati. Wizara pia, itashiriki matamasha, matukio, maonesho na mikutano ya mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kutoa elimu kuhusu shughuli za utalii.

#### 5.3.3.2 Tozo ya Maendeleo ya Utalii – TDL

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Tozo ya Maendeleo ya Utalii (TDL) itawezesha Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya utalii katika maeneo ya hifadhi ikiwemo malango ya kuingilia wageni, maeneo ya kupumzikia, kambi za watalii, migahawa, mabanda ya watalii, vituo vya burudani vya utalii; *picnic site,* vituo vya taarifa na kumbukumbu pamoja na miundombinu ya michezo na burudani ikiwemo viwanja vya mpira na bwawa la kuogelea. Aidha, TDL itawezesha ujenzi na ukarabati wa majengo ya kihistoria na barabara katika maeneo ya hifadhi.

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha masoko ya utalii ndani na nje ya nchi, TDL itawezesha kutangaza vivutio vya utalii kupitia maonesho, matamasha na mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa na kuanzisha ushirikiano na vyombo vya habari vya Kimataifa na Klabu kubwa za michezo Duniani. Aidha, itawezesha utoaji wa mafunzo ya utalii na ukarimu,

kufanya tafiti mbalimbali ili kutambua masoko mapya na mahitaji ya watalii pamoja na kufanya uhakiki wa huduma za malazi. Katika hatua nyingine, TDL itawezesha ufungaji wa mabango ya kidijitali ya taarifa kwa wageni pamoja na ununuzi wa vifaa vya shughuli za utangazaji utalii ikiwemo ununuzi wa vifaa vya maonesho.

#### 5.3.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania – TTB

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kutekeleza jukumu la kutangaza na kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya Nchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kutangaza utalii kupitia mashirika ya ndege ya kitaifa na kimataifa yakiwemo *Air Tanzania Company Limited*, *Turkish Airlines*, *Emirates* na *Qatar Airways* kwa kuweka matangazo mbalimbali; kutumia Ligi za michezo zenye wafuatiliaji wengi ikiwemo CHAN, AFCON na Ligi za mpira zilizopo nchini; kuendelea kuandaa na kurusha makala za vivutio vya utalii kupitia vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa kama *Expedia Group*. Pia, Bodi itaratibu utangazaji wa Filamu ya *Amazing Tanzania* kwenye vyombo mbalimbali vya habari vya Nchini China. Kadhalika, Bodi itakamilisha uandaaji wa maudhui ya kutangaza vivutio vyetu vya utalii katika soko la India kupitia watu maarufu wa Nchini humo. Kwa upande mwingine, Bodi itaendelea kutumia treni za kisasa za Shirika la Reli Tanzania kutangaza na kusafirisha watalii wa kitaifa na kimataifa kutembelea vivutio vya utalii.

**277.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea kutumia Mabalozi wa Hiari na watu mashuhuri katika kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya Nchi. Pia, Bodi itaratibu Kampeni mbalimbali zinazolenga kuhamasisha utalii wa ndani hususan wakati wa mapumziko ya sikukuu za kitaifa, likizo na msimu wa mwisho wa mwaka.

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi zetu za Ubalozi zilizopo katika nchi mbalimbali kutangaza utalii kupitia misafara ya utangazaji utalii (Road Shows) kwenye Bara la Amerika, Asia, Ulaya na Mashariki ya Kati; ziara za mafunzo (Familiarization Trips) kwa waandishi wa habari, wakala wa utalii na watu wenye ushawishi kutoka kwenye masoko ya msingi na kimkakati. Vilevile, Bodi itaratibu ushiriki wa Nchi katika maonesho na matukio mbalimbali ya utangazaji utalii ndani na nje ya nchi. Aidha, Bodi itaandaa onesho la 9 la *Swahili International Tourism Expo – S!TE* 2025 kwa kushirikisha waoneshaji na wanunuzi wa Kimatifa wa bidhaa za utalii kwa lengo la kutangaza utalii na fursa za uwekezaji zilizopo nchini.

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutangaza na kutoa huduma za utalii kidijitali, Bodi ya Utalii Tanzania itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa kujenga mfumo wa *"Destination Portal"* wenye huduma za akili mnemba, *chatbot* na *booking platform*; pamoja na kutengeneza na kusimika mabango matano (5) ya kutangaza utalii kidijitali kwenye Jiji la Dar es Salaam (1), Arusha (1), Dodoma (1), Mwanza (1) na Mbeya (1). Aidha, Bodi itaendelea kushirikiana na wadau kutangaza mazao ya utalii ikiwemo utalii wa meli, fukwe, mikutano na matukio, michezo, uwindaji wa kitalii, utamaduni, malikale, ikolojia, miamba, kilimo, matibabu, nyuki na vyakula. Vilevile, Bodi itaendelea kuhamasisha utalii wa ndani kwa kufanya kampeni za utalii wa ndani kwa makundi mbalimbali ikiwemo wanafunzi, wafanyakazi, taasisi za kidini, wasanii na watu mashuhuri.

**280.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaongeza juhudi ya kutangaza mazao ya Utalii wa Utamaduni, Utalii wa Mikutano na Matukio, na Utalii wa Historia ili kukuza utalii wa ndani na kuvutia watalii wa kimataifa. Hatua hiyo itakwenda sambamba

na uratibu na udhamini wa matamasha mbalimbali ya utamaduni; na utangazaji wa maeneo ya kihistoria ikiwemo sehemu zenye kumbukizi za harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. Pia, Bodi itakamilisha usajili katika Shirika la Mikutano Duniani (ICCA) ili kupata fursa ya kuitangaza Tanzania kama Kituo Bora cha Utalii wa Mikutano na Matukio sambamba na kuvutia mikutano mbalimbali ya kimataifa kufanyika nchini.

#### 5.3.3.4 Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

**281.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Chuo cha Taifa cha Utalii kitaendelea na ujenzi wa jengo jipya la taaluma kampasi ya Arusha ambalo litafanikisha ongezeko la udahili wa wanafunzi kutoka 1,500 hadi 2,000. Aidha, Chuo kitapanua wigo wa huduma zake kwa: utoaji wa mafunzo; utafiti wa kisekta; na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa wadau mbalimbali walio katika mnyororo wa thamani wa utalii.

**282.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kitaendelea na mpango wa kuimarisha kampasi ya Mwanza, ili kujitanua na kufikia mahitaji ya wadau mbalimbali, kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa majengo ya taaluma katika viwanja viwili (2) Shibula na Semba vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Sambamba na hilo chuo kitaimarisha mpango wa mafunzo ya Uanagenzi *(apprenticeship)* pamoja na mpango wa kurasimisha ujuzi kwa watoa huduma za ukarimu na utalii (*Recognition of Prior Learning*).

**283.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza udahili wa wanafunzi na kuboresha utoaji huduma za utalii na ukarimu Nchini, Chuo kitaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kufanya huduma mkoba (Outreach programs) kwa kutembelea shule za Sekondari 80, kushiriki maonesho mbalimbali pamoja na kuandaa vipindi vya televisheni (5) na

redio (10) kwa ajili ya kutangaza programu za Mafunzo kwa Wanafunzi na Wadau mbalimbali wa Utalii.

**284.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kitaanza maandalizi ya Kongamano la 4 la Kimataifa (The 4th Linking Industry with Academia in the Tourism and Hospitality in Developing Countries (LIATH-DC)) litalokutanisha Wadau na Wanataaluma katika masuala ya Utalii na Ukarimu.

**285.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kitaendelea na utekelezaji wa Mpango wa mafunzo kwa Watumishi 46 kuwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya Nchi ambapo watumishi 8 watapata mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Uzamili (Masters) na Uzamivu (PhD) na watumishi 38 watawezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi. Utoaji wa mafunzo hayo utajikita zaidi katika fani za ukarimu, utalii na uratibu wa matukio.

### 5.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

#### 5.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

**286.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara itatangaza maeneo sita (6) ya malikale kuwa Urithi wa Taifa, kukusanya taarifa za kiuhifadhi za maeneo 25 ya malikale kwa ajili ya kuhuisha orodha ya Urithi wa Taifa; kufanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo nane (8) yaliyopo kwenye Orodha ya Urithi wa Taifa katika mikoa ya Mara, Geita, Kagera na Shinyanga; na kufanya ukaguzi wa hali ya uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 10 ya malikale, makumbusho saba (7), kusajili makumbusho binafsi pamoja na kuratibu utatuzi wa migogoro ya mipaka katika maeneo matano (5) ya malikale. Aidha, Wizara itafanya vikao viwili (2) vya wadau katika mikoa miwili (2) kwa ajili ya kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008, kuratibu vikao

vinne (4) vya Kamati ya Majadiliano kuhusu masuala ya urejeshwaji wa malikale za Tanzania zilizopo nje ya nchi; na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba miwili (2) ya uhifadhi kati ya Wizara na wadau.

**287.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Wizara itafanya vikao viwili (2) vya wadau kwa ajili ya kupata maoni kuhusu mwongozo wa kutwaa na kuhamisha umiliki wa rasilimalikale na kufanya kikao kimoja cha wadau kwa ajili ya kutathimini utendaji wa sekta. Vilevile, Wizara itashiriki mikutano ya kikanda na kimataifa inayohusu uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Pia, Wizara itafanya tathmini na kuandaa andiko la kuorodhesha njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Katika hatua nyingine, Wizara itawezesha watumishi watano (5) kupata mafunzo ya muda mrefu na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo pamoja na kushiriki katika maonesho na matamasha ya kitaifa ikiwemo Sabasaba na Nanenane kwa lengo la kuhamasisha matumizi endelevu ya malikale.

#### 5.3.4.2 Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale – NFA

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mfuko wa Mambo ya Kale utawezesha maandalizi ya kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura ya 333 na miongozo ya Uhifadhi wa maeneo ya malikale; ukusanyaji wa taarifa za uhifadhi wa maeneo 30 ya malikale ili yaweze kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa; maandalizi ya Mpango wa Uhifadhi wa Makumbusho ya Mtwa Mkwawa- Kalenga; na usimamizi wa hali za uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 45 ya Urithi wa Taifa.

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika hatua nyingine, Mfuko utawezesha ushiriki wa Wizara katika maonesho kwa lengo la

kubainisha na kutangaza shughuli za Mifuko; kufanya vikao vya wadau vya kujadili uhifadhi wa Nyayo za ZAMADAMU Laetoli na Engarasero; utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwl. Nyerere; na kuwezesha mafunzo ya uhifadhi wa maeneo na majengo ya kihistoria.

#### 5.3.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT

**290.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Shirika litaendelea kuhifadhi na kuendeleza urithi wa malikale na mikusanyo kwa kufungua kituo cha taarifa chenye historia ya kuanza kwa vita ya Majimaji, Nandete-Kilwa na kujenga nyumba za asili 3 kwa mfumo wa kaya katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Vilevile, Shirika litasimamia ukarabati wa majenzi ya kale 18 katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara pamoja na kutumia mifumo ya TEHAMA kuhifadhi kumbukumbu za maeneo hayo. Pia Shirika, litaendelea kushirikisha wadau binafsi na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale nchini.

**291.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Shirika litaboresha miundombinu ya utalii na uhifadhi kwa kuboresha maonesho manne (4) ya kudumu katika kituo cha Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni-Dar es Salaam, kufungua maonesho mapya matatu (3) ya kudumu katika vituo vya Mbuamaji-Kigamboni (1), Mikumbi – Lindi Mjini (1) na Mkwajuni – Tendaguru (1). Aidha, Shirika litaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika shughuli za utalii na uhifadhi zikiwemo usajili wa mikusanyo na maonesho. Vilevile, Shirika litakarabati stoo mbili (2) za uhifadhi wa mikusanyo katika kituo cha Majimaji-Songea (1) na Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni-Dar es Salaam (1).

**292.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika litaendelea kutangaza vivutio vya malikale na makumbusho ili kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia matamasha manne (4) ya urithi wa mtanzania, maonesho, matukio, warsha na programu zenye kujenga uelewa kuhusiana na utalii wa malikale. Vilevile, Shirika litafanya tafiti tano (5) za masuala ya urithi wa utamaduni na kutoa vibali vya utafiti katika maeneo ya malikale; kukusanya na kuhifadhi mikusanyo 1,000 ya asili na kiutamaduni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa makumbusho binafsi. Aidha, Shirika litaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makumbusho ya Marais, Dodoma na kuratibu Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi, Kutangaza na Kuhifadhi Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika hatua nyingine, Shirika litawezesha watumishi saba (7) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu, 35 mafunzo ya muda mfupi na kuajiri watumishi wapya 41 wa kada mbalimbali.

## 5.4 Miradi ya Maendeleo

**293.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 105,749,922,000.00** kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 32,476,051,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo **Shilingi 105,749,922,000.00** zinajumuisha **Shilingi 34,348,073,903.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Idara na Vitengo vilivyo chini ya Wizara; na **Shilingi 71,401,848,097.00** za Miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, TAWA, TFS, NMT, NCT na TAWIRI).

**294.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

## (A) Mradi wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programe VI)

Mradi wa Programu ya maboresho ya usimamizi wa Fedha za Umma Awamu ya Sita (PFMRP VI) ni mradi wa ubia wa maendeleo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Benki ya Dunia. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 57,476,764.00** fedha za ndani na **Shilingi 920,000,000.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kujenga jukwaa la kufungamanisha na kubadilishana taarifa za mifumo ya Sekta ya Maliasili na Utalii (MNRT Faru-Gateway);

(ii) Kuboresha miundombinu ya "datacenter" ya Wizara pamoja na "Disaster Recovery ya Wizara"; na

(iii) Kuwezesha mafunzo kwa watumishi tisa (9) kuhusu utafiti na ubunifu wa miradi ya maendeleo.

## (B) Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 18,682,561,593.00** fedha za ndani kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania (Southern Tanzania Destination Marketing Center) katika eneo la Kihesa Kilolo-Iringa;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliji

katika skimu za mabonde madogo ya mito Chimala na Kimani kwa ujenzi wa Skimu za Mbuyuni-Kimani na Makangarawe katika Wilaya ya Mbarali;

(iii) Kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Madibira;

(iv) Kuwezesha huduma za ushauri elekezi katika ujenzi wa Kituo cha Utangazaji Utalii Kusini mwa Tanzania katika eneo la Kihesa Kilolo-Iringa;

(v) Kuwezesha ujenzi wa Malambo ya kunywesha mifugo (cattle troughs) katika vijiji vya Ikanutwa, Mabadaga, Mahango, Manienga na Itamboleo katika Wilaya ya Mbarali; na

(vi) Kuwezesha Usimamizi na Uratibu wa mradi kwa kufanya Tathmini na Ufuatiliaji, Usimamizi wa Fedha, Manunuzi na upatikanaji wa vitendea kazi kwa watekelezaji wa mradi.

**(C) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves)**

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani, Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 1,114,138,124.00** kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ukarabati wa miundombinu na Majengo chakavu PASIANSI; na

(ii) Ununuzi wa visukuma mawimbi 50 pamoja na mabomu baridi 20,000.

### (D) Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Combating Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania)

Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) inatekeleza Mradi wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara unaofadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira "Global Environmental Facility – GEF" katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 2,586,276,000.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwezesha mafunzo ya mbinu za kisayansi za uchunguzi wa makosa ya ujangili na biashara haramu ya nyara kwa maafisa kutoka Kikosi Kazi Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP) na Kanda za Ki-ikolojia za Kuratibu Doria (TCGs);

(ii) Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuwezesha utendaji wa mfumo wa kukusanyia taarifa na kuratibu doria;

(iii) Kuwezesha doria za ki-intelijensia za kupambana na ujangili katika mifumo ikolojia yenye changamoto ya ujangili;

(iv) Kuwezesha tathmini ya kisayansi kuhusu hali ya ujangili nchini na uwezo wa Serikali kukabiliana nao;

(v) Kuwezesha ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Chamwino;

(vi) Kuwezesha tathmini ya rasilimali za wanyamapori katika eneo la Ikungi na kuandaa Mpango wa Kanda wa Usimamizi WMA tarajiwa ya Ikungi;

(vii) Kuwezesha utekelezaji wa mbinu shirikishi za kukabiliana na Wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yanayopakana na hifadhi kwenye Wilaya ya Itigi;

(viii) Kuwezesha jamii katika Jumuiya za ufugaji nyuki za Mwakintaru, Muhesi na WMA ya WAGA mizinga na vifaa vya kusindika mazao ya nyuki ili kuongeza thamani;

(ix) Kuwezesha kampeni za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara za wanyamapori katika maeneo yanayozunguka hifadhi kwenye mfumo Ikolojia wa Ruaha – Rungwa;

(x) Kuwezesha mafunzo ya uongozi kwa Bodi ya Ushauri wa Maliasili pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa Askari wa Vijiji katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Jamii Chamwino; na

(xi) Kuwezesha utekelezaji wa Mpango Shirikishi wa Kijamii wa Ufuatiliaji wa Vitendo vya Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara katika Kanda ya Kiikolojia ya Kuratibu Doria Moyowosi – Ugalla.

**(E) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping)**

Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mradi utatumia **Shilingi 570,403,992.00** fedha za ndani kwa ajili ya

(i) Kujenga maabara ya kisayansi ya mafunzo kwenye Chuo cha Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI);

(ii) Kukarabati miundombinu na majengo chakavu FITI;

(iii) Kukarabati miundombinu na majengo chakavu FTI; na

(iv) Kukarabati miundombinu chakavu – TAFORI.

**(F) Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC)**

Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Umoja wa Ulaya. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi utatumia **Shilingi 1,842,401,666.00** fedha za nje kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kujenga vituo vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika Wilaya za Uyui, Urambo na Itigi;

(ii) Kuandaa mipango ya biashara (business plan) kwa ajili ya vituo vya kukusanyia asali na mazao mengine ya nyuki katika wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo na Mlele;

(iii) Kuanzisha Ukanda wa kufugia nyuki kwenye Hifadhi ya Msitu Kigosi (hekta 923,904);

(iv) Kuwezesha mapitio ya Sheria ya Ufugaji Nyuki Na. 15 ya Mwaka 2002 na Kanuni za Jumla za Ufugaji Nyuki za Mwaka 2005 ili ziendane na mahitaji ya sasa;

(v) Kuwezesha wadau wa ufugaji nyuki kushiriki makongamano ya kitaifa, kikanda na ya kimataifa kwa lengo la kuwaunganisha na masoko ya asali na mazao mengine ya nyuki;

(vi) Kujenga uzio na kuweka matenki ya maji kwenye vituo vya kukusanyia mazao ya nyuki vilivyopo katika wilaya za Ushetu, Sikonge, Kaliua, Tanganyika, Nsimbo na Mlele;

(vii) Kuwajengea uwezo vikundi vya wafugaji nyuki wakiwemo

vijana na wanawake na vyama vya ushirika juu ya huduma za kifedha na masuala ya teknolojia katika kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki;

(viii) Kujenga Kituo cha kuuzia asali na mazao mengine ya Nyuki (Marketing center) Wilaya ya Wete-Pemba Kaskazini;

(ix) Kuwezesha wafanyabiashara sita (6) wenye viwanda vya kuchakata asali kupata cheti cha uthibiti wa ubora wa chakula (HACCP);

(x) Kuwezesha makampuni manne (4) ya uuzaji wa asali kupata cheti cha uuzaji wa asali mahuluku (Organic Certificate);

(xi) Kukarabati kituo cha kuchakata mazao ya nyuki cha SIDO-Singida pamoja na ununuzi wa seti ya mashine za kuchakata asali;

(xii) Kuandaa mfumo wa ukusanyaji wa bei ya asali na kusambaza kupitia TANTRADE;

(xiii) Kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara 30 juu ya mbinu za utafutaji masoko ya asali; na

(xiv) Kutoa mafunzo ya kuongeza thamani mazao ya nyuki kwa wanawake wajasiriamali.

### (G) Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR)

Mradi huu unafadhilia na Mfuko wa Mazingira wa Dunia "Global Enviromental Facility – GEF" na katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 3,664,636,331.00** fedha za nje kuendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufungamanisha mipango iliyopo ya usimamizi wa kisekta katika eneo la Kilombero kwa ajili ya kuandaa mfumo Shirikishi wa Usimamizi wa Ardhi;

(ii) Kutekeleza mpango kazi wa Usimamizi Shirikishi wa vyanzo vya maji katika Bonde la Kilombero na maeneo ya Kiashange-Mokotoni na Kinyasini-Kisongoni (Zanzibar);

(iii) Kuwezesha maandalizi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi za vijiji katika maeneo ya kipaumbele Kilombero na Zanzibar;

(iv) Kutoa mafunzo na kujenga uelewa kuhusu usimamizi shirikishi wa ikolojia Kilombero na Zanzibar;

(v) Kuwezesha tathmini ya vihatarishi kwenye maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kwa ajili ya uongoaji kwenye maeneo yaliyoharibiwa  Kilombero na Zanzibar;

(vi) Kusimamia maeneo yenye thamani kubwa ya uhifadhi katika ikolojia lengwa kupitia mbinu zilizofanya vizuri kwenye maeneo mengine kwa Kilombero na Zanzibar; na

(vii) Kuwezesha wadau wanaotekeleza jitihada za uongoaji wa maeneo yaliyoharibiwa kwa kujikita zaidi kwa wakulima wadogo na sekta binafsi Kilombero na Zanzibar.

**(H) Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Misitu, Matumizi Bora ya Ardhi na Kuongeza thamani ya Mazao ya Misitu (Forestry Land Use and Value Chains Development in Tanzania- FORLAND)**

Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Ufini (Finland) na katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 4,001,200,000.00** fedha za nje kuendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo kwa Jumuiya 30 za wakulima wa miti kuhusu upandaji, utunzaji na usimamizi wa mashamba ya miti;

(ii) Kuwezesha mapitio na maandalizi ya Mipango 20 ya matumizi bora ya ardhi katika Mkoa wa Iringa;

(iii) Kujenga uwezo kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kuhusu biashara ya Mazao ya Misitu Yaliyohandisiwa pamoja na mikakati mingine ya biashara;

(iv) Kujenga uwezo kwa timu za vijiji za usimamizi wa moto kuhusu mbinu za kupambana na majanga ya moto; na

(v) Kujenga uwezo wa miundombinu ya kufundishia ya Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC).

**(I) Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Uhifadhi wa Misitu ya Mikoko (Enhancing Management of State Forest Plantations and Mangroves Forest Reserve in Tanzania)**

Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa na katika mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 32,253,375,989.00** fedha za nje kuendeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kupanda miti kwenye eneo la hekta 4,500 katika Mashamba ya Miti ya Mtibwa (hekta 500), Silayo (hekta 3,000) na Wino (hekta 1,000) pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara katika mashamba hayo;

(ii) Kufanya tathmini ya maeneo ya Misitu ya Mikoko yaliyopo Wilaya za Kilwa, Rufiji na Kibiti na kuandaa Mipango ya Usimamizi ya hifadhi hizo;

(iii) Kununua magari 22, mitambo 9 na kujenga vituo vya ulinzi 5 ili kuimarisha usimamizi wa maeneo ya hifadhi; na

(iv) Kuwezesha miradi ya kiuchumi, kijamii na uhifadhi wa mazingira itakayoibuliwa na jamii zinazopakana na misitu ya hifadhi.

## (J) Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project)

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 908,979,433.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuanza kwa ujenzi wa ukumbi wa mikutano na matukio; na

(ii) Kuendeleza Kituo cha Utangazaji Utalii Kidijitali kupitia mfumo wa "Travel Companion".

## (K) Mradi wa Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mradi huu utatumia fedha za ndani kiasi cha **Shilingi 1,654,595,091.00** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma kwenye Kampasi ya Arusha. Jengo hilo litakuwa na miundombinu ya madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 kwa wakati mmoja, kumbi za mihadhara, kumbi za mikutano na vifaa vya mafunzo vikiwemo majiko, chumba cha kufulia, mgahawa na vyumba vya wageni.

## (L) Uanzishwaji wa makumbusho ya Marais, Dodoma

Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani na kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 utatumia **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Makumbusho ya Marais, jijini Dodoma.

## (M) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi Makao Makuu ya TAWIRI

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Nchini (TAWIRI) katika kuimarisha mazingira rafiki ya kufanyia kazi kwa watumishi, Taasisi imetengewa fedha za ndani **Shilingi 1,000,000,000.00** kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu. Jengo hili litakuwa na miundombinu ya Ofisi za watumishi, maabara za wanyamapori na kumbi za mikutano.

## (N) Miradi ya TANAPA

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) litatumia kiasi cha **Shilingi 18,489,000,000.00** fedha za nje ili kutekeleza shughuli zifuatazo: -

(i) Ukarabati wa mradi wa usambazaji maji wa Naabi; uchimbaji wa visima sita lango la Ndabaka, uwanja wa ndege wa Lobo, ofisi ya Mkuu wa Hifadhi, Makoma, Mawe Meupe na uwanja wa ndege wa Kusini; pamoja na uwekaji wa mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua kwenye nyumba za Askari za Ndabaka, Kirawira A na B, Nyamuma, Kogatende, Lobo, Kuka Main Base, Naabi Hill Gate, Moru Main Base, Crater Sub-Base na Simiyu;

(ii) Ujenzi wa mabwawa nane katika wilaya za Serengeti (5) pamoja na Ngorongoro (3);

(iii) Ujenzi wa madaraja matatu (Kapilula – 1, Mongwe - 1 katika hifadhi ya Taifa Katavi pamoja na Kogatende – 1 katika hifadhi ya Taifa Serengeti);

(iv) Ujenzi wa gereji kubwa na ya kisasa katika hifadhi ya Taifa Katavi;

(v) Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa hifadhi, nyumba ya kupumzikia wageni, gereji ndogo pamoja na uzio katika vituo vya askari viwili vya Ikamba na Mabilibili katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale;

(vi) Kugharamia shughuli ya uzoeshaji wa Sokwe mtu katika hifadhi ya Taifa Milima ya Mahale;

(vii) Ujenzi wa miundombinu ya kudhibiti mwenendo wa magari ikiwemo minara ya kuimarisha mtandao kutoka TANAPA Makao Makuu kupitia Hifadhi za Taifa Arusha, Tarangire, Ziwa Manyara, Ngorongoro hadi Serengeti;

(viii) Kuunganisha mifumo ya umeme jua kwenye mfumo wa ukusanyaji mapato katika malango yote ya kuingilia na kutokea wageni katika Hifadhi ya Taifa Serengeti;

(ix) Ununuzi wa magari mawili kwa ajili ya kuwezesha shughuli za tathmini na ufuatiliaji wa mradi;

(x) Ujenzi wa jengo la "control room" kubwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenengo wa magari ndani ya Hifadhi ya Taifa Serengeti; na

(xi) Kuwezesha uandaaji mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 32 vilivyopo jirani na hifadhi katika wilaya za Bariadi (18), Bunda (7) na Tarime (7).

## (O) Miradi ya TAWA

Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori itatumia kiasi cha **Shilingi 17,004,877,017.00** ambapo kiasi cha **Shilingi 7,487,896,003.00** ni fedha za

ndani na **Shilingi 9,516,981,014.00** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa vivuko 96 katika Pori la Akiba Selous kanda ya Kingupira na Liwale;

(ii) Ujenzi wa madaraja mawili ya Lungónya Kanda ya Kingupira (1) na Matandu Kanda ya Miguruwe (1) katika Pori la Akiba Selous;

(iii) Ujenzi wa bweni la watumishi katika Pori la Akiba Selous kanda ya Miguruwe;

(iv) Kuwezesha ununuzi wa mafuta ya ndege pamoja na matengenezo ya mara kwa mara ya ndege katika Pori la Akiba Selous-Miguruwe;

(v) Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo GPS 80, ndege nyuki 6 na Kamera kwa ajili ya Mapori ya Akiba Selous na Lukwika Lumesule;

(vi) Ununuzi wa magari ya doria 14 kwa ajili ya Mapori ya Akiba Selous (10) na Lukwika Lumesule (4) na gari maalum moja (1) kwa ajili ya shughuli za uhamasishaji na utoaji elimu kwa Pori la Akiba Selous;

(vii) Ujenzi wa kilomita 197 za barabara katika Mapori ya Akiba Mpanga Kipengere (30), Rukwa (17), na Wami-Mbiki (150);

(viii) Ununuzi wa magari sita (6), boti 1, trekta 1, pikipiki 16, engine 10 za boti pamoja na ununuzi wa samani kwa ajili ya ofisi sita (6) za Mapori ya Akiba Maswa, Uwanda, Mpanga Kipengere, Igombe, Moyowosi na Pori Tengefu Ziwa Natron; na

(ix) Ujenzi wa ofisi ya Kanda ya Magharibi kwa ajili ya Mapori ya Akiba ya Rukwa, Ugalla na Inyonga.

## 6.0 SHUKRANI

**295.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuchukua fursa hii tena kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa miongozo, maelekezo na msukumo anayotupatia katika Sekta ya Maliasili na Utalii ambayo imeiwezesha sekta hii kuendelea kukua, kuimarika na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Pia, natumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

**296.** ***Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mailiasili na Utalii kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa ushauri na usimamizi madhubuti wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru Wakurugenzi wa Idara na Wakuu wa Vitengo vya Wizara; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa ushirikiano wanaonipa na kujituma bila kuchoka katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya kila siku. Asanteni sana na *Kazi Iendelee*.

**297.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa Wizara yetu ikiwa ni pamoja na Washirika mbalimbali wa Maendeleo, kwa mchango wao mkubwa katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Mchango wao umeendelea kuimarisha juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuwaletea wananchi maendeleo endelevu.

**298.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi marafiki, Jumuiya za Kikanda, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali pamoja na wadau wengine wakiwemo Sekta Binafsi kwa mchango wao mkubwa katika kukuza na kuendeleza Sekta ya Maliasili, Malikale na Utalii. Ushirikiano wao umeendelea kuwa kichocheo muhimu cha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa letu. Vilevile, nazishukuru kwa dhati Serikali za Canada, China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya kwa kuendelea kushirikiana nasi.

**299.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia fursa hii kuyashukuru na kuyatambua Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambazo zimeendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha Sekta ya Maliasili na Utalii. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na: EU, AfDB, AWF, AWHF, ENABEL, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, RTI, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UN-Tourism, IORA, USAID, Honey Guide Foundation, CIFOR, ICRAF, INBAR, GATSBY, FOREST- FARM FACILITY, SIX RIVERS, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Mchango wao umeendelea kuwa muhimu katika kulinda na kuendeleza rasilimali zetu kwa manufaa ya Taifa.

**300.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru wadau wote wa ndani wa Sekta ya Maliasili na Utalii wakiwemo: TCT, TATO, HAT, TAHOA, TLTO, TTGA, KGA, NTSGS, IGS, TGS, KTGA, NGTF, KPA, TPO, TACTO, TAOA, TAHA, TAWTO, TWEA, CWMAC, TABEDO, TAF, TTGAU, API-SUPPORT, HEAT, SHIVIMITA, Nature Tanzania na wadau wote wanaoshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale, uendelezaji na utangazaji utalii ikiwemo ofisi zetu za Ubalozi nje ya Nchi.

**301.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutambua mchango wa Viongozi wetu wa Dini na Viongozi wa Kimila katika kuelimisha jamii, kusimamia na kushiriki kikamilifu katika juhudi za uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi yetu zikiwemo wanyamapori, misitu na malikale. Viongozi hawa wamekua mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii kulinda na kuhifadhi maliasili za Taifa letu, kuzuia ujangili, ukataji holela wa miti, uharibifu wa malikale pamoja na kuhimiza utalii wa ndani unaozingatia mila, desturi na utunzaji wa mazingira. Kwa upande mwingine, natambua mchango mkubwa unaotolewa na wenzetu wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Shule za Sekondari na Msingi kwa namna walivyojikita katika utunzaji wa rasilimali za misitu na nyuki kwa kuanzisha vitalu vya miti na miradi ya ufugaji nyuki katika maeneo yao. Vilevile, natambua mchango wa taasisi za tafiti kwa namna zinavyoshirikiana na Wizara kutafuta suluhisho la changamoto mbalimbali zinazokabili sekta ya Maliasili na Utalii.

**302.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee, navishukuru vyombo vya ulinzi na usalama, Taasisi za Himasheria pamoja na vyombo vya habari kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu. Aidha, ninapenda kuwashukuru Wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji Utalii.

**303.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ninawahakikishia kuwa Wizara inatambua na kuthamini mchango wenu na itaendelea kuimarisha na kufungua milango ya ushirikiano zaidi kwa maendeleo ya sekta yetu na Taifa kwa ujumla.

**304.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kwa mara nyingine kuzishukuru Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika utekelezaji wa majukumu yetu katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji Utalii na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

## 7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/2026

**305.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara iweze kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 359,982,271,000.00** kwa matumizi ya Fungu 69 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 254,232,349,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 105,749,922,000.00** ni za Miradi ya Maendeleo.

**306.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 130,709,054,000.00** za Mishahara na **Shilingi 123,523,295,000.00** za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 32,476,051,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 73,273,871,000.00** fedha za nje.

## 8.0 HITIMISHO

**307.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa rai kwa Watanzania wote kuendelea kushiriki katika uhifadhi wa Maliasili, Malikale na uendelezaji wa Utalii. Aidha, ninaomba tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

**308.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.maliasili.go.tz

**309.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

# ORODHA YA VIAMBATISHO

**Jedwali Na. 1:** Maduhuli ya Wizara kwa mwaka 2023/2024 na Makusanyo kwa Mwaka 2024/2025

| Wizara/ Taasisi | Makusanyo kwa mwaka 2023/2024 | Makadirio kwa mwaka 2024/2025 | Makusanyo hadi Aprili, 2025 | % |
|---|---|---|---|---|
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
| **A: Maduhuli yaliyokusanywa kupitia Mfumo wa *MNRT Portal*** | | | | |
| Wizara | 11,000,000,000 | 11,000,000,000 | 10,066,026,247.07 | 91.51 |
| Taasisi | 189,363,068,234 | 202,419,063,000 | 172,099,754,869.20 | 85.02 |
| **JUMLA** | **200,363,068,234** | **213,419,063,000** | **182,165,781,116.27** | **85.36** |
| **B: Maduhuli ya Taasisi za Wizara (TANAPA, NCAA na TAWA) yaliyowasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia TRA** | | | | |
| TANAPA | 339,115,231,823 | 430,864,198,480 | 433,612,732,617.63 | 100.64 |
| NCAA | 155,400,000,000 | 230,000,000,000 | 231,186,145,522.22 | 100.52 |
| TAWA | 78,390,387,647.92 | 94,558,757,000 | 65,935,682,043.68 | 69.73 |
| **Jumla Ndogo** | **572,905,619,470.92** | **755,422,955,480** | **730,734,560,183.53** | **96.73** |
| **JUMLA KUU** | **773,268,687,704.92** | **968,842,018,480** | **912,900,341,299.80** | **94.23** |

* *Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 2**: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

| Na. | Idara/ Taasisi | Fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2024/2025 | Makadirio kwa Mwaka 2025/2026 |
|---|---|---|---|
| **I: Mfuko Mkuu wa Serikali** | | | |
| 1 | Utawala | 7,000,000 | 7,000,000 |
| 2 | Utalii | 10,943,000,000 | 12,943,000,000 |
| 3 | Mambo ya Kale | 50,000,000 | 50,000,000 |
| 4 | TAWA | 94,558,757,000 | 100,536,198,276.65 |
| | **Jumla Ndogo** | **105,558,757,000** | **113,536,198,276.65** |
| **II: Taasisi zinazokusanya na kutumia** | | | |
| 1 | TAWIRI | 3,276,299,600 | 3,650,000,000 |
| 2 | CAWM | 7,997,383,503 | 8,256,635,466.16 |
| 3 | PWTI | 2,988,800,219 | 2,990,167,719 |
| 4 | CBCTC | 1,597,604,000 | 1,115,199,000 |
| 5 | TAFORI | 1,015,610,000 | 1,037,500,000 |
| 6 | FTI | 1,526,400,000 | 1,800,000,000 |
| 7 | BTI | 586,290,000 | 753,090,000 |
| 8 | FITI | 980,000,000 | 1,148,325,000 |
| 9 | TTB | 1,720,000,000 | 2,000,000,000 |
| 10 | NCTA | 3,729,747,117 | 3,830,231,909 |
| 11 | NMT | 1,404,382,561 | 1,600,000,000 |
| 12 | TFS | 175,596,546,000 | 181,760,670,000 |
| 13 | TANAPA | 430,864,198,480 | 600,106,097,959.74 |
| 14 | NCAA | 230,000,000,000 | 260,000,000,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **863,283,261,480** | **1,070,047,917,053.9** |
| | **Jumla (I + II)** | **968,842,018,480** | **1,183,584,115,330.55** |

**Jedwali Na. 3:** Mwenendo wa Utalii Nchini kuanzia Mwaka wa Fedha 2020 hadi 2024

| **Mwaka** | | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watalii wa kimataifa | | 620,867 | 922,692 | 1,454,920 | 1,808,205 | 2,141,895 |
| Watalii wa Hotelini | | 563,779 | 848,936 | 1,365,861 | 1,710,333 | 1,990,697 |
| Mapato (Dola za Kimarekani - Milioni) | | 714.5 | 1,310.34 | 2,527.77 | 3,373.83 | 3,903.06 |
| Wastani wa siku za Mtalii kukaa Nchini | | 10 | 10 | 9 | 10 | 10 |
| Wastani wa matumizi ya fedha kwa Mtalii kwa Siku (Dola za Kimarekani) | Safari za Vifurushi | 312 | 364 | 377 | 419 | 416 |
| | Safari zisizo za Vifurushi | 115 | 141 | 166 | 178 | 172 |

**Jedwali Na. 4:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| **Na.** | **Mwaka wa Fedha** | **Watalii wa Nje** | **Watalii wa Ndani** | **Jumla ya Watalii** | **Mapato (Shilingi)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2020/2021 | 72,632 | 118,982 | 191,614 | 31,426,077,258 |
| 2. | 2021/2022 | 228,810 | 196,576 | 425,386 | 91,131,434,281 |
| 3. | 2022/2023 | 458,351 | 293881 | 752,232 | 171,322,125,734 |
| 4. | 2023/2024 | 553,875 | 354,752 | 908,627 | 219,547,542,813 |
| 5. | 2024/2025* | 556,246 | 368,917 | 925,163 | 231,186,145,522.22 |
| | **Jumla** | **1,869,914** | **1,333,108** | **3,203,022** | **744,613,325,608.22** |

* *Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 5:** Mwenendo wa Uwindaji wa Kitalii na Mapato Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Na. | Mwaka | Idadi ya Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Wawindaji** | **Watazamaji *(Observers)*** | **Jumla** | |
| 1. | 2020/2021 | 355 | 255 | 610 | 24,945,979,320.00 |
| 2. | 2021/2022 | 531 | 313 | 844 | 49,535,183,266.00 |
| 3. | 2022/2023 | 580 | 207 | 787 | 47,504,406,125.31 |
| 4. | 2023/2024 | 649 | 646 | 1,295 | 54,605,249,171.43 |
| 5. | 2024/2025* | 554 | 534 | 1,088 | 44,465,795,425.70 |
| | **Jumla** | **2,669** | **1,955** | **4,624** | **221,056,613,308.44** |

**Jedwali Na. 6:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Mapori ya Akiba na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

*Hadi Aprili, 2025

| Na. | Mwaka | Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Nje** | **Ndani** | **Jumla** | |
| 1. | 2020/2021 | 26,854 | 10,830 | 37,684 | 3,399,960,437.84 |
| 2. | 2021/2022 | 109,674 | 48,434 | 158,108 | 9,940,367,816.68 |
| 3. | 2022/2023 | 123,840 | 43,124 | 166,964 | 12,940,469,659.54 |
| 4. | 2023/2024 | 114,218 | 68,213 | 182,431 | 21,356,483,179.75 |
| 5. | 2024/2025* | 133,145 | 76,377 | 209522 | 21,469,886,617.98 |
| | **Jumla** | **507,731** | **246,978** | **754,709** | **69,107,167,711.79** |

***Hadi Aprili, 2025**

**Jedwali Na. 7:** Mwenendo wa Upandaji Miti katika Mashamba ya Miti Kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Na. | Jina la Shamba | Ukubwa wa Shamba (Hekta) | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025* | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lililopandwa (Hekta) | | | | |
| 1 | Buhigwe | 1,383 | 130 | 126 | 57 | 186 | 121 | 620 |
| 2 | Buhindi | 21,880 | 495 | 504 | 258.6 | 227 | 200 | 1,684 |
| 3 | Iyondo Mswima | 2,935 | 175 | 101 | 102 | 100 | 76 | 554 |
| 4 | Kawetire | 5,182 | 62 | 78 | 70.58 | 27 | 39 | 277 |
| 5 | Kiwira | 2,820 | 87 | 136 | 182 | 217 | 208 | 830 |
| 6 | Korogwe | 10,276 | 108 | 0 | 98 | 89 | 15 | 310 |
| 7 | Longuza | 7,067 | 133 | 223 | 218 | 182 | 303.2 | 1,059 |
| 8 | Makere Kusini | 65,178 | 173 | 334 | 611 | 544 | 372 | 2,034 |
| 9 | Mbizi | 23,824 | 249 | 123 | 130 | 80 | 108 | 690 |
| 10 | Meru | 8,195 | 180 | 258 | 286 | 310 | 346 | 1,380 |
| 11 | Morogoro | 12,950 | 263 | 220 | 185 | 189 | 87 | 944 |
| 12 | Mpepo | 20,905 | 500 | 0 | 470 | 320 | 103 | 1,393 |
| 13 | Mtibwa | 16,109 | 97 | 166.5 | 211 | 141 | 95 | 711 |
| 14 | North Kilimanjaro | 8,069 | 155 | 201 | 249.5 | 236 | 224 | 1,066 |
| 15 | North Ruvu | 1,926 | 170 | 42 | 142 | 102 | 100 | 556 |
| 16 | Rondo | 31,930 | 154 | 207 | 201 | 13 | 100 | 675 |
| 17 | Rubare | 2,979 | 0 | 36 | 22 | 44 | 23 | 125 |
| 18 | Rubya | 6,374 | 72 | 76 | 113 | 75 | 94 | 430 |
| 19 | Sao Hill | 135,903 | 2,793 | 2,761 | 3,355 | 2,960 | 4,235 | 16,104 |

| Na. | Jina la Shamba | Ukubwa wa Shamba (Hekta) | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 | 2023/2024 | 2024/2025* | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Eneo lililopandwa (Hekta) | | | | |
| 20 | Shume | 4,863 | 174 | 161 | 255 | 204 | 113 | 907 |
| 21 | Silayo | 69,756 | 825 | 1200 | 1101 | 523 | 685 | 4,334 |
| 22 | Ukaguru | 3,127 | 230 | 210 | 63 | 26 | 0 | 529 |
| 23 | West Kilimanjaro | 7,632 | 160 | 144 | 393.9 | 256 | 401 | 1,355 |
| 24 | Wino | 39,400 | 428 | 509 | 440.5 | 503 | 222 | 2,103 |
| | **Jumla Kuu** | **510,663** | **7,813** | **7,817** | **9,215** | **7,554** | **8,270** | **40,669** |

** Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 8:** Mauzo ya Asali na Nta Nje ya Nchi kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Na. | Mwaka | Asali | | Nta | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Tani | Thamani (Shilingi) | Tani | Thamani (Shilingi) |
| 1. | 2020/2021 | 1,988 | 19,878,220,000 | 393 | 6,489,999,500 |
| 2. | 2021/2022 | 1,562.93 | 15,629,295,500 | 747.56 | 14,951,148,000 |
| 3. | 2022/2023 | 1,199 | 14,397,780,000 | 479 | 7,185,000,000 |
| 4. | 2023/2024 | 951.62 | 11,419,488,000 | 458.14 | 6,675,405,000 |
| 5. | 2024/2025* | 1,321.35 | 15,856,164,000 | 314.73 | 4,720,965,000 |
| | **Jumla** | **7,022.9** | **77,180,947,500** | **2392.43** | **40,022,517,500** |

** Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 9:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Misitu ya Mazingira Asilia na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Na. | Mwaka | Watalii wa Nje | Watalii wa Ndani | Jumla ya Watalii | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2020/2021 | 4,348 | 55,258 | 59,606 | 154,965,050 |
| 2. | 2021/2022 | 17,141 | 134,861 | 152,002 | 609,794,840 |
| 3. | 2022/2023 | 31,141 | 211,833 | 242,974 | 1,377,993,865 |
| 4. | 2023/2024 | 33,713 | 223,849 | 257,542 | 1,689,095,459 |
| 5. | 2024/2025* | 36,642 | 240,081 | 276,723 | 2,169,832,146 |
| | **Jumla** | **122,985** | **865,882** | **988,847** | **6,001,681,360** |

** Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 10:** Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Na. | Mwaka | Watalii | | | Mapato (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nje | Ndani | Jumla | |
| 1. | 2020/2021 | 153,389 | 358,500 | 511,889 | 56,979,796,789 |
| 2. | 2021/2022 | 412,480 | 594,029 | 1,006,509 | 174,715,158,494 |
| 3. | 2022/2023 | 812,241 | 858,196 | 1,670,437 | 337,424,076,896.29 |
| 4. | 2023/2024 | 958,559 | 904,549 | 1,863,108 | 410,903,648,082.30 |
| 5. | 2024/2025* | 938,338 | 347,538 | 1,285,876 | 433,612,977,617.63 |
| | **Jumla** | **3,275,007** | **3,062,812** | **6,337,819** | **1,413,635,657,879** |

** Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 11:** Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Malikale na Mapato kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025

| Kituo | 2020/2021 | | 2021/2022 | | 2022/2023 | | 2023/2024 | | 2024/2025* | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** |
| Bonde la Olduvai | 6,269 | 178,585,353.60 | 12,391 | 799,696,715.00 | 21,803 | 1,576,084,868.60 | 26,230 | 2,258,334,268.00 | 24,155 | 1,966,138,514.40 |
| Laetoli | 9 | 0 | 63 | 7,664,157.00 | 74 | 3,984,789.20 | 92 | 6,241,834.20 | 148 | 3,756,010.80 |
| Magofu ya Kaole | 21,259 | 39,857,800 | 36,951 | 20,249,000 | 36,640 | 71,279,380 | 40,517 | 80,520,000 | 39,080 | 79,761,260 |
| Zama za Mawe Isimila | 6,823 | 14,866,924.5 | 10,485 | 25,192,935 | 7,266 | 22,841,393 | 5.835 | 23,088,780 | 5,439 | 22,229,400 |
| Mji Mkongwe - Bagamoyo | 9,573 | 21,162,000 | 22,788 | 11,779,730 | 18,229 | 52,688,030 | 17,633 | 52,805,000 | 17,480 | 53,883,610 |
| Makumbusho Ya Mkwawa – Kalenga | 3,672 | 5,966,730 | 6,004 | 8,977,935 | 5,049 | 8,685,870 | 6,706 | 12,917,040 | 17,778 | 31,143,400 |
| Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara | 4,040 | 27,563,500 | 5,993 | 34,911,550 | 6,370 | 66,024,402 | 6,983 | 91,102,950 | 4,904 | 111,846,890 |
| Kimondo cha Mbozi | 3,726 | 11,252,480 | 2,143 | 5,654,360 | 5,204 | 8,033,318 | 2,902 | 5,360,620 | 2,159 | 4,046,220 |
| Mapango ya Amboni | 8,434 | 18,692,280 | 14,042 | 30,373,200 | 14,716 | 30,368,480 | 17,694 | 35,243,060 | 15,004 | 31,831,740 |
| Magofu ya Tongoni | 192 | 373,000 | 174 | 239,000 | 449 | 1,043,500 | 458 | 850,000 | 850 | 1,227,500 |
| Dkt. Livingstone Ujiji, Kigoma | 3,027 | 6,876,475 | 32,486 | 66,815,780.00 | 4,336 | 17,099,478 | 4,974 | 18,365,680 | 3,838 | 12,686,680 |

| Kituo | 2020/2021 | | 2021/2022 | | 2022/2023 | | 2023/2024 | | 2024/2025* | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** | **Wageni** | **Mapato** |
| Tembe la Kwihara | 392 | 338,000 | 419 | 708,000 | 1,212 | 1,810,840 | 771 | 1,626,700 | 797 | 2,931,295 |
| Michoro ya Miambani Kondoa, Kolo | 2,316 | 9,407,000 | 5,990 | 10,495,162 | 5,665 | 26,588,500 | 6,849 | 28,151,860 | 4,847 | 24,429,005 |
| Makumbusho ya Caravan Serai, Bagamoyo | 2,190 | 3,478,000 | 5,186 | 9,347,000 | 5,409 | 13,765,060 | 5,975 | 14,325,300 | 4,797 | 11,223,400 |
| Nyumba Kumbukizi ya Mwl. Nyerere – Magomeni | 181 | 283,000 | 1,226 | 2,160,580 | 470 | 1,858,500 | 1,211 | 2,630,220 | 611 | 1,700,380 |
| Magofu ya Engaruka | 28 | 293,520 | 177 | 434,180 | 154 | 464,921 | 77 | 879,100 | 80 | 713,900 |
| Magofu ya Kunduchi | 45 | 22,500 | 2,343 | 3,087,807 | 5,557 | 6,465,000 | 2,998 | 4,812,000.00 | 2,307 | 4,460,840 |
| **Jumla** | **72,176** | **339,018,563.1** | **158,861** | **1,037,787,091** | **138,603** | **1,909,086,329.8** | **142,076** | **2,637,254,412.2** | **144,274** | **2,364,010,045.2** |

* *Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 12:** Idadi ya Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa na Mapato Kuanzia Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi 2024/2025

| Mwaka | 2022/2023 | | | | 2023/2024 | | | | 2024/2025* | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kituo | Wageni | | | Mapato | Wageni | | | Mapato | Wageni | | | Mapato |
| | Nje | Ndani | Jumla | | Nje | Ndani | Jumla | | Nje | Ndani | Jumla | |
| Nyumba ya Utamaduni | 7,800 | 159,381 | 167,181 | 470,069,263.40 | 10,714 | 149,996 | 160,710 | 361,648,650 | 8,695 | 124,469 | 133,164 | 503,735,019.00 |
| Kijiji cha Makumbusho | 3,426 | 635,582 | 639,008 | 239,458,300 | 5,972 | 122,120 | 128,092 | 509,004,780.84 | 4,697 | 128,104 | 132,801 | 501,560,170.84 |
| Azimio la Arusha | 146 | 1,259 | 1,405 | 19,265,400 | 446 | 19,042 | 19,042 | 24,900,200 | 469 | 8,862 | 9,331 | 39,958,700.00 |
| Vita vya Majimaji | 71 | 2,340 | 2,441 | 47,611,200 | 68 | 14,797 | 14,865 | 18,188,500 | 86 | 4,852 | 4,938 | 20,817,559.00 |
| Mwl. Nyerere – Butiama | 60 | 5,008 | 5,068 | 38,325,300 | 98 | 13,315 | 13,413 | 69,796,300 | 37 | 9,850 | 9,887 | 18,366,406.16 |
| Makumbusho ya Elimu Viumbe | 2,445 | 38,536 | 40,981 | 71,284,290 | 3,048 | 33,535 | 36,583 | 98,553,675 | 3,584 | 15,946 | 19,530 | 99,667,356 |
| Dkt. Rashid M. Kawawa | 9 | 3,321 | 3,330 | 2,372,900 | 18 | 1,339 | 1,357 | 1,698,300 | - | 417 | 417 | 701,800 |
| Mji Mkongwe – Mikindani | 4 | 4,293 | 4,297 | 3,835,500 | 24 | 3,065 | 3,089 | 4,189,000 | - | 1,980 | 1,980 | 2,935,384 |
| **JUMLA** | **13,841** | **908,476** | **922,317** | **892,222,153.40** | **20,388** | **357,209** | **377,597** | **1,087,979,405.84** | **17,568** | **294,480** | **312,048** | **1,187,742,395.00** |

** Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 13**: Nafasi ya Tanzania kwa Idadi ya Wanyamapori Barani Afrika kwa Mwaka 2024

| Na. | Wanyamapori | Nchi Tano zinazoongoza kwa wanyamapori na idadi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1. | Tembo | Botswana 130,000 | Zimbabwe 100,000 | Tanzania 60,000 | Afrika Kusini 35,000 | Namibia 24,000 |
| 2. | Nyati | Tanzania 225,000 | Afrika Kusini 46,000 | Mozambique 45,000 | Kenya 42,000 | Zambia 41,000 |
| 3. | Simba | Tanzania 17,000 | Afrika Kusini 3,284 | Botswana 3,064 | Kenya 2,515 | Zambia 2,349 |
| 4. | Faru | Namibia 2,196 | Afrika Kusini 2,056 | Zimbabwe 1,033 | Kenya 938 | Tanzania 212 |
| 5. | Chui | Tanzania 24,000** | | | | |

*** Idadi ya Chui kwa Nchi nyingine za Afrika haipo kwa sasa.*

**Jedwali Na. 14:** Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa katika Vyuo vilivyo chini ya Wizara kuanzia Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025.

| Chuo | Wanyamapori | | | Utalii | Misitu na Nyuki | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka | CAWM-Mweka | PWTI - Pasiansi | Likuyu Seka - maganga | NCT -Utalii | FITI - Moshi | BTI -Tabora | FTI - Olmotonyi | |
| 2020/2021 | 929 | 343 | 162 | 1,087 | 224 | 408 | 867 | **4,020** |
| 2021/2022 | 834 | 410 | 204 | 1,082 | 286 | 378 | 892 | **4,086** |
| 2022/2023 | 854 | 418 | 333 | 1,045 | 310 | 372 | 869 | **4,201** |
| 2023/2024 | 1,074 | 646 | 593 | 1,229 | 358 | 394 | 840 | **5,134** |
| 2024/2025* | 1,216 | 621 | 329 | 1,398 | 388 | 287 | 934 | **5,173** |
| **Jumla Kuu** | **4,907** | **2,438** | **1,621** | **5,841** | **1,566** | **1,839** | **4,402** | **22,614** |

*Hadi Aprili, 2025*

**Jedwali Na. 15:** Muhtasari wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

| **Na.** | **Namba ya Mradi** | **Jina la Mradi** | **Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Sh.)** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Fedha za Ndani** | **Fedha za Nje** | **Jumla** | **Mhisani** |
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) |
| | **Fedha na Uhasibu** | | | | | |
| 1 | 6251 | Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP – VI) na ujenzi wa Tanzania Online Safari Booking system | 57,476,764 | 920,000,000 | 977,476,764 | WB/GoT |
| | **Jumla Ndogo** | | **57,476,764** | **920,000,000** | **977,476,764** | |
| | **Sera na Mipango** | | | | | |
| 2 | 5203 | Mradi wa Kuendeleza Utalii Kusini mwa Tanzania. | 18,682,561,593 | 0 | 18,682,561,593 | GoT |
| | | **Jumla Ndogo** | **18,682,561,593** | **0** | **18,682,561,593** | |
| | **Wanyamapori** | | | | | |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Sh.) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Fedha za Ndani** | **Fedha za Nje** | **Jumla** | **Mhisani** |
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) |
| 3 | 4810 | Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves) | 1,114,138,124 | 0 | 1,114,138,124 | GoT |
| 4 | 4812 | Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Support to Combating Wildlife Crime) | 0 | 2,586,276,000 | 2,586,276,000 | UNDP |
| | | **Jumla Ndogo** | **1,114,138,124** | **2,586,276,000** | **3,700,414,124** | |
| | **Misitu na Nyuki** | | | | | |
| 5 | 4648 | Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping) | 570,403,992 | 0 | 570,403,992 | GoT |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Sh.) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | Mhisani |
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) |
| 6 | 4651 | Programu ya Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC) | 0 | 1,842,401,666 | 1,842,401,666 | EU |
| 7 | 4630 | Mradi wa Usimamizi wa Mifumo ya Chakula, Matumizi Bora ya Ardhi na Urejeshaji wa Uoto wa Asili Tanzania (Food Systems, Land Use and Restoration in Tanzania's Landscapes – FOLUR) | 0 | 3,664,636,331 | 3,664,636,331 | EU |
| 8 | 4650 | Mradi wa Kusimamia Uhifadhi wa Misitu, Matumizi Bora ya Ardhi na Kuongeza thamani ya Mazao ya Misitu (Forestry | 0 | 4,001,200,000 | 4,001,200,000 | Finland |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Sh.) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani | Fedha za Nje | Jumla | Mhisani |
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) |
| | | Land Use and Value Chains Development in Tanzania-FORLAND) | | | | |
| | | **Jumla Ndogo** | **570,403,992** | **9,508,237,997** | **10,078,641,989** | |
| | **Utalii** | | | | | |
| 9 | 4816 | Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE-Tourism Development Project) | 908,979,433 | 0 | 908,979,433 | GoT |
| | | **Jumla Ndogo** | **908,979,433** | **0** | **908,979,433** | |
| | **Taasisi za Wizara** | | | | | |
| 10 | 4817 | Miradi ya TAWA | 7,487,896,003 | 9,516,981,014 | 17,004,877,017 | GoT & KfW |
| 11 | 4813 | Miradi ya TANAPA | 0 | 18,489,000,000 | 18,489,000,000 | KfW |
| 12 | 4342 | Kujenga Uwezo na Kuimarisha Chuo cha Taifa cha Utalii | 1,654,595,091 | 0 | 1,654,595,091 | GoT |
| 13 | 6389 | Ujenzi wa Jengo la Ofisi | 1,000,000,000 | 0 | 1,000,000,000 | GoT |
| 14 | 5221 | Uanzishwaji wa makumbusho ya | 1,000,000,000 | 0 | 1,000,000,000 | GoT |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Fedha zinazoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Sh.) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Fedha za Ndani** | **Fedha za Nje** | **Jumla** | **Mhisani** |
| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) |
| | | Marais, Dodoma | | | | |
| 15 | 4634 | Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mashamba ya Miti ya Serikali na Uhifadhi wa Misitu ya Mikoko | 0 | 32,253,375,989 | 32,253,375,989 | Ufaransa |
| | | **Jumla Ndogo** | **11,142,491,094** | **60,259,357,003** | **71,401,848,097** | |
| | | **JUMLA KUU** | **32,476,051,000** | **73,273,871,000** | **105,749,922,000** | |

**Jedwali Na. 16:** Muhtasari wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

| Maelezo | | | Bajeti 2025/2026 |
|---|---|---|---|
| 1. | Matumizi ya Kawaida | Mishahara | 130,709,054,000 |
| | | Matumizi Mengineyo | 123,523,295,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **254,232,349,000** |
| 2. | Matumizi ya Maendeleo | Ndani | 32,476,051,000 |
| | | Nje | 73,273,871,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **105,749,922,000** |
| **Jumla Kuu** | | | **359,982,271,000** |




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akipanda mti wa asili aina ya Mkangazi katika Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa Mkoani Njombe.*



*Katibu Mkuu wa Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism), Bw. Zurab Pololikashvili, akiwa pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), alipotembelea Hifadhi ya Taifa Arusha wakati wa Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Vyakula la Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) kwa Kanda ya Afrika.*



*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) akiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakati wa ziara ya kutembelea Hifadhi ya Wanyamapori Makuyuni iliyopo Wilayani Monduli Mkoani Arusha.*




*Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akiwa na Naibu Waziri, Mhe. Dunstan Kitandula (Mb), Naibu Katibu Mkuu (Utalii), Bw. Nkoba Mabula na baadhi ya watendaji wa Wizara, katika maandalizi ya Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Vyakula la Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) Kanda ya Afrika lililofanyika jijini Arusha.*



*Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula (Mb) akiwa ziarani katika Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi Mwanza akikagua taswira za wanyamapori za kufundishia.*




*Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi akipokea Tuzo ya World Travel Awards ambayo hutambua na kusherehekea ubora katika sekta ya usafiri, utalii na ukarimu.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii anayeshughulikia Maliasili Kamishna wa Polisi Benedict Wakulyamba akitoa mafunzo ya Haki jinai kwa Askari wa Jeshi la Uhifadhi kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) wa Mikoa ya Simiyu na Mara.*



*Watalii kutoka nchi mbalimbali wakitalii Hifadhi ya Urithi wa Utamaduni wa Dunia ya Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara.*



*Maporomoko ya maji yaliyopo katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere ikiwa ni moja ya vivutio vya utalii vinavyopatikana mkoani Njombe.*



*Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi H. Chana (Mb) upande wa (kushoto) akiwa pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Dunstan Kitandula (katikati) na Mkurugenzi wa Utalii Dkt. Thereza Mugobi wakati wa Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Vyakula Duniani, Jijini Arusha.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango (katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi mbalimbali kwenye ufunguzi wa Jukwaa la Pili la Kimataifa la Utalii wa Vyakula Duniani, Jijini Arusha.*